# USAWIRI WA DAWA ZA KULEVYA KATIKA MATINI TEULE ZA FASISHI YA WATOTO YA KISWAHILI

**MBEERE CYPRIAN KITHINJI**

**Tasnifu Iliyowasilishwa katika Shule ya Mafuzu ya Chuo Kikuu cha Chuka kwa Minajili ya Kutosheleza baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili.**

**CHUO KIKUU CHA CHUKA**

**SEPTEMBA 2022**

## UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo la mwanafunzi**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya Shahada au Stashahada katika Chuo Kikuu kingine.

Sahihi ____________________ Tarehe 5/9/2022

Mbeere Cyprian Kithinji
AM12/19185/15.

**Idhini ya wasimamizi**

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini ya wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Chuka.

Sahihi ____________________ Tarehe 05/09/2022

Prof. John M. Kobia
Chuo Kikuu cha Chuka.

Sahihi ____________________ Tarehe 05/09/2022

Dakt. Allan Mugambi
Chuo Kikuu cha Chuka.

## HATILINZI

©2022

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuigwa, kunakili, kurudufisha, kuhifadhi kwa mifumo ya kieletroniki au kutoa vipengele fulani kwa namna yoyote ile bila idhini kutoka kwa mwandishi na Chuo Kikuu cha Chuka.

## TABARUKU

Kazi hii naitabarukia wanangu Mike Munene, Joy Gatwiri na Ken Muthomi.

## SHUKRANI

Kwanza, namshukuru Mola kwa kunijalia uwezo, busara na ustahimilivu katika shughuli zangu zote, katika masomo yangu na hasa katika utafiti huu wa shahada ya Uzamili. Pili, natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi Profesa John M. Kobia na Daktari Allan Mugambi kwa ushauri wao muhimu ambao uliniongoza katika utafiti huu kutoka mwanzo hadi mwisho. Tulipokuwa tunawasiliana, mlinitia moyo wa kuendelea na shughuli za utafiti hasa wakati nilikuwa ninahisi ninalemewa. Ahsanteni, Maulana awabariki.

Natoa shukrani kwa walimu wangu Profesa John M. Kobia, Dkt. Allan Mugambi, Bw. Kimathi Muembu, Bw. Enock Matundura, Bw. Sebastian Mbogo na Bw. Mutahi Miricho. Ahsanteni kwa kozi ambazo mlinifunza zilichangia pakubwa kunitia hamu ya kuendelea na masomo. Siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu wapendwa tulioshirikiana nao na kutiana moyo katika kozi zetu. Shukrani kwenu: Magdaline, Mutwiri, Irene na Faith.

Nawashukuru wote walionisaidia kupiga chapa kazi hii na kuikosoa Bw. Dan Chabari, Bw. Kirema Josphat na Bw. Domenic Mukwa, Mungu awabariki. Mwisho, shukrani zangu zimwendee mke wangu Deborah Gatiria na watoto wangu Mike, Joy na Ken kwa kunitia moyo kuendelea hata wakati kazi ilikuwa ngumu. Wote waliochangia kwa vyovyote vile ufanisi wa utafiti Mungu awabariki.

**IKISIRI**

Utafiti huu ulichunguza usawiri wa dawa za kulevya katika matini teule za Fasihi ya watoto ya Kiswahili. Utafiti ulilenga kufafanua matumizi ya taswira kusawiri matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule, kueleza athari za matumizi ya dawa za kulevya na kutathimini mielekeo ya watoto kuhusu dawa za kulevya katika matini teule za Fasihi ya watoto ya Kiswahili. Malengo haya yalitimizwa kwa kuchanganua matini tatu: *Vioja vya Musa*, *(*Mogambi, 2007*), Atamlilia nani? (Mohamed, 2009)*, na *Ah! Ajizi (Nyambeka, 2015).* Uteuzi wa sampuli wa maksudi ulitumika kuteua vitabu husika kawa kuwa ni vya fasihi ya watoto, vilivyo andikwa na wataalamu tofauti, vikachapishwa miaka tofauti na kusheheni data toshelevu kuhusu dawa za kulevya. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani na Nyanjani. Maktabani, matini teule Pamoja na machapisho mengine yaliyofaidi utafiti huu yalichambuliwa. Uchambuzi wa matini ulichangia kupata data ya malengo ya Matumizi ya taswira kusawiri matumizi ya dawa za kulevya na kuelezea athari za dawa za kulevya. Nyanjani wasailiwa sita kutoka kila shule tatu, moja kutoka kila lokesheni, Nkondi, Matakiri na Mwanyani za Tarafa ya Nkondi Wilayani Tharaka Kusini, Gatuzi la Tharaka Nithi walihojiwa kutathimini mielekeo wa watoto kuhusu dawa za kulevya. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji. Mihimili ya Mwitikio wa Msomaji iliongoza uchambuzi wa malengo ya utafiti katika matini teule. Data iliyopatikana ilichanganuliwa kwa njia elezi na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo na jedwali. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa taswira hutumika kusawiri dawa za kulevya, dawa za kulevya huwa na athari kwa watoto na watumiaji wengine. Matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa kuwa yataongezea maarifa katika taaluma ya kielimu katika Uchanganuzi wa fasihi ya watoto, kuwafaidi wasomi na wahakiki kuhusu usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya katika fasihi ya watoto. Matokeo ya utafiti huu yatafaidi wizara ya elimu wanaotayarisha mitaala kuhusisha dawa za kulevya katika mtaala wa Elimu. Washikadau kama walimu, wazazi na viongozi wanaweza kutumia matokeo ya utafiti huu kuwashauri watoto kuhusu athari za dawa za kulevya. Wahakiki wa kazi za kifasihi wanafaidi matokeo ya utafiti huu kwa kuelewa matumizi ya nadharia ya Mwitikio wa Msomaji katika Fasihi ya watoto ya Kiswahili.

## ABSTRACT

This research sought to analyse three selected Kiswahili literary texts meant for children with an aim of showing how they portray drug abuse in children's literature. The objectives of the research were to identify the imageries used by writers of the selected texts to portray drug abuse, to discuss the effects of drug abuse as portrayed in children's Literature and to assess the children's perception towards drug abuse. These objectives were achieved by analysing the selected texts: *Vioja vya Musa (Mogambi, 2007), Atamlilia nani? (Mohamed, 2009) and Ah! Jizi (Nyambeka, 2015).* These texts were selected because they contained substantial information on drug abuse, they were written by different authors and published in different years. These texts were analysed to identify the imageries used to potray drug abuse and discuss effects of drug abuse which are objectives one and two. In order to achieve objective three children's perception on drug abuse, six different learners were sampled from each of the 3 schools. One from each location: Nkondi, Matakiri and Mwanyani in Nkondi Division, in Tharaka South Sub-County in Tharaka Nithi County. In selecting the texts and learners purposeful sampling was employed. The learners were expected to read the selected texts, answer a questionnaire based on Likert Scale and discuss on given questions in focus groups for the researcher to assess their perception on drug abuse. This research was guided by the Reader Response Theory whose tenets were used to analyse the selected texts based on the objectives. Descriptive method of data analysis and presentation was used. The research findings indicated that imageries were used to portray drug abuse, the texts portray effects of drug abuse and the respondents' percpeption towards drug abuse was positive. It's hoped that the findings of this study contribute to scholary Literature in Literary critics and works on portrayal of drug abuse in children's Literature in providing additional information to already existing knowledge in portrayal of drug abuse in children's literature. Furthermore, these findings can help the reader to understand the imageries as guided by stylistic devices and responses for the Children's Literature. The research findings will be of great use to parents, Educationists and researchers in getting more additional information on portrayal of drug abuse in children's Literature. The researchers and critics of the literary texts in children's Literature will understand the use of Reader Response Theory in portrayal of drug abuse in children's Literature.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI** ..... **ii**

**HATILINZI** ..... **iii**

**TABARUKU** ..... **iv**

**SHUKRANI** ..... **v**

**IKISIRI** ..... **vi**

**ABSTRACT** ..... **vii**

**YALIYOMO** ..... **viii**

**ORODHA YA MAJEDWALI** ..... **xi**

**MAELEZO YA ALAMA NA VIFUPISHO** ..... **xii**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ..... **1**

1.1 Usuli wa Mada ..... 1

1.2 Suala la Utafiti ..... 4

1.3 Malengo ya Utafiti ..... 5

1.4 Maswali ya Utafiti ..... 5

1.5 Umuhimu wa Utafiti ..... 5

1.6 Sababu za Kuchagua Mada ..... 6

1.7 Upeo wa Utafiti ..... 6

1.8 Maelezo ya Istilahi ..... 7

**SURA YA PILI: MWAUO WA MAANDISHI** ..... **8**

2.1 Utangulizi ..... 8

2.2 Maandishi kuhusu Fasihi ya Watoto ..... 8

2.3 Dhana na Dhima ya Fasihi ya Watoto ..... 17

2.4 Dhana ya Dawa za Kulevya ..... 18

2.6 Kiunzi cha Nadharia ..... 23

2.7 Hitimisho ..... 26

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI** ..... **27**

3.1 Utangulizi ..... 27

3.2 Mpango wa Utafiti ..... 27

3.3 Uteuzi wa Sampuli ..... 27

3.4 Vifaa vya Utafiti ......................................................................................28
3.5 Ukusanyaji wa Data ...................................................................................28
3.6 Uchanganuzi wa Data ................................................................................30
3.7 Uwasilishaji wa Data .................................................................................30
3.8 Maadili ya Utafiti.......................................................................................31
3.9 Hitimisho...................................................................................................31

**SURA YA NNE: AINA ZA TASWIRA ZINAZO JIDHIHIRISHA KATIKA MATINI TEULE ZA FASIHI YA WATOTO YA KISWAHILI.......................................................32**
4.1 Utangulizi...................................................................................................32
4.2 Muhtasari wa Vioja vya Musa ...................................................................32
4.3 Muhtasari wa Atamlilia nani?....................................................................32
4.4 Muhtsari wa Ah! Ajizi ...............................................................................33
4.5 Aina za taswira zilizojidhihirisha katika matini teule.................................33
4.5.1 Taswira za Kimaelezo..............................................................................33
4.6 Taswira za Kimsingi na Kimtindo ..............................................................40
4.7 Taswira za Mnuso.......................................................................................47
4.8 Taswira za Mwonjo.....................................................................................50
4.9 Taswira ya Kiishara ...................................................................................52
4.10 Hitimisho...................................................................................................55

**SURA YA TANO: ATHARI ZA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA KWA WATOTO KATIKA MATINI TEULE ZA FASIHI YA WATOTO YA KISWAHILI ..............................56**
5.1 Utangulizi...................................................................................................56
5.1 Athari ya kutenda maovu ...........................................................................56
5.2 Aina mbalimbali za athari zilizosawiriwa katika matini Teule ..................59
5.3 Utovu wa Nidhamu .....................................................................................60
5.4 Kuathirika Kiakili na Kiuchumi..................................................................63
5.4.1 Athari ya Kiakili .......................................................................................63
5.4.2 Athari ya Kiuchumi....................................................................................65
5.5 Kuathirika Kimasomo..................................................................................65
5.6 Athari ya Kutenda Maovu na Kufungwa Jela..............................................67

5.7 Uraibu wa Mihadarati ........................................................................................69
5.8 Hitimisho..........................................................................................................71

**SURA YA SITA: MIELEKEO WA WATOTO KUHUSU DAWA ZA KULEVYA KATIKA MATINI TEULE ZA FASIHI YA WATOTO YA KISWAHILI .................................72**
6.1 Utangulizi.........................................................................................................72
6.2 Uchanganuzi wa Hojaji ya Mizani ya Likert ....................................................72
6.3 Hitimisho..........................................................................................................82

**SURA YA SABA: MUHTASARI WA UTAFITI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO .........................................................83**
7.1 Utangulizi.........................................................................................................83
7.2 Muhtasari .........................................................................................................83
7.3 Matokeo ya Utafiti ............................................................................................85
7.4 Hitimisho..........................................................................................................86
7.5. Mapendekezo ...................................................................................................87
7.5.1 Mapendekezo ya Kushughulikia athari za matumizi ya dawa za kulevya..87
7.5.2 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye ........................................................87

**MAREJELEO .........................................................................................................89**
**VIAMBATISHO .....................................................................................................95**
Kiambatisho 1: Hojaji ya Wanafunzi (Mfumo wa Likert).......................................95
Kiambatisho 2: Dodoso ya Wanafunzi ya Mjadala .................................................97
Kiambatisho 3: Kibali cha Utafiti ............................................................................98

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Ripoti ya Ulimwengu kuhusu Dawa za Kulevya kulingana na UNODC...1
Jedwali 2: Wasailiwa waliochaguliwa....28
Jedwali 3: Kauli ya kwanza: Dawa za kulevya huwa na athari nyingi kwa watoto wanaozitumia....73
Jedwali 4: Kauli ya pili: Dawa za kulevya huchangia watoto wanaozitumia kuacha shule....74
Jedwali 5: Kauli ya Tatu: Watoto uhadaiwa kuingilia dawa za kulevya bila kujua athari zake....74
Jedwali 6: Kauli ya nne: Dawa za kulevya Huchangia Utovu wa Nidhamu Shuleni 75
Jedwali 7: Kauli ya tano: Dawa za kulevya zinaweza mfanya mtumizi kufungwa jela....76
Jedwali 8: Kauli ya sita: Watoto wanaotumia Dawa za kulevya huwa ni kero kwa walimu, wanafunzi, wazazi na jamii....76
Jedwali 9: Kauli ya saba: Dawa za kulevya zina athari kubwa na zinapaswa kupigwa vita na kila mtu....77
Jedwali 10: Kauli ya 8: Kuwa dawa za kulevya huwa na uraibu....77
Jedwali 11: Kauli ya 9: Dawa za kulevya uharibu akili....78
Jedwali 12: Kauli ya 10: Dawa za kulevya huwafanya watoto kuipoteza ndoto yao ya siku za usoni....78
Jedwali 13: Kura kuhusu Kuunga Mkono, Kupinga au Kutokuwa na Hakika....80

## MAELEZO YA ALAMA NA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **AU** | : | Afican Union |
| **CAMDCCP** | : | Conference of Ministers for Drug Control and Crime Prevention |
| **KICD** | : | Kenya Institute of Curriculum Development |
| **NACADA**: | | National Authority for the Compaign against Alcohol and Drugs Abuse |
| **NPS** | : | New Psychoactive drugs |
| **NYC** | : | National Youth Council |
| **SDG** | : | Sustainable Development Goals |
| **UKIMWI** | : | Ukosefu wa kinga mwilini |
| **UNODC** | : | United Nations Office on Drugs and Crime |
| **WHO** | : | World Health Organization |

# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Suala la dawa za kulevya limekuwa na linaendelea kuwa suala nyeti na tisho kote ulimwenguni. Kulingana na ripoti ya ulimwengu kuhusu dawa (2018), dawa za kulevya zimeathiri watu wengi ulimwenguni wakubwa kwa wadogo kulingana na ripoti ya Kimataifa kuhusu dawa hizi. Matumizi ya dawa za kulevya yameendelea kusagaa kote ulimwenguni huku kukiendelea kuibuka aina mbalimbali za dawa za kulevya na soko la dawa hizi kupanuka kila kuchao. Mbinu mbalimbali za kusafirisha na kuuza dawa za kulevya kote ulimwenguni zimeibuliwa na wauzaji na wasafirishaji wa dawa za kulevya. Ulimwengu mzima unaendelea kuwapoteza watu wake na fedha nyingi a katika harakati za kupambana na walanguzi na kuwatibu waathiriwa.

Mwaka wa 2015 watu elfu 450,000 walikufa kutokana na matumizi ya dawa za kulevya. Mwaka wa 2018, kulingana na ofisi wa mataifa ya mihadarati na Jinai (UNODC), watu milioni mia mbili sabini na tano (275 milioni) walikuwa wametumia dawa za kulevya. Hii ni asilimia 5.6 ya watu ulimwenguni wenye umri wa miaka 15-64. Ripoti hii inaonyesha waathiriwa milioni 31 wanahitaji matibabu. Watoto milioni 13.8 wa umri wa miaka 15-16 ikiwa ni asilimia 5.6 wanatumia dawa za kulevya (Cannabis). Kulingana na Shirika la Afya Duniani (WHO) watu elfu 167, 750 walikufa kwa kuzidisha kipimo cha dawa za kulevya wanazozitumia. Wengine walikufa kutokana na magonjwa ya UKIMWI na *Hepatitis* C. Bangi inasababisha vifo vingi vya asilimia 76. Kuwepo na idadi kubwa ya wanaoathiriwa na dawa za kulevya na wanaoendelea kuzitumia ni jambo ambalo linahitaji kutafitiwa na kutafutiwa suluhu ili kunusuru vizazi vya leo na vya kesho. Utafiti huu unahusu usawiri wa dawa za kulevya katika matini teule za fasihi ya watoto. Katika mwaka wa 2016, kulingana na ripoti ya ulimwengu kuhusu dawa za kulevya, watu takribani milioni 308 walikuwa wakitumia aina mbali ya dawa za kulevya.

Jedwali 1: Ripoti ya Ulimwengu kuhusu Dawa za Kulevya kulingana na UNODC.

| Dawa | Kannabisi | Opiamu | Amfetamini na dawa za kisisimua | Ekastasi | Kokaini | Dawa zinazotokana na bangi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watumiaji | 182 M | 34 M | 34 M | 21 M | 18 M | 19 M |

Mamilioni ya watu wanaendelea kuathiriwa na dawa za kulevya huku matumaini ya maisha yao yakididindimia. Watu hawa hawajiwezi na huwa mzigo kwa nchi zao kuwatibu. Hili ni tisho kubwa kwa nchi ambazo hazijastawi kiuchumi. Lazima kila nchi na kila mtu apige vita dawa za kulevya. Fasihi ni njia moja inayoweza kutumiwa kuelimisha na kuhamasisha watu wakubwa kwa wadogo kuhusu matumizi ya dawa za kulevya.

Fasihi ya watoto ni dhana inayorejelea fasihi inayowalenga watoto. Kulingana na Mwanzi (1982), fasihi ya watoto huweza kuwa hadithi, ushairi, visakale na drama ambazo zimetungwa kwa ajili ya watoto wadogo. Mawazo haya yanatiliwa mkazo na Senkoro (1982) anapozungumzia juu ya uandishi wa kazi ya kifasihi. Maoni ya Senkoro ni kuwa mwandishi wa kazi ya sanaa husukumwa na yale yanayomzunguka katika maisha yake halisi katika jamii anamoishi. Mazingira yake humwathiri kwa njia moja au nyingine katika mawazo yake na maisha yake. Mazingira ya mtoto huchangia sana maisha ya kesho ya mtoto. Kazi ya mwandishi hufunza maadili na mifumo ya kijamii inayokubalika. Mwandishi kwa kutumia wahusika huelezea tabia inayokubalika katika jamii husika kwa kuonyesha kufaulu kwa mhusika mwenye nidhamu na kutofaulu au kuadhibiwa kwa mtoto au mtu mwenye tabia isiyo kubalika katika jamii.

Mwandishi huchora picha ya mambo halisi yalivyo katika jamii anamoishi kupitia kazi ya sanaa. Kwa mujibu wa Sutherland (1985), mwandishi wa fasihi ya watoto huandika yale halisi yanayowakumba watoto katika jamii kwa kuonyesha kila jamii huwa na mielekeo wao wa kimaisha. Sutherland (Keshatajwa) anasema kuwa kila mwandishi wa kazi ya Fasihi huwa na lengo la kuandikia kwa mfano kutoa maonyo katika jamii kwa kumchora mhusika mwenye vitendo visivyokubalika katika jamii yake akiadhibiwa. Hii inakuwa njia fiche ya kupinga vitendo viovu vya wanajamii. Mwandishi anapomchora mhusika wake mwenye matendo na mienendo mizuri inayokubalika huwa anafunza maadili.

Fasihi ya watoto huwatayarisha mapema kuwa watu wazima. Fasihi ya watoto ni muhimu sana kwa kupanua mawazo, akili, ukuaji na utangamano wa watoto katika jamii. Fasihi ya watoto huwatayarisha katika maisha ya usoni. Wamitila, (2008), anasema kuwa fasihi ya watoto imetumika na waandishi wengi kuathiri wasomaji walengwa ili waweze kufuata mielekeo na mienendo inayokubalika katika jamii. Lengo

moja la fasihi ya watoto likiwa ni kuadilisha. Wataalamu wa fasihi ya watoto kama vile Ohly (1985), Osazee (1991), Muriungi (2006), Matundura (2007), na Ngugi (2009), wametoa mifano ya kazi inayofaa kutekelezwa na Fasihi ya watoto. Wametoa majukumu ya Fasihi ya watoto kama vile, Kuburudisha, kuonya, kuelimisha, kuchangamsha, kukuza maadili miongoni mwa watoto katika jamii. Fasihi ya watoto hukuza utamanduni wa jamii husika na utunzaji wa mazingira. Watoto wanaweza kuyaelewa mazingira wanamoishi na kutangamana na wanajamii wengine.

Fasihi ya watoto huwa na majukumu kwa watoto. Odaga (1985), anaeleza kuwa fasihi ya watoto huwasaidia watoto kuelewa yanayotendeka mahali wanamoishi. Fasihi ya watoto huwasaidia watoto kutamalaki hulka nzuri na kuwaepusha na tabia mbaya. Huwa na maadili yanayowawezesha kukua na kuwa watu wazuri na kuheshimika siku za usoni. Anasema fasihi ni muhimu nyakati hizi vyombo vya habari vimeachwa kukidhia matakwa ya watoto kifasihi. Redio na runinga zinatumiwa kusambaza fasihi ya watoto kupitia nyimbo, mashairi, masimulizi ya hadithi, vitendawili, methali pamoja na michezo ya kuigiza. Odaga (Keshatajwa) anaeleza kuwa tangu jadi watoto wamekuwa wakifurahia fani simulizi kama; ngano, nyimbo, methali, vitendawili, mafumbo na usemi. Vipera hivi vya fasihi simulizi vina mafunzo na maelekezi muhimu ya kimaadili kwa kuwa kila mwanadamu anahitaji uelekezi mwema.

Fasihi ya watoto nchini Kenya ilianza katika miaka ya 1960. Ngugi, (2009), anasema kuwa fasihi ya watoto ilipigwa jeki mwaka wa 1989, wakati viongozi wa Umoja wa Nchi huru za Kiafrika, kwenye mkutano wa kumi na sita uliofanyika Monorovia ambapo haki za watoto zilitambuliwa. Nchini Kenya, sheria ya kuwalinda watoto ilipitishwa mwaka 1991 (The Republic of Kenya 2001 The Hansard) Haya yalitokana na mwamko wa jamii ya kisasa taifa kuyazingatia masuala ibuka, na matumizi yake katika jamii. Changamoto hizi ni kama maswala ya afya, mazingira, siasa, elimu, ulemavu, familia za mzazi mmoja, umaskini, ukosefu wa ajira, dhuluma dhidi ya watoto, unajisi, ajira ya watoto na dawa za kulevya. Wizara ya Elimu na Teknolojia (2002) ilipopendekeza watoto kushughulikiwa katika silibasi kulichangia waandishi kuandika matini za fasihi ya watoto. Hii ndio sababu utafiti huu unakusudia kuchunguza na kuchambua matini tatu teule za fasihi ya watoto ili kufafanua taswira, zilizotumiwa kueleza matumizi ya dawa za kulevya athari za matumizi ya dawa za kulevya na

mielekeo wa watoto kuhusu dawa za kulevya. Kila mwandishi ana mtindo wake wa kuandika anaojitambulisha nao. Mwandishi anaweza kutumia mbinu ya kimajazi, takiriri, taharuki, na fantasia. Kusudi la kutumia mbinu hizi ni kuwavuta na kuwanata wasomaji au hadhira yake. Taharuki na fantasia kwa mfano inapotumika katika fasihi ya watoto huwa na mvuto wa kipekee.

Fasihi ya watoto hutoa mwongozo muhimu kwa watoto. Stephen (1992), anasema Fasihi ya watoto hutumika kama daraja ya kuwavukisha watoto kutoka utotoni hadi utu uzima na utumika kama dira ya kuwaongoza watoto kimaadili. Fasihi ya watoto yastahili kukuzwa kwa njia ya kuiandikia vitabu vyenye maudhui yanayohusu mambo yanayowaathiri kama vile dawa za kulevya. Muleka (2001) anasema lazima wanaohusika na kuwalea watoto waelewe kuwa watoto husoma yale wanaosoma na kuyatafakari ili kuchukua hatua fulani. Watoto wakiadilishwa vizuri wataweza kuepukana na matumizi ya dawa za kulevya zinazowaathiri vibaya katika jamii husika.

Maisha ya usoni ya mtoto yanapaswa kutayarishwa ipasavyo na mapema. Tucker (1976) anaonyesha umuhimu wa kushughulikia masuala yanayowakumba watoto ili maisha yao ya usoni yawe ya fanaka. Utafiti huu umetilia maanani umuhimu wa kuwa maisha ya mtoto ya utotoni huchangia pakubwa kuamua mtoto atakuwa mtu mzima wa aina gani. Utafiti huu unakusudia kusawiri dawa za kulevya katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Utafiti huu ulikusudia kuliziba pengo hili kwa kuchambua matini teule ambazo zimeshughulikia kwa kina dawa za kulevya katika fasihi ya watoto. Matini teule zilizochambuliwa ni; *Vioja vya Musa (*Mogambi, 2007) *Atamlilia nani?* (Mohamed, 2009) *Ah! Ajizi* (Nyambeka, 2015). Kusudi kuu la utafiti huu ni kubainisha taswira zilizotumika, katika matumizi ya dawa za kulevya kueleza athari za matumizi ya dawa za kulevya na mielekeo wa watoto kuhusu dawa za kulevya. Ili kupata maarifa ya kitaaluma, kielimu na kutoa maelezo kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya. Ufahamu wa athari za dawa za kulevya ni muhimu kuwafunza watoto kujiepusha na matumizi ya dawa za kulevya.

### 1.2 Suala la Utafiti

Suala la dawa za kulevya ni miongoni mwa masuala mtambuko yanayowakumba watoto katika jamii. Suala la dawa za kulevya limekuwa na linaendelea kuwa sugu

kitaifa na kimataifa, na linapaswa kushughulikiwa ili kupata suluu na kuzuia maenezi na athari zake katika jamii. Fasihi ya watoto ni njia moja inayoweza kutumiwa kueleza athari za matumizi ya dawa za kulevya. Utafiti huu ulilenga kubainisha usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya katika fasihi ya watoto ya Kiswahili, kwa kuirejelea matini teule: *Vioja vya Musa*, *Atamlilia nani? na Ah! Ajizi*. Matini teule ziliandikwa na waandishi tofauti na kuchapishwa miaka tofauti. Licha ya kuwa na utafiti katika fasihi ya watoto ya Kiswahili hapajakuwepo na utafiti unaohusu usawiri wa dawa za kulevya katika matini teule za fasihi ya watoto.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo:

i. Kufafanua taswira zinazojidhihirisha katika usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule za fasihi ya watoto ya Kiswahili.
ii. Kueleza athari za matumizi ya dawa za kulevya katika fasihi teule ya watoto ya Kiswahili.
iii. Kutathimini mielekeo wa watoto kuhusu dawa za kulevya katika fasihi teule ya watoto ya Kiswahili ili waweze kushauriwa

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulinuiwa kujibu maswali ya utafiti yafuatayo:

i. Je, taswira inajidhihirisha vipi katika usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule katika fasihi ya watoto?
ii. Ni vipi waandishi wameeleza athari za matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule katika fasihi ya watoto?
iii. Mielekeo wa watoto kuhusu dawa za kulevya ni upi?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza matini tatu teule za fasihi ya watoto ya Kiswahili kwa lengo la kuelezea matumizi ya dawa za kulevya kwa watoto. Utafiti huu utawafaidi wasomi na watafiti wa fasihi ya watoto ya Kiswahili, kwa kuwa data iliyopatikana itaongezea maarifa na kuwaelekeza kuhusu matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa watoto. Data iliyopatikana ikichapishwa inaweza kutumiwa na wizara ya Elimu wanaotayarisha

mitaala ya shule kwa kuweza kuangazia masuala yanayohusu matumizi ya dawa za kulevya katika fasihi ya watoto.

### 1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Waandishi wengi wameviandika vitabu mbalimbali vya watoto vikishughulikia masuala yanayowakumba watoto katika jamii husika. Lengo lao kuu lilikuwa ni kuelimisha, kuonya au kukashifu mitindo au tabia pinzani inayokashifiwa na jamii husika ya mtoto na mwandishi mwenyewe. Kuna masuala mengi yanayoikumba jamii inayowakuza watoto. Wizara ya Elimu ilipendekeza yafunzwe shuleni (Wizara ya Elimu na Teknolojia (2002). Njogu, (2007) anaeleza kuwa masuala mtambuko huwafanya watoto wayaelewe maisha yao na hali halisi inayomzingira mtoto ili awe na uwezo wa kukuza uhusiano na ushirikiano wake na wanajamii wenzake. Ni muhimu kuelewa kuwa uhakiki au uchambuzi wa matini yoyote ya kifasihi zikiwemo matini za fasihi ya watoto unachangia pakubwa katika uboreshaji na uendelezaji wa fasihi. Ni katika mielekeo sawa na huu ambapo kuna umuhimu wa kutafitia kuhusu usawiri wa dawa za kulevya katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Kutafitia kuhusu usawiri wa dawa za kulevya kutasaidia kuiboresha na kuiendeleza fasihi ya watoto. Utafiti huu utasaidia kuchangia uelewaji wa masuala ya dawa za kulevya.

### 1.7 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga Kuchunguza suala la usawiri wa dawa za kulevya katika matini teule za Fasihi ya watoto ya Kiswahili kwa kufafanua matumizi ya taswira kusawiri matumizi ya dawa za kulevya, kuelezea athari za matumizi ya dawa za kulevya na kutathimini mielekeo wa watoto kuhusu matumizi ya dawa za kulevya. Uwanja wa Fasihi ya watoto ni mpana wenye matini ambazo ni vigumu kuzichambua zote. Hivyo utafiti huu ulijikita katika kuchambua matini tatu: *Vioja vya Musa* (Mogambi, 2007), *Atamlilia nani?* (Mohamed, 2009) na *Ah! Ajizi* (Nyambeka, 2015). Vitabu hivi teule na machapisho mengine yaliyochangia utafiti huu yalisomwa maktabani. Watoto wasailiwa walipewa matini teule wasome ili wajibu hojaji za mizani ya Likert nyanjani. Watoto wasailiwa walishirikishwa katika dodoso ili kutathimini mielekeo wa watoto kuhusu matumizi ya dawa za kulevya.

## 1.8 Maelezo ya Istilahi

Katika sehemu hii istilahi zilizotumiwa katika utafiti huu zimetolewa maelezo yake na jinsi zinavyohusiana na utafiti huu.

**Athari** Ina maanisha akili na tabia za mwathiriwa haziko sawa kutokana na kulewa zaidi, matumizi ya tegemezi na matumizi ya kusisimua.

**Dawa za kulevya** Ni matumizi ya dawa zisizoruhusiwa kimatibabu na huwa na athari katika mwili au akili ya mtumizi.

**Fasihi ya Watoto** Fasihi maalumu inayoandikwa kwa ajili ya watoto.

**Haki za Watoto** Sheria za kulinda maslahi ya watoto.

**Kijana** kijana ni kiumbe wa kiume au kike wa miaka 14 hadi 25.

**Maadili** Mwenendo mwema au maonyo au mafundisho ya kumwongoza mtoto kuwa na tabia nzuri.

**Masuala Ibuka** Maudhui yanayorejelea mambo yanayozuka na kuwaathiri wanajamii moja kwa moja.

**Matini** Hivi ni vitabu vya kusoma vya kifasihi.

**Matumizi mabaya ya dawa za kulevya –** Ofisi ya Umoja wa mataifa ya Mihadarati na Jinai (UNODC) 2008 ni matumizi ya dawa zisizoruhusiwa au zinazoruhusiwa kwa kupita kiasi. Utafiti huu una kusudia kuelezea dawa hizi za kulevya na jinsi zinavyotumiwa vibaya.

**Mtoto** Mtu mwenye umri mdogo; kutoka miaka saba hadi kumi na mitatu.

**Nadharia** Mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza kutatua na kutekeleza jambo fulani kwa kuweka nguzo ya ushahidi.

# SURA YA PILI

# MWAUO WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti aliangazia dhana ya fasihi ya watoto ya Kiswahili, maandishi kuhusu fasihi ya watoto dhana ya dawa za kulevya, dhima ya fasihi ya watoto na misingi ya nadharia. Mtafiti alizirejelea tafiti za watafiti mbalimbali na yaliyoandikwa na waandishi mbalimbali ili kuonyesha uhusiano na tofauti zilizoko kati ya kazi zao na utafiti huu na mchango wake kuhusu utafiti huu.

## 2.2 Maandishi kuhusu Fasihi ya Watoto

Lugha ya Kiswahili imechangia pakubwa katika kukuza fasihi ya watoto. Halliday (1978) na Odaga (1985) wanaeleza kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili ulimwenguni kuandikia hadithi kumechangia pakubwa uandishi wa matini nyingi za fasihi ya watoto ya Kiswahili. Lugha inayotumika katika fasihi ya watoto ni muhimu kueneza matumizi ya dawa za kulevya katika matini za fasihi ya watoto ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili inatumika kukuza na kueneza maadili miongoni mwa watoto. Halliday (keshatajwa), anasema kuwa kupitia lugha mtoto hurithishwa mila, utabaka na mwonoulimwengu wake kuhusu jamii.

Fasihi ya watoto si ya zamani sana ikilinganishwa na fasihi ya watu wazima iliyoanza muda mrefu. Fasihi ya watoto imepuuzwa na kutelekezwa kwa muda mrefu kutokana na kutopewa umuhimu unaostahili na wahakiki na wasomi na hivyo kudharauliwa na wanajamii Bakize (2013). Wanajamii wengi wameinasibisha fasihi ya watoto na mambo ya kitoto ambayo ni rahisi, yasiyo ya msingi wala uzito wowote wa kudhaminiwa. Hii ndiyo sababu ikaitwa fasihi ya watoto (Wamitila, 2008). Tafiti zinaonyesha kwamba fasihi ya watoto ya Kiswahili limechipuka barani Afrika hivi karibuni, hasa kwenye miaka ya 1980 kutokana na kutiliwa mkazo kwa masuala ya haki za watoto (Ngugi, 2016).

Fasihi ya watoto si kongwe kama fasihi ya watu wazima. Mulokozi (2008), kwa upande wake anaeleza kwamba nchini Tanzania fasihi ya watoto ilichipuka wakati na baada ya ukoloni katika miaka ya 1960 na kushika mizizi miaka ya 1970. Zaidi ya hayo, fasihi hii ilishika mizizi zaidi miaka ya 1990. Hii ilitokana na sababu kama vile kupitishwa

sheria za haki za watoto 1991 kutokana na mwamko wa umoja wa Kimataifa kuhusu masuala ibuka. Masuala ibuka haya yalileta maudhui tofauti ya kuandikia juu yake. Sababu nyingine muhimu sana ni kuzinduliwa kwa mradi wa vitabu vya watoto Tanzania. Mradi huu uliwawezesha waandishi, wachapishaji na wachoraji wa vitabu vya watoto kufanya kazi za fasihi ya watoto kwa weledi zaidi.

Aidha, mradi huu pia ulifungua maktaba katika shule zilizo chini ya mradi huo na kusambaza vitabu vilivyochapishwa kwa usomaji wa ziada. Kufikia mwaka wa 2015 mradi huu ulikuwa umechapisha na kusambaza vitabu zaidi ya 350 (CODE, 2015). Mradi huu ulileta msisimko wa usomaji vitabu vya fasihi ya watoto. Uandishi nchini Kenya wa fasihi ya watoto ulipata umaarufu miaka ya 2000 baada ya kujumuishwa katika somo la Kiswahili kuanzia shule za msingi hadi shule za upili. Hatua ya Serikali ya kugharamia masomo imechangia pakubwa katika maendeleo haya kwa sababu Serikali ilichukua jukumu la kununua vitabu vya ziada na kiada.

Ngugi, 2014) anasema kuwa fasihi ya watoto ni ile fasihi iliyotungwa na watu wazima au watoto wenyewe, yenye kutumia lugha ya Kiswahili na kukusudiwa kusomwa au kutendwa na watoto. Osazee (1991), anasema fasihi ya watoto ni sanaa inayochota malighafi yake kutokana na mielekeo au mwonoulimwengu wa Kiafrika, iliyoandikwa katika lugha na mtindo ambao mtoto wa Kiafrika ataelewa. Fasihi ikuze utamaduni wa Kiafrika na kumsaidia mtoto kuelewa mazingira yake na kuyakubali. Osazee anaegemea mielekeo wa kuinua Afrika na kukuza fasihi ya Kiafrika.

Kuna fasihi ya watoto, vijana na ya watu wazima na huwa na sifa zake. Kulingana na Wamitila (2008), Fasihi huwa na sifa zake bia. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), anasema kuwa fasihi ya watoto ni fasihi maalum iliyoandikiwa walengwa wake ambao ni watoto. Fasihi hii ya watoto huwa na mambo matatu makuu. Mhusika mkuu awe mtoto, dhamira, iwahusu watoto na lugha sahihi itumiwe kuendeleza msuko. Hata ingawa Katiba ya Kenya (2010) inasema mtoto ni mtu aliye chini ya miaka kumi na minane. Kwa hivyo maoni ya mtafiti ni kuwa fasihi ya watoto ni kazi ya sanaa inayotumia lugha kwa usanii na inayowasilisha suala fulani pamoja kwa njia inayoathiri, kugusa na kuacha athari fulani kwa mlengwa ambaye ni mtoto.

Fasihi ya watoto ina sifa zake ambazo ni muhimu na huwa zinaitofautisha na fasihi ya watu wazima na ile ya vijana. Kulingana na Matundura (2007) na Wamitila 2008 kuna sifa bia za Fasihi ya watoto zinazokubalika ulimwenguni kote. Sifa hizi ni kama: mhusika mkuu ni mtoto, mgogoro umuhusu mtoto, hadithi hizi huwa fupi, na huandikwa kwa lugha nyepesi na ploti sahihi, hutumia fantasia na kushirikisha wahusika wa aina mbalimbali. Maudhui ya hadithi hizi ni kuwahamasisha watoto kuhusu masuala ya jamii, mienendo na uvumbuzi wa masuala mtambuko hutumia picha na michoro ili kuwavutia watoto. Hadithi hizi pia huwa na miishio yenye upeo wa furaha. Matini hizi ziwe fupi na zizingatie wahusika watoto na uhusika ulenge maudhui ya watoto. Kuna tanzu za fasihi simulizi na fasihi andishi katika fasihi ya watoto. Kila utanzu una vipera vyake. Katika simulizi kuna vitanzu kama hadithi, semi, nyimbo na katika utanzu andishi kuna hadithi fupi, riwaya, tamthilia na ushairi (Ngugi na wenzake). Sifa hizi ni muhimu kuzingatiwa kuainisha matini za watoto.

Kuna watafiti wametafitia kuhusu fasihi ya watoto. Fasihi ya watoto inaweza kushabihiana kutoka nchi hadi nyingine. Odaga (1985) alichunguza hadithi za kubuni za watoto katika nchi ya Kenya. Alitambua kuwa fasihi ya watoto katika nchi za Kenya, Tanzania na Uganda zilikuwa na uhusiano kwa kiwango fulani kwani hizi nchi za Afrika Mashariki zina historia ya ukoloni inayoshabihiana kando na kuwa na wachapishaji sawa. Hata hivyo anasema kuwa fasihi hii ya watoto inayoandikiwa watoto katika nchi ya Kenya, Uganda na Tanzania tofauti kwani kila nchi huendeleza itikadi tofauti na nyingine kwa nia ya kujitambulisha kama taifa huru. Ingawa utafiti wake uliangazia fasihi ya watoto ya Kiswahili nchini Kenya, aliangazia vitabu vilivyo andikwa kwa lugha ya Kiingereza. Tofauti na utafiti wake Odaga (keshatajwa), utafiti huu ulitafitia usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule za fasihi ya watoto ya Kiswahili. Mtafiti anaelewa matini na maudhui yanayoshughulikiwa katika fasihi ya watoto. Yale utafiti huu ulishughulikia yanaweza kuwa yanawakumba watoto wa nchi zingine.

Usomaji wa kazi ya fasihi huwa na athari fulani kwa msomaji. Stephen (1992), alibaini kuwa msomaji hushawishiwa na kushikilia mawazo ya mwandishi ambayo huwa yamefumbatwa katika matendo ya mhusika mkuu katika hadithi. Nafasi ya majukumu ya wahusika hupitisha ujumbe mahususi kwa msomaji. Mwandishi humwelekeza mtoto

jinsi atakavyo mchukulia mhusika fulani wa hadithini na jinsi anafaa kuonyesha hisia zake kuhusu matukio katika hadithi. Utafiti wa Stephen (keshatajwa) kuhusu majukumu ya wahusika ni muhimu kwa kuwa unaonyesha kuwa msomaji anaweza kuathiriwa na mhusika wa hadithi na kuonyesha hisia zake. Utafiti huu ulichunguza matumizi ya usawiri wa dawa za kulevya katika fasihi ya watoto. Vilevile ulichunguza mielekeo wa msomaji wa hadithi baada ya kusoma na kuonyesha hisia zake. Uchunguzi wa Stephen unafaa utafiti huu kwa kufanya mtafiti kuelewa kuwa mtoto msomaji anaweza akaathiriwa na usomaji wa hadithi. Matumizi ya usomaji wa matini utajidhihirisha katika matendo na hatua atakazozichukua baada ya kuisoma matini. Stephen (keshatajwa) alichunguza wahusika nao utafiti huu ulichunguza usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya. Fasihi inapoandikwa au kushughulikwa na wataalamu huwa na majukumu iliyotengewa kutekeleza, kama vile kushauri, kuelimisha, kuburudisha na kuonya miongoni mwa mengine.

Mpesha (1996) alitafitia hadithi za Kiswahili za watoto nchini Tanzania. Aling'amua kuwa fasihi ya watoto ina majukumu mengi katika jamii. Anasema kuwa fasihi ya watoto si rekodi ya matukio ya kijamii lakini pia hutumiwa kama kifaa cha kutangamania. Utafiti wa Mpesha (keshatajwa) unatoa umuhimu wake kwa kuwa ulitambua kuwa hadithi za watoto ni hali halisi ya yale yanayowakumba watoto katika jamii. Yale yanayopatikana katika matini hizi ni picha kamili ya yale yamo katika jamii husika. Utafiti wa Mpesha (keshatajwa) ni muhimu kwa kuwa ulichangia mtafiti kuelewa kuwa yale yanayopatikana katika matini hizi teule za fasihi ya watoto ya Kiswahili kuhusu matumizi ya dawa za kulevya ni hali halisi au picha kamili ya yale yanayopatikana katika jamii husika. Tofauti kati ya utafiti wake na utafiti huu ni kuwa alitafitia hadithi za watoto nchini Tanzania. Utafiti huu nao ulitafitia usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya. Hakushirikisha matini hizi teule za Kiswahili; *Vioja vya Musa* (Mogambi, 2007) *Atamlilia nani?* (Mohamed 2009) na *Ah! Ajizi* (Nyambeka, 2015).

Fasihi ya watoto inavyo vipera tofauti vinavyochangia fasihi hii kuwa na mashiko. Vipera hivi ni kama ngano, hadithi, vitendawili na methali. Vipera hivi pia huchangia pakubwa kukuza na kuelewa umuhimu wa fasihi ya watoto. Uchunguzi wa Nkata (2001) uliohusu maendeleo na mabadiliko katika usimulizi wa hadithi hasa za watoto

nchini Uganda, ulionyesha umuhimu wa nyimbo katika fasihi ya watoto. Alieleza kuwa nyimbo zinazotumika katika usimulizi husaidia kushirikisha hadhira na pia kuchangia katika kufanikisha fasihi ya watoto. Utafiti wake ulionyesha kuwa kazi zilizotumia nyimbo huzifanya kazi hizi kuonekana kuwa nzuri zaidi. Utafiti huu ulimsaidia mtafiti kuelewa matumizi ya nyimbo katika fasihi ya watoto kama vile taswira zinavyotumika katika matini teule kuwasilisha ujumbe kuhusu matumizi ya dawa za kulevya katika fasihi ya watoto. Nkata alitafitia nyimbo nao utafiti huu ulishughulikia matumizi ya taswira katika usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule za fasihi ya watoto ya Kiswahili.

Kila mwanafasihi huwa na mbinu yake ya kuwasilisha maudhui au ujumbe wake kwa njia ya sanaa. Mbinu huwa ni matumizi ya methali, uradidi, majazi, tashbihi miongoni mwa mengine. Akinyemi (2003) alichunguza fasihi simulizi ya watoto ya jamii ya Wayoruba na kumaizi kuwa fasihi hii ilitumia takriri, jazanda, na tashbihi na mbinu zingine za lugha ili kuipamba na hivyo kupendeza mtoto msomaji. Anasema kuwa mbinu hizi za lugha hazikusaidia tu kuvutia watoto bali pia zilisaidia watoto kukumbuka kwa urahisi maadili yaliyokuwa yakipitishwa kwao. Utafiti wa Akinyemi ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa alichunguza fasihi simulizi nao huu ulichunguza fasihi andishi yaani matini teule za fasihi ya watoto ukiangazia usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya. Hata hivyo utafiti wake ulifaa utafiti huu kwa kumfanya mtafiti kuelewa zaidi jinsi waandishi hutumia mbinu mbalimbali za lugha kuwasilisha maudhui yao hata katika matini andishi kama ilivyo katika fasihi simulizi.

Fasihi yoyote ile huwa na jukumu la kufunza maadili kulingana na kaida za jamii. Brunner (2003) alichunguza tungo za hadithi kwa kurejelea maisha na sheria za jamii. Brunner (keshatajwa) alitambua kuwa hadithi huelezea matukio yaliyokuwepo katika jamii na mambo yaliyotarajiwa katika jamii fulani. Hata ingawa hadithi hutumika kutoa mwongozo kwa jamii, dhima yake kuu ni kuonya wanajamii. Hii ndio maana hadithi nyingi husawiri wahusika waliokiuka sheria na kuvunja miiko katika jamii. Mawazo yake yalieleza sababu ya wasomaji watoto kusisimuliwa na hadithi ambazo huangazia makosa ya mhusika yasiotarajiwa au matukio ambayo ni ya kushangaza katika jamii. Utafiti huu wa Brunner uliufaa utafiti huu kwa kuongoza mtafiti kuelewa kuwa hadithi katika matini teule zinatumiwa kama dira ya kumwongoza mtoto msomaji kuyaona

makosa yanayopaswa kuepukwa. Kutoa onyo kama utafiti huu ulikusudia kuwa matini hizi teule zitatoa onyo kuhusu matumizi ya dawa za kulevya kwa kuangazia athari za matumizi yake.

Msomaji yeyote wa fasihi iwe ni ya vijana, watoto au watu wazima huwa na athari fulani baada ya kuisoma matini fulani. Athari hii humpelekea kuchukua hatua fulani. Karuga (2005), alichunguza mwitikio wa mtoto msomaji kuhusu matini anazozisoma. Alichunguza matini teule zinazotumiwa katika shule za msingi nchini Kenya akitilia maanani/mkazo mtindo, maudhui na uhusika. Alimaizi kuwa kwa kutumia matumizi mazuri ya mtindo mwandishi anaweza kuwasiliana na mtoto msomaji barabara. Alisisitiza umuhimu wa uhusika katika matini za watoto. Utafiti wake ulifaa utafiti huu kwa kuwa mtafiti ataufahamu zaidi mtindo, maudhui na uhusika anapokumbana na mambo haya ya mtindo, maudhui na uhusika katika matini teule. Tofauti iliyoko katika tafiti hizi mbili ni kuwa Karuga (keshatajwa) alitafitia mtindo, maudhui na uhusika katika hadithi za watoto nao. Utafiti huu ulichunguza matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule. Katika tafiti zote mbili kuna athari inayomkumba msomaji.

Utafsiri wa vitabu vya fasihi huzingatia sifa zinazomwongoza mtafsiri. Muthubi (2005), alitafitia mikakati iliyotumiwa katika utafsiri na kurahisishwa kwa matini zilizotafsiriwa kutokana na matini za watu wazima na kuvifanya vitabu vya fasihi ya watoto. Mifano ikiwa ni *Mkasa wa shujaa Liyongo*. Hata hivyo utafiti wa Muthubi ni tofauti na huu, kwa kuwa alitafitia tafsiri ya mwandishi wa vitabu vya watoto na utafiti huu ulitafitia Usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya. Utafiti wa Muthubi (keshatajwa) uliongoza mtafiti kuzifahamu sifa za kuzingatia wakati wa kuchagua matini za utafiti. Aidha ulimsaidia mtafiti kuelewa matini hizi barabara, kutambua ni zipi zilizotafsiriwa na ni zipi hazikutafsiriwa. Mtafiti aliweza kulinganisha na kulinganua mtindo, maudhui na uhusika katika fasihi za watoto.

Taswira humwongoza msomaji kuielewa matini kwa kutafakari picha za akilini anapoisoma matini. Matundura (2007), alichunguza taswira dumifu za Uana katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Lengo lake lilikuwa kuchunguza jinsi na kiwango ambacho waandishi wa fasihi ya watoto wanashirikisha taswira dumifu za Uana katika matini zao. Alichunguza iwapo usawiri wa taswira dumifu zilishirikishwa kimakusudi

au zilipenyezwa kiholelaholela tu. Alichunguza kama kuna usawa wa uana au jinsia moja ilikuwa ikibaguliwa katika matini teule. Aligundua kuwa jinsia ya kike ilisawiriwa kama jinsia nyonge na jinsia ya kiume kusawiriwa kama mabingwa. Anasema kuwa ni muhimu waandishi kushughulikia jinsi watoto wanavyosawiriwa katika kazi zao jambo linalofanywa na utafiti huu. Utafiti wa Matundura (keshatajwa) ni tofauti na huu kwa kuwa alitafitia taswira dumifu za Uana na utafiti huu unatafitia usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule za fasihi ya watoto ya Kiswahili. Matundura alishughulikia taswira dumifu kwa jumla akishirikisha watu wazima. Utafiti huu ulijikita kwa watoto peke yake.

Watoto katika jamii wanapitia dhuluma nyingi kama vile ajira za watoto, kuteswa, kubakwa miongoni mwa zingine kama inavyoangaziwa katika matini za watoto. Kavuria (2008), alichunguza dhuluma dhidi ya watoto katika riwaya za Kiswahili. Aling'amua kuwa watoto wanapitia dhuluma kama kuchapwa, kunyimwa chakula, na ajira yenye malipo duni. Utafiti wa Kavuria (keshatajwa) ni muhimu kwa kuwa dhuluma dhidi ya watoto ni sababu moja inayowafanya watoto kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya suala linalorejelewa na utafiti huu. Hata hivyo utafiti huu ulitofautiana na huu wa Kavuria kwa kulenga makusudi suala la matumizi ya dawa za kulevya na jinsi zilivyosawiriwa katika fasihi ya watoto.

Waandishi wa fasihi hutumia mitindo mbalimbali kuelezea jinsi mambo yalivyo katika jamii. Kairu (2009), alichunguza mtindo na uhalisi ulivyojidhihirisha katika vitabu vya hadithi vya Ken Walibora. Alitambua kuwa yale yameandikwa katika matini hizi ni hali halisi ya yale watoto wanapitia katika jamii. Kwa msomaji ni kuwa anafahamikiwa na mambo zaidi katika mazingira ya mtoto. Kairu (keshatajwa) alitafitia mtindo na uhalisia nao utafiti huu ulitafitia usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya. Utafiti wake Kairu ulishughulikia matini za mwandishi mmoja ilhali utafiti huu ulishirikisha matini za waandishi mbalimbali. Hata hivyo utafiti wake ni muhimu kwa kuwa ulimwelekeza mtafiti kuelewa masuala yanayowakumba watoto katika jamii. Utafiti huu ulishirikisha usawiri wa dawa za kulevya katika matini za fasihi ya watoto kama hali halisi ya yale watoto wanapitia katika jamii. Utafiti wake unamwongoza mtafiti kuelewa jinsi hali halisi ya mambo katika jamii yanavyo sawiriwa katika matini za watoto.

Watoto katika jamii wanakumbwa na masuala ibuka kama vile dawa za kulevya, UKIMWI, utunzaji wa mazingira miongoni mwa masuala mengine yanayowakumba katika jamii husika. Masuala ibuka yana matumizi yake. Tonui (2010) alitafitia maudhui ya UKIMWI katika fasihi ya watoto. Amebaini athari zinazo watinga watoto baada ya wazazi wao kuambikizwa virusi vya UKIMWI au wao wenyewe wanapoambukizwa virusi vya UKIMWI. Watoto walioambukizwa wanapitia vipindi vigumu sana. Utafiti wake ulichangia utafiti huu kwa kuongoza mtafiti kuelewa zaidi masuala yaliyowakumba watoto katika jamii na matumizi yake. Utafiti wake unakaribiana na huu kwa kuwa ulichunguza masuala yanayowakumba watoto, UKIMWI, huu mwingine ulichunguza suala linalowakumba watoto ambalo ni matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule katika fasihi ya Kiswahili.

Matini za watoto zinazoshirikisha fantasia huwa ni za kuvutia sana kwa watoto. Pia zinavuta makini ya kusoma na kumakinika ili waweze kuelewa matini kutoka mwanzo hadi mwisho. Akinyi (2017) alichunguza upokezi wa hadithi za kifantasia miongoni mwa watoto wa shule za msingi. Hadithi hizi licha ya kuwa zingine zinaweza kutisha watoto zina ukumbusho mkubwa unaowafanya watoto kutamani kusoma zaidi na kuwa na kumbukumbu ya mambo hayo. Wanaposoma kuhusu mazingaombwe haya utamani kujua litakalotokea mwishoni. Utafiti huu ni muhimu kwa kuwa unahusisha upokezi ambao utafiti huu unagusia katika mielekeo wa msomaji. Tofauti ya utafiti wake na huu ni kuwa alitafitia Upokezi wa hadithi za kifantasia nao huu ulishughulikia matumizi ya dawa za kulevya katika fasihi ya watoto.

Suala la uana limeshughulikiwa kwa njia mbalimbali na wanasanaa tofauti tofauti. Kuna wale wamekuza usawa na wengine wakileta mielekeo hasi kwa jinsia fulani. Wengine watakuwa na mielekeo chanya kuhusu jinsia fulani. Miricho na Mbuthia (2017), walichunguza usawiri wa mtoto wa kike na wa kiume katika matini teule za fasihi ya watoto; *Mwepesi wa Kusahau* na *Likizo ya Mkasa*. Wataalamu hawa walichunguza jinsi jinsia mbili zilisawiriwa sawa au kuna usawiri hasi kwa jinsia au usawiri chanya kwa jinsia moja. Aligundua waandishi wengine wamewasawiri sawa na wengine wamependelea upande fulani. Kuna wale wamechora kijana wa kiume akiwa mnyonge asiyeweza kujiamlia mambo ilhali yule wa kike akiwa na uwezo mkubwa kuliko wa kiume. Usawiri huu unaweza kuwa na athari kubwa za kimawazo

wakajichukia, au wakachukia jinsia nyingine au kutotamani kutenda vitendo vya wahusika wengine wa fasihi ya watoto. Mawazo ya wataalamu hawa yalimwongoza mtafiti kuyaelewa masuala ya watoto kwa kina zaidi katika usawiri wa kijinsia. Tofauti ni kuwa walishughulikia usawiri wa kijinsia na utafiti huu ulishughulikia usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya katika fasihi ya watoto.

Matini za kifasihi huwa na itikadi mbalimbali kama vile kisiasa, kiuchumi na kidini. Itikadi hizi zimechorwa katika fasihi ya watoto ili waweze kuzielewa. Nyaga (2017), alitafitia itikadi za kisiasa zilivyojitokeza katika vitabu teule *Usininyonye, Mkasa wa shujaa Liyongo, Karamu mbinguni, Zimwi la leo na Sungura mpanda ngazi* vya fasihi ya watoto ya Kiswahili. Nyaga alibaini kuwa itikadi za kisiasa hujitokeza katika fasihi ya watoto kupitia maudhui, mbinu za lugha na jinsi wahusika walivyosawiriwa katika hadithi husika. Utafiti huu wa Nyaga unalimfanya mtafiti kufahamu zaidi masuala ya watoto kwa kuzingatia maudhui, Lugha na wahusika. Mtafiti alielewa matini hizi zaidi kwa kuzingatia na kuangazia maudhui, lugha na uhusika kwa makini. Tofauti katika utafiti wake na huu ni kuwa alitafitia itikadi za kisiasa katika fasihi ya watoto ya Kiswahili nao utafiti huu ulitafitia usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule za fasihi ya watoto ya Kiswahili.

Uhusika na wahusika ni jambo muhimu katika kazi ya fasihi. Mwanasanaa hutumia wahusika ili kupitisha ujumbe wake na kuonyesha mielekeo wake kuhusu jambo fulani. Mbuthia (2018) alichunguza usawiri wa wahusika wa waandishi mbalimbali na kuonyesha athari na mwonoulimwengu wao. Ameng'amua waandishi wengine wanadunisha jinsia fulani na kuifanya kuonekana ndio hasi, kama vijana wakiume wanavyochorwa kama waasi na wavunja sheria na wanaonekana wakiumia kutokana na kuvunja sheria. Wanawake hawajasawiriwa kwa njia hasi. Usawiri wa aina hii ni hatari kwa kuwa jinsia moja ilisawiriwa kuwa ni wavunja kanuni. Utafiti huu unamwongoza mtafiti kuelewa matini za fasihi ya watoto zaidi. Utafiti wake Mbuthia (keshatajwa) ni tofauti na huu kwa kuwa alitafitia usawari wa wahusika nao utafiti huu ulitafitia usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule za fasihi ya watoto.

Kuna uwezekano wa nchi zilizokaribiana kijiografia kuwa na masuala yanayoelekeana na kushabihiana katika fasihi ya watoto. Utafiti wa Ngugi na wenzake (2018) walitafitia maendeleo ya fasihi ya Kiswahili ya watoto nchini Tanzania na Kenya. Waling'amua kuwa maendeleo ya fasihi Tanzania na Kenya yalielekeana. Kila nchi inaweza kujifunza kutokana na ile nyingine. Kuna umuhimu wa kuanzisha mradi wa kushughulikia uandishi wa masuala ya watoto. Kukiwa na mradi wa watoto utashughulikia uandishi, uchapishaji na uratibu wa kazi za watoto utakuwa rahisi sana. Hali hii itaendeleza na kuikuza fasihi ya watoto. Utafiti huu wao ulimwelekeza mtafiti kuelewa maendeleo ya fasihi ya watoto ya Kiswahili.Tofauti ya utafiti wao na huu ni kuwa walitafitia maendeleo ya fasihi ya watoto nao utafiti huu ulishughulikia matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule. Kutokana na tafiti hizi na zingine, kwa kuwa haziwezi zikatajwa zote, ni kuwa hakuna utafiti uliofanywa kushirikisha suala la matumizi ya dawa za kulevya katika matini tatu zilizo teuliwa katika utafiti huu za fasihi ya watoto ya Kiswahili. Utafiti huu ulikusudia kuuziba mwanya huu, kwa kutafitia suala la matumizi ya dawa za kulevya katika fasihi ya watoto ya Kiswahili.

## 2.3 Dhana na Dhima ya Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto ina dhima sana kwa watoto. Hunt (1999), anadai kwamba, dhima ya fasihi ya watoto ni pana kwa kuwa inategemeana na mahitaji husika na kwa kipindi tofauti. Kwa mfano, baadhi ya vitabu ni vizuri kwa kupotezea muda, kupata elimu, kupanua uwezo wa kufikiri, kurithisha tamaduni na maadili ya kijamii, kupambana na masuala kadhaa au kupambana na matatizo mbalimbali ya magonjwa. Mathalani, vingine pia ni vizuri kwa kusoma katika namna ya usomaji ili kupata weledi wa usomaji na kupambana na ubaguzi. Utafiti huu ulikusudia kuonyesha jinsi waandishi wa matini za *Vioja vya Musa, Atamlilia nani? na Ah! Ajazi* walipambana na suala la dawa za kulevya katika Fasihi ya watoto.

Fasihi yoyote ile, huwa na dhima ya kutekeleza inapoendelezwa na wanajamii. Fasihi ya watoto huwa na dhima yake. Ngugi (2011), anabainisha kwamba, fasihi ya watoto kama ilivyo ile ya watu wazima, inayo dhima muhimu sana katika jamii ya watoto na jamii pana kwa ujumla. Baadhi ya dhima hizo ni kujiburudisha, kujiondoa katika hali fulani ya matatizo anayopitia mtoto, kuchachawisha ubunifu, kuwasaidia watoto kujielewa na kuwaelewa watoto wengine na kupata uzoefu wa kuelewa umbo la lugha.

Ngugi (2012) alisisitiza kwamba, kama ilivyo fasihi ya watu wazima, fasihi ya watoto huwafanya watoto waburudike na kujielimisha. Alifafanua kuwa, fasihi hii huwaelimisha watoto kwa kupanua mawazo yao kutokana na maisha ya watu wengine katika jamii. Mtoto hupata maonyo, mawaidha, makatazo na maelekezo. Vilevile alieleza kwamba fasihi hii huendeleza utamaduni kwa kueneza au kuwarithisha watoto mambo yanayothaminiwa na jamii ili wayaendeleze na kuyahifadhi, kama vile kudumisha mila za kijamii.

Fasihi ya watoto huwa na dhima maalum kwa watu wote. Matundura na wenzake (2013) wakishadidia hoja za Ngugi (2011 & 2012) walieleza kwamba fasihi ya watoto huzua raghba kubwa miongoni mwa wanajamii kwa sababu huhusu kitengo cha jamii ambacho takribani kila mtu katika jamii ana uhusiano nacho. Dhima hiyo lina kwenda mbali kidogo kwa kuonesha kwamba fasihi ya watoto pia, ina manufaa makubwa kwa watu wazima. Matundura na wenzake (keshatajwa) waliongeza kuwa, fasihi ya watoto ni suala nyeti kwa sababu fasihi hiyo hutoa mchango mkubwa katika kukuza taswira ya watoto kuhusiana na maisha yao wenyewe na ulimwengu pindi watakapokuwa watu wazima. Wataalamu hao wanadai kuwa fasihi ya watoto huwapa watoto maarifa na ukweli kuhusu hatua ya maendeleo iliyofikiwa na jamii zao. Wanasema kuwa fasihi ya watoto ni nyenzo muhimu ya kuwasaidia watoto kuelewa mazingira ya nyumbani, jamii zao na ulimwengu kwa ujumla.

Dhima za fasihi ya watoto zimewashughulisha watu wengi ambao hawawezi wote kutajwa hapa. Wengine waliochangia ubainishaji wa dhima ya fasihi ya watoto ni pamoja na Deaton (1946), Cianciolo (1981), Freeman na Levistik (1988) Erickson (1994), Nawrot (1996), Reycik na Rosier (2009), Lyimo (2014), Ngugi (2014), Ni muhimu kutaja hapa kuwa ni dhima hizi ndizo zilizoibua fasihi hii katika umahususi wake ili mtoto apate kile alichokuwa alikikosa hapo awali. Watoto wanapata faida kubwa siku hizi kusoma kazi za fasihi zenye mafunzo mengi sana kwao. Mafunzo haya huwaongoza, huwakuza na kuwafanya watu wa maana siku za usoni.

### 2.4 Dhana ya Dawa za Kulevya

Kwa mujibu wa umoja wa mataifa kuhusu afya (WHO) dawa za kulevya ni matumizi ya dawa zisizoruhusiwa kitiba na huwa na athari katika akili na mwili wa binadamu.

Pia wanasema kuwa dawa za kulevya zinahusisha vitu vinavyoleta hisia au misisimko mwilini mwa mwanadamu. Wanadamu wanashirikisha matumizi ya dawa za kulevya kama vile; bangi, mandras, heroini, kokaini, pombe za kienyeji kama Chang'aa ambayo haijaruhusiwa. Zingine zimeruhusiwa kama vile miraa, sigara na pombe. Watoto hushirikishwa katika uraibu huu wa dawa za kulevya kama wasafirishaji wa mihadarati, watumiaji, wauzaji wa dawa za kulevya baada ya kuhadaiwa watalipwa vizuri au kwa kutunukiwa zawadi. Hatimaye na wao huishia kuwa waraibu.

Janga la dawa za kulevya linachangamoto nyingi sana. Usafirishaji wa dawa za kulevya unachukua mkondo tofauti ulimwenguni. Matumizi ya simu tamba huwapa wasafirishaji na wauzaji njia mbadala za kuuza kwa kutumia simu na mitandao bila kujulikana kwa urahisi. Uuzaji wa dawa za kulevya umeongezeka kwa asilimia 50 kati ya Septemba 2013 na Januari 2016. Kulingana na utafiti wa 2017 kuhusu dawa za kulevya ulimwenguni ni kwamba mwaka wa 2014 makundi ya magaidi yanayovunja sheria yalikuwa yamechuma pesa nyingi kutokana na uuzaji wa dawa za kulevya. Makundi haya ya magenge hutumia fedha kufadhili vitendo viovu kama ulipuaji mabomu na vilipuzi vingine. Vitendo vya kigaidi vinatishia maisha ya watu wasio na hatia hata kidogo na husababisha uharibifu wa mali ya watu. Magaidi hutumia faida kutokana na biashara ya dawa za kulevya kufadhili ugaidi. Taliban ambacho ni kitivo cha ugaidi upata nusu ya kipato chake kutokana na dawa za kulevya. Asilimia 85 ya bangi hukuzwa Taliban nchini Afghanistan.

Kulingana na shirika la kimataifa linaloshughulikia dawa za kulevya na makosa ya jinai UNODC (2015) soko la dawa za kulevya ulimwenguni linaendelea kupanuka. Matumizi ya bangi ulimwenguni yameongezeka kwa kiwango kikubwa. Dawa ya heroini, ni dawa zinazotumiwa kutibu watu zinageuzwa na kutumiwa vibaya kama dawa za kulevya. Mwaka wa 2015 dawa za kulevya ziliongezeka kutoka 260 (NPS) hadi (483) NPS. Dawa zilizo na uwezo wa kuathiri ubongo na mawazo ya mtumiaji. Mwaka wa 2016 ukuzaji wa bangi na soko la Kokaini liliendelea kupanuka sana. Ukuzaji wa bangi uliendelea kwa thuluthi moja nchini Afghanistan.Soko la Kokaini lilipanuka zaidi kati ya miaka ya 2013 na 2015 upanzi wa miti ya kokaini imeongezeka kwa asilimia 30 baada ya ukuzaji wake kuongezeka nchini Colombia. Kokaini

limeongezeka katika uuzaji wake baada ya masoko mawili makuu kupanuka, Marekani kaskazini na Uropa.

Mwaka wa 2018 (UNODC) ilionyesha kuwa wanaume ndio wanaoathiriwa pakubwa kuliko wanawake. Kwa kila mwanamke mmoja kuna wanaume watano ambao wameathiriwa. Hawa ni watu walio na umri wa miaka 40 na zaidi ni watu ambao wanapaswa kuliendeleza taifa lao. Watoto wadogo na vijana ndio walioathiriwa zaidi na dawa za kulevya. Watoto wanaanza kutumia dawa za kulevya wakiwa kati ya miaka 12-14 wengi wakihadaiwa kuwa wakizitumia dawa za kulevya watakuwa werevu sana masomoni. Wengi wao huingizwa katika dawa za kulevya wakiwa kati ya miaka 15-17. Kilele cha matumizi ya dawa za kulevya huweza kuwa kati ya miaka ya 18-25. Hili ni jambo la kusikitisha mno kuona watoto wadogo wakihusika katika dawa za kulevya ambazo zina athari kubwa katika maisha yao. Watoto hawa ndio wanatarajiwa kuwa viongozi wa kesho, na pia wafanyikazi katika idara mbalimbali za serikali.

Dawa za kulevya huwazuzua watoto kiasi cha kuwa huwategemea watu wengine ili kuwapa matibabu na kuwapeleka katika vituo vya kurekebisha tabia kutokana na unywaji wa dawa za kulevya. Wengi wa watoto huacha shule. Ni muhimu juhudi zichukuliwe kuwakinga watoto kutokana na matumizi ya dawa za kulevya na athari zake. Utafiti huu ulikusu kutafitia kuhusu taswira zilizotumiwa na waandishi wa matini teule katika fasihi ya watoto, kufafanua athari za matumizi ya dawa za kulevya na mielekeowa watoto kuhusu dawa za kulevya katika matini teule za watoto *Vioja vya Musa* (Mogambi 2007) *Atamlilia nani?* (Mohamed 2009) *Ah! Ajizi* (Nyambeka 2015).

Barani Afrika, Nchi zinazopatikana Magharibi mwa Afrika, Afrika ya Kati na Afrika ya Kaskazini aina ya bangi inayoitwa Tramado inayotumiwa kama tiba hutumiwa siku hizi kama dawa za kulevya. Mwaka wa 2016, Tramado ilisafirishwa katika maeneo ya Afrika kwa wingi. Mwaka wa 2016 kulingana na WHO bangi ilikuwa asilimia 87 ya idadi ya jumla ya dawa za kulevya katika ulimwengu mzima. Dawa za kulevya zikitoka maeneo ya Afrika zinauzwa Mashariki ya Kati na Mashariki ya karibu. (Mashariki ya kati na Karibu

Umoja wa Afrika ulikutana mwaka wa 1987 na kuunda chama cha Kimataifa cha siku ya kupambana na matumizi ya dawa za kulevya na usafirishaji wazo. Jukumu lake lilikuwa kupambana na dawa za kulevya katika nchi za Afrika na kuwa na jamii isiyo na matumizi ya dawa za kulevya. Viongozi waliunda kundi hili kwa kuwa waliona umuhimu wa kupambana na matumizi ya dawa za kulevya kupunguza matumizi yake. Katika mkutano wa mawaziri wanaohusu Shirika la Kupambana na dawa za kulevya na Jinai (CAMDCCP) mjini Kampala Uganda mwaka 2011 walijadiliana haya ya kujitolea kwa nchi za Umoja wa Afrika, kutumia raslimali kuanzisha vituo vya kuwarekebisha waathiriwa wa dawa za kulevya. Hata hivyo kuna changamoto nyingi kwa sababu si watu wengi wanauwezo wa kufikia vituo hivi. Dawa za bei ghali zinahitajika katika vituo hivi ambazo nchi nyingi haziwezi kujimudu.

Nchini Kenya masuala ya dawa za kulevya yanashughulikiwa na kundi linalofahamika kama NACADA (National Authority for the Compaign Against Alcohol and Drugs Abuse) iliyoundwa kupitia sheria za bunge tarehe 24 Julai 2012. Nchini Kenya kuna aina za dawa za kulevya ambazo ni pombe, kokini, gundi, tumbako, bangi, matumizi mabaya ya dawa zinazopeanwa hospitalini na daktari, miraa, heroini na matumizi ya dawa za kulevya. NACADA (shirika linaloshughulikia dawa za kulevya Nchini Kenya) imetwikwa majukumu ya kutoa leseni za kuendeleza shughuli za vituo vya kutibu na kurekebisha tabia za waathiriwa wa dawa za kulevya. Kuendeleza vituo vya kutibu na kurekebisha tabia kama hospitali ya Mathari na kuhakikisha kazi inayofanywa ni ya kiwango cha juu. Kutayarisha na kutoa ripoti kuhusu unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya kwa mabunge yote mawili.

Nchi ulimwenguni zimejizatiti kupambana na matumizi ya dawa za kulevya. Athari zimekuwa mzigo mkubwa kwa jamii ya waathiriwa kuwashughulikia kimatibabu. Pesa zinazotumiwa kununua dawa hizi za kulevya, zingetumika kujiendeleza kama mwathiriwa hakujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya. Pesa nyingi za nchi ambazo zingetumiwa katika kuendeleza nchi kimaendeleo zinatumiwa kuwatunza na kuwatibu waathiriwa.

Katika Ajenda ya 2030 kuhusu malengo ya kudumisha miradi ya maendeleo ulimwenguni (SDG) wakiwa na lengo la kuubadilisha ulimwengu kuwa mzuri.

Malengo haya ya Ajenda ya 2030 yalizungumziwa mwaka wa 2015 mjini New York. Katika mkutano huu walitambua umuhimu wa watoto, vijana, wanawake na wanaume katika mabadiliko kuufanya ulimwengu kuwa mahali pazuri pa kuishi. Katika lengo la 3.5 Ajenda hii ilisisitiza umuhimu wa kukaza uzuiaji na matibabu ya wale wanaoathiriwa na dawa za kulevya kama bangi, heroini, sigara na pombe. Walijua isingewezekana kufikia malengo yao pasipo kupambana na dawa za kulevya. Utafiti huu wa kuchunguza usawiri wa dawa za kulevya katika matini teule *Vioja vya Musa, Atamlilia nani?* na *Ah! Ajizi* ulisaidia kutoa onyo kwa watumiaji na kuwa ni njia moja ya kupambana na dawa za kulevya.

Katika Ajenda 2040 kulingana na mkutano uliofanywa katika jiji la Cape, 2013 waliuzungumzia umuhimu wa kuwafahamisha watoto, vijana na wazazi kuhusu matumizi ya dawa za kulevya kwa mtu binafsi, jamii na uchumi wa nchi. Kulishughulikia suala la dawa za kulevya na kushirikisha washiKandau wote naKuwa na mikakati ya kupambana na kuzuia matumizi ya dawa za kulevya. Ajenda ya 2040 ilionyesha umuhimu ulioko wa kupambana na kuzuia zaidi maenezi ya matumizi ya dawa za kulevya ili kufaulisha malengo ya kudumisha na kuendeleza miradi ya maendeleo (SDG).

Kulingana na shirika la UNODC ROEA (2019) viongozi wa Afrika kupitia Muungano wa Afrika waliona umuhimu wa kushughulikia masuala ya dawa za kulevya katika Ajenda ya 2063.Waliona ili kufaulu katika mikakati yao ya kuendeleza malengo ya maendeleo kwa miaka hamsini ijayo ni lazima wapambane na matumizi ya dawa za kulevya. Walizungumzia namna kuzuia na kutibu waathiriwa wa dawa za kulevya katika nchi zilizoko chini ya mwavuli wa Muungano wa Afrika. Waathiriwa wa virusi vya UKIMWI wanafaa watunzwe ili kuzuia kueneza zaidi maradhi ya UKIMWI.

Kupitia tafiti zilizosomwa na mtafiti, licha ya kuwa zinatafitia kuhusu maswala ya watoto katika Fasihi ya watoto ya Kiswahili hapajakuwa na utafiti uliochunguza usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya, kuchunguza matumizi ya taswira kusawiri matumizi ya dawa za kulevya, kueleza athari za dawa za kulevya na kutathimini mielekeo wa watoto kuhusu matumizi ya dawa za kulevya, katika matini teule za Fasihi ya watoto ya Kiswahili.

## 2.6 Kiunzi cha Nadharia

Nadharia nyingi za hapo awali zilijikita katika kuchunguza usomaji wa Ki-historia ili kupata maudhui ya matini Ki-muktadha. Walichunguza matini kwa msingi ya kiutamaduni, kijamii, kisiasa na kiuchumi ili kujua masharti yaliyopelekea kuandikwa na kupokelewa kwa matini. Usomaji huu hukushughulikia athari au utaratibu wa usomaji kwa msomaji mwenyewe. Usomaji huu ulijihusisha na jinsi tanzu za kimatini zinasomwa na kufasiriwa katika muktadha wa ki-wakati au ki-historia. Kwa kutumiua vigezo vifuatavyo; akili yake, misingi ya kijamii, misingi ya kiuchumi, kiutamaduni, kijiografia, msingi ya kiisimu, kihistoria, kisaikolojia na umbo la matini. Masuala huwa katika ulimwengu wa msomaji na huwa amekumbana nayo. Akili ya awali kuhusu matini humsaidia kuelewa zaidi.

Kwa mujibu wa Phelan (2005) ni kuwa kitendo cha kusoma huwa na maadili. Usomaji huu unahusisha mambo yafuatayo: kutoa uamuzi kuhusu maudhui ya mwandishi, kutamani kujua zaidi au kutenda kulingana na mawazo ya mwandishi wa matini, kutoa hisia za msomaji na hatimaye kutenda matendo ya kimaadili yanayopendekezwa na jamii husika. Katika harakati za kupata maana ya matini inayosomwa, msomaji anaweza kukubaliana na maoni au lengo la mwandishi, msomaji anaweza kashifu au kuisahili matini kwa kujiuliza maswali kadha wa kadha.

Suala na mchango wa msomaji ulipuuzwa katika nadharia za kifasihi za hapo awali zilizojishughulisha na mwandishi wa matini katika nadharia za ki-historia au za zamani. Nadharia za uhakiki wa kisasa zilijihusisha na uchambuzi wa matini kama njia ya kupata maana ya kimatini. Nadharia ya Mwitikio wa Msomaji iliyoanzishwa miaka ya 1960-1970. Watafiti wa Mwitikio wa Msomaji wanachunguza tajriba ya usomaji na uchangamano uliopo kati ya msomaji na matini, msomaji na muktadha wa usomaji katika matini ambazo ni za kifasihi.

Nadharia ya Mwitikio wa Msomaji ni zao la waasisi mbalimbali waliokuwa na nadharia mbalimbali zilizokuzwa na kuunda nadharia ya Mwitikio wa Msomaji. Katika miaka ya 1960 na 1970, kulikuwa na mabadiliko katika nadharia za kifasihi ya kuchukulia kuwa matini ndiyo ilikuwa na uzito mkubwa. Kukawa na kumchukulia msomaji kuwa muhimu kulitokana na mawazo ya makundi au matapo matatu. Tapo la kwanza lilikuwa

la waasisi walioamini kuwa matini zisomwe na kuchambuliwa kwa njia ya uchanganuzi. Waasisi wa tapo ili ni Louise Ronsenblatt, Wolfgang Iser na Hans Robert Jauss.

Tapo la pili ni la wanasaikolojia ambao ni Norman Holland na David Bleich. Nalo kundi la tatu ni mwanautamanduni na kijamii ambaye ni Stanley Fish. Nadharia hizi zilichangiwa na mageuzi ya kiutendaji katika kueleza uhusiano uliopo kati ya mwandishi na msomaji, mosomaji na matini. Nadharia hii ilitumika na Mmarekani mhakiki wa kifasihi Louise Rosenblatt kama mkakati wa kuitalii fasihi (1938). Kulingana na Sumara, (1996) ni kuwa Rosenblatt aliona kuwa usomaji wa kazi au matini za kifasihi ni mahala ambapo msomaji na matini ukutania. Rosenblatt alishikilia kuwa matini ni chombo cha karatasi na rangi na hakingekuwa na maana mpaka msomaji atolee ishara zilizo karatasini maana ambayo ndiyo mwitikio wake kuhusu matini husika. Msomaji anaongozwa na lengo la usomaji kuwa tendo la usomaji upatikana katika harakati ya usomaji. Usomaji unaibua mitazamo miwili; kuna matini ya msomaji kwa yale yanayosomwa wakati wa usomaji na pili ni yale yanayohifadhiwa baada ya tendo la usomaji. Rosenblatt anasema kuwa si utafsiri wote unakubalika. Anapendekeza mbinu za kufanya utafsiri uwe unakubalika, uendelezwa kutokana na yale yanayokubalika kwa sababu zina timiza matarajio yanayokubalika kuliko utafsiri mwingine.

Mjerumani mwanafenomenolojia Wolfgang lser wakiwa na Hans Robert Jauss (1960 - 1970) walitetea wazo kuwa somo la usomaji na upokeaji wa matini za kifasihi ni muhimu. Waliona kuwa msomaji wa matini na matini yenyewe huchangiana ili kuibua maudhui ya matini. Walipinga wazo la wahakiki wa awali kuwa mbinu za kifasihi ambazo zinasisitiza utoaji wa matini na uchanganuzi wa matini bila kuhusisha msomaji. Iser anashikilia kuwa kuna masuala mawili muhimu wakati wa kushughulikia kazi za kifasihi; Usanaa yaani matini iliyoandikwa na mwandishi.

Kuna ung’amuzi wa msomaji baada ya kusoma matini. Iser anasema kuwa kwa sababu ya mianya iliyoko katika matini ya kifasihi kazi ya kifasihi haiwezi ikafanana na kuwa sawia na matini. Maana ya kifasihi haipatikani kwa matini pekee na haiwezi ikaegemezwa kwa msomaji pekee. Utafakari wa msomaji unasisimuliwa na mianya

iliyoko katika matini inayokamilishwa na tajiriba ya msomaji. Iser kwa maoni yake anaona kuwa umuhimu wa msomaji unapaswa kutiliwa maanani wakati wa kuchambua matini. Waasisi wa tapo la tatu walishikilia kuwa maana za matini za kifasihi na tafsiri iwe ni kazi ya msomaji, pasipo kujali hali za miundo ya matini na ishara za ki-Isimu.Waasisi wa tapo hili ni Norman Holland na David Bleich. Msingi wa Norman Holland (1975) ni Saikolojia changanuzi. Holland anashikilia kuwa Mwitikio wa Msomaji kwa matini za kifasihi ni masuala ya kihisia, yanayoathiriwa na mahitaji ya kisaikolojia ya mtu binafsi. Holland anasema kuwa wasomaji huchota kutoka kwa hazina ya kazi ya kifasihi inayomwezesha kujiundia sifa zao kwa kutumia utaratibu wa kisaikolojia.

Utaratibu wa usomaji kulingana na Holland ni kuwa unapendelea sana tajiriba ya msomaji na kupuuza miundo ya matini ya mitindo ya waandishi wa matini. Miundo ya matini na mitindo ya waandishi humsaidia msomaji kuelewa mitindo ya wandishi mbalimbali. Msomaji uelewa muundo wa matini. Kwa hivyo sehemu ya miundo na mtindo haiwezi kupuuzwa katika uchambuzi wa matini. Rosenblatt, Iser na Juass wote wanakubaliana kuwa ni muhimu kuhusisha mchango wa msomaji na matini na si matini pekee. Holland (1975) na Bleich (1978) wanasisitiza uzingativu wa saikolojia ya msomaji. Haya ni yale msomaji anapitia akilini mwake anaposoma matini za kifasihi. Fish kwa upande wake anasisitiza msomaji kujikita katika kutazama muktadha wa kijamii na kiutamaduni.

Msomaji yeyote wa kazi ya matini aelewe kuwa masuala ya kijamii na kiutamdauni ni muhimu kuzingatiwa wakati wa usomaji na uchambuzi wa matini za kifasihi. Nadharia ya Mwitikio wa Msomaji inaweza kutumika kuhakiki matini za kifasihi kama riwaya, mfano za kibunilizi, ushairi, tamthilia na hata hadithi fupi. Nadharia hii inatumika kuhakiki kumbukizi. Mtafiti baada ya kuipitia nadharia hii amegundua kuwa inafaa sana katika utafiti huu kwa kuwa matini zinazochambuliwa ni za kifasihi. Mtafiti aliwapa watoto matini teule; *Vioja vya Musa* (Mogambi 2007), *Atamlilia nani?* Mohamed (2009) na *Ah! Ajizi* (Nyambeka 2015). Watoto walijibu hojaji na kushirikishwa katika dodoso kupitia mijadala ya kimakundi ili kupata mielekeo wao.

Nadharia hii ya Mwitikio wa Msomaji ina mihimili yake inayotumiwa kuchunguza kazi za kifasihi. Mihimili hii ni Usomaji na upokezi. Msomaji wa kazi ya kifasihi upokea akilini mwake yale anayopitia katika Usomaji wa matini. Upokeaji wa msomaji wa Matini hutokana na kuelewa kwake na tajriba yake. Katika kuichanganua kazi ya Kifasihi, msomaji anachukuliwa kuwa ataupokea ujumbe ulio kusudiwa na mwandishi wa matini. Watoto walipopewa matini wasome, ilichukuliwa wataelewa na wachukue hatua ya kujibu maswali ya Hojaji na kushiriki mijadala ya kimakundi. Mhimili huu ulitumika kushughulikia lengo la pili la utafiti ambalo ni kueleza athari za dawa za kulevya. Ili waweze kujibu maswali, lazima waelewe.

Mhimili wa pili ni kuwa kuna picha zinazomjia msomaji akilini mwake. Ung'amuzi wa msomaji hutokana na tajriba ya mtu mwenyewe. Picha za akilini humjia msomaji na kumwezesha kuelewa matini vizuri. Picha zinazomjia msomaji akilini ndizo huwa ni taswira, kwa mfano harufu ya kitu fulani ambayo imerejelewa na mwandishi huwa msomaji ameinusa awali na anapoelezewa na mwandishi wa matini huweza kuilinganisha harufu ya awali na inayosimuliwa katika hadithi. Mhimili huu ulitumika katika lengo la kwanza ambalo ni kufafanua aina za taswira zilizotumiwa na waandishi wa matini teule kusawiri dawa za kulevya.

Mhimili wa tatu kulingana na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji ni kuwa msomaji wa matini huchukua hatua fulani baada ya kuisoma na kuielewa matini. Hatua inayochukuliwa na msomaji hutokana na yale amekumbana nayo anapoisoma matini husika. Msomaji atakuwa na mielekeo fulani kuhusu yale aliyoyasoma. Huenda akakubaliana nayo. Akikubaliana nayo atakuwa na mielekeo chanya. Huenda msomaji akapinga yale ameyasoma. Akipinga basi atakuwa na mielekeo hasi. Mhimili huu ulitumika kushughulikia lengo la tatu ambalo ni kutathimini mielekeo wa watoto.

**2.7 Hitimisho**

Katika sura hii mambo yaliyoshughulikiwa ni: Utangulizi, Maandishi kuhusu fasihi ya watoto, dhana ya dawa za kulevya na kiunzi cha nadharia. Tafiti za wataalamu zilirejelewa na kuangazia uhusiano wa tafiti hizo na huu. Mchango wa tafiti zilizorejelewa ulielezewa. Katika sura iliyofuata mbinu za utafiti zilishughulikiwa.

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti alishughulikia mbinu za utafiti kwa kushughulikia, mpango wa utafiti, vifaa vya utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data.

### 3.2 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ni wa maktabani na nyanjani. Mtafiti alikusanya data kwa kuvisoma vitabu teule vya fasihi ya watoto ya Kiswahili. Matini hizi ni *Vioja vya Musa* (Mogambi, 2007) *Atamlilia nani?* Mohamed (2009) *Ah! Ajizi*, Nyambeka (2015). Mtandao na majarida yalirejelewa ili kupata maoni ya watafiti wengine. Matini teule zilitumika kama kiwakilishi cha fasihi ya watoto ya Kiswahili. Mtafiti alitafiti nyanjani ili kupata mielekeo wa moja kwa moja wa watoto kuhusu matumizi ya dawa za kulevya. Utafiti wa maktabani uliweza kupata data kuhusu taswira zilizotumiwa na waandishi kuelezea matumizi za dawa za kulevya na athari zake. Mtafiti alisoma matini teule ili kujifahamisha na yale yaliyo andikwa. Watoto wasailiwa walipewa matini hizo ili kusoma ili waweze kujibu maswali ya Hojaji ya Mizani ya Likert.

### 3.3 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa Sampuli hutegemea aina ya data ambayo mtafiti huhitaji na upatikanaji wa data anayohitaji katika utafiti wake (Mugenda na Mugenda, 1999) wanasema idadi ya sampuli itakayochaguliwa lazima iwe na sifa nyingi kama vile wajibu unao faa, upatikanaji, ujuzi na mwongozo wa utafiti. (Nsubuga 2000) anasema sampuli bora ni ile inayoleta data inayotarajiwa. Mtafiti ahakikishe kuwa sampuli yake ni ile inamfaa kupata data. Uteuzi wa sampuli wa kimakusudi ulitumika kwa sababu mtafiti alikusudia kupata data inayohusu usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Matini hizi zilizochaguliwa kwa kuwa zina data ya kutosha iliyokusudiwa kutimiza malengo ya utafiti. Pia matini hizi ni za watoto kwa kuwa mhusika mkuu ni mtoto. Yanayozungumziwa yanahusu watoto. Matini zilizoteuliwa ni; *Vioja vya Musa* (Mogambi, 2007) *Atamlilia nani?* (Mohamed, 2009) *Ah! Ajizi* (Nyambeka, 2015).

Kupata mielekeo wa watoto na uelewaji wao kuhusu matumizi ya dawa za kulevya, Utafiti wa nyanjani ulifanyika katika tarafa ya Nkondi wilaya ya Tharaka Kusini,

Kaunti ya Tharaka Nithi kuwakilisha Tarafa zingine nne. Jumla ya kata ni tatu: Nkondi, Matakiri na Mwanyani Shule moja ilichaguliwa kwa kila Kata kwa misingi ya kuwa karibu na soko, ilipatikana kijijini na shule ya kibinafsi. Mtafiti alichagua shule ya Premier Junior iliyo katika kata ya Matakiri na ni ya kibinafsi, pia shule ya Miomponi iliyo katika kata ya Mwanyani ambayo ni ya umma na ilipatikana mashinani. Shule ya Karou iliyopatikana katika kata ya Nkondi na iko karibu na soko la Nkondi, ni ya umma, shule ya bweni na kutwa. Wanafunzi sita, wavulana watatu na wasichana watatu kutoka kila shule walishirikishwa kwa utafiti huu. Watoto hawa walishirikishwa kwa msingi wa kijinsia. Kwa jumla wanafunzi wote walio shirikishwa ni kumi na nane kutoka darasa la sita hadi la nane.

Jedwali 2: Wasailiwa waliochaguliwa

| Jina la Shule | Darasa | Wavulana Wasailiwa | Wasichana Wasailiwa | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Miomponi | 6 | 1 | 1 | 2 |
| | 7 | 1 | 1 | 2 |
| | 8 | 1 | 1 | 2 |
| Premier | 6 | 1 | 1 | 2 |
| | 7 | 1 | 1 | 2 |
| | 8 | 1 | 1 | 2 |
| Karou | 6 | 1 | 1 | 2 |
| | 7 | 1 | 1 | 2 |
| | 8 | 1 | 1 | 2 |
| JUMLA | | 9 | 9 | 18 |

### 3.4 Vifaa vya Utafiti

Mtafiti alitumia hojaji na dodoso ya mijadala ya makundi katika utafiti wa nyanjani. Mtafiti aliwapa matini teule za kusoma kisha akawapa hojaji ili wajibu na kuwashirikisha katika mahojiano ya mijadala ya makundi. Majibu ya watoto yalichambuliwa ili kupata uelewaji na mielekeo wao kuhusu matumizi ya dawa za kulevya katika fasihi ya watoto. Mihimili ya nadharia ya Mwitikio wa Msomaji na malengo ya utafiti yalitumika kuchanganua data. Data iliyochanganuliwa iliwasilishwa kwa njia ya maelezo

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Ili kupata data iliyotarajiwa, mtafiti alichambua matini tatu teule za watoto; *Vioja vya Musa* (Mogambi, 2007) *Atamlilia nani?* (Mohamed, 2009) na *Ah! Ajizi* (Nyambeka,

2015). Kwa kuwa kazi hizi zinashughulikia masuala ya matumizi ya dawa za kulevya zilichambuliwa kwa kuangazia malengo ya utafiti, na kutathmini mielekeo wa watoto kuhusu matumizi ya dawa za kulevya. Utafiti wa nyanjani ulishirikisha watoto waliochaguliwa kusoma matini teule na kujibu maswali ya hojaji kutokana na matini teule ili kutathimini kuelewa kwa mtoto kuhusu matumizi ya dawa za kulevya na athari zake, mielekeo wao kuhusu matumizi ya dawa za kulevya ulitathiminiwa kupitia hojaji na mahojiano ya kushiriki mijadala. Data ya kinathari ilikusanywa. Ili kupata data iliyotarajiwa, mtafiti alizichagua matini ambazo zilikuwa zimeshughulikia athari za matumizi ya dawa za kulevya kwa watoto. Matini tatu za waandishi tofauti tofauti zilichaguliwa. Matini teule zilizochaguliwa ni riwaya za watoto. Mtafiti alikusudia kuwapa watoto wasailiwa matini wasizome na kisha kujibu maswali ya hojaji, kushiriki mjadala wa kimakundi.

Mtafiti alipata kibali cha Utafiti cha Chuo Kikuu chaa Chuka. Kisha alikitumia kibali cha Utafiti kupata kibali cha NACOSTI, taasisi ambayo inayopatiana kibali cha utafiti Nchini. Mtafiti alitembelea maktaba ya Vyuo vikuu yaliyolengwa kama vile; Chuka, K.U, Nairobi na KEMU. Lengo kuu lilikuwa kupitia majarida na majuzuu ambayo yangechangia ufanisi wa utafiti huu. Nyanjani, mtafiti alizichagua shule tatu kutoka kata tatu kuwakilisha shule zingine katika Tarafa nzima ya Nkondi, Kaunti ndogo ya Tharaka Kusini na Gatuzi la Tharaka Nithi kwa jumla. Kwa kila shule kuliteuliwa wasailiwa sita, kwa misingi ya kijinsia na kuanzia darasa la sita walichaguliwa. Kila darasa watatu wakiwa wavulana na wasichana. Ilichukuliwa kuwa wanafunzi wa darasa la sita hadi la nane wangekuwa na ufahamu kuhusu dawa za kulevya. Kila darasa mtafiti aliwafahamisha watoto kuhusu utafiti. Waliandikiwa ‘*Ndio*’ tatu kwa wavulana na kwa wasichana. Karatasi hizo zingine ziliandikwa ‘*La*’. Wale wote waliookota ‘*Ndio*’ walishirikishwa katika utafiti.

Wasailiwa walipewa matini za kusoma na baadaye wajibu maswali ya hojaji na kushiriki mijadala ya kimakundi. Majibu ya kila swali yalitiliwa maanani sana kwa kuwa yalikuwa data ya kimsingi. Maoni yao katika mijadala ya kimakundi ilikuwa muhimu kuelezea mielekeo wa watoto kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya kwa watoto wanaozitumia. Data iliyokusanywa kutokana na maswali ya hojaji na mijadala ya kimakundi ndiyo iliyochanganuliwa. Mtafiti aliwapa watoto walioteuliwa

nakala teule za kusoma kwa muda wa majuma mawili. Baada ya kusoma nakala teule, mtafiti aliwapa wasailiwa hojaji funge wasijaze. Baada ya kujaza maswali funge, mtafiti aliwapa maswali funge na huru wajadili ili kupata mielekeo wao kuhusu dawa za kulevya. Mjadala wa ana kwa ana unaweza kumsaidia mtafiti kusoma hisia za mhojiwa ambazo zinaweza kushuhudiwa kupitia ishara za uso au macho. Mtafiti huweza kuona kama msailiwa anaonyesha huzuni, furaha au yote wawili.

## 3.6 Uchanganuzi wa Data

Mtafiti baada ya kupata data maktabani na nyanjani, akizingatia mihimili ya nadharia ya Mwitikio wa Msomaji na malengo ya utafiti aliichanganua. Mbinu elezi ni mbinu mwafaka ambayo hujaribu kuchanganua data hasa ya kinathari kwa maelezo. Data ilichanganuliwa kwa maelezo kwa kueleza jinsi aina mbalimbali za taswira zilivyotumiwa kuelezea usawiri wa dawa za kulevya katika matini teule za fasihi ya watoto ya Kiswahili. Hatua zilizofuatwa kuchanganua data zilielezwa.

Kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia husika alibainisha taswira zilizotumiwa na waandishi wa matini kuelezea matumizi ya dawa za kulevya katika fasihi ya watoto. Athari za matumizi ya dawa za kulevya zilizojidhihirisha katika matini teule za fasihi ya watoto zilifafanuliwa. Hatimaye mtafiti alielezea kuhusu mielekeo wa watoto kuhusu dawa za kulevya kama ulivyojidhihirisha katika hojaji na mahojiano ya watoto. Ili kutekeleza uchanganuzi huu wa data mtafiti alishirikisha malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia ya Mwitikio wa Msomaji. Utafiti huu ulinuiwa kupima mielekeo wa watoto kuhusu dawa za kulevya katika matini teule za fasihi ya watoto ya Kiswahili. Mtafiti alitumia vifaa viwili: Hojaji ya Likert, na Dodoso ya maswali ya majadiliano ya kimakundi. Kwanza mtafiti alichanganua Hojaji ya Mizani ya Likert, kisha dodoso za mijadala wa kimakundi.

## 3.7 Uwasilishaji wa Data

Data iliyochanganuliwa kwa kuchambua matini teule, maswali ya hojaji na mjadala wa kimakundi, iliwasilishwa kwa maelezo. Maelezo yaliyotolewa yalishirikisha malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya Mwitikio wa Msomaji. Maelezo ya matokeo yalikusudiwa kubaini kuwa malengo ya utafiti yaliafikiwa au la. Maelezo ya kila lengo yalizingatiwa aya kwa aya. Data kuhusu mielekeo wa watoto iliwashilishwa kwa

kutumia majedwali mbalimbali kulingana na maswali ambayo yalihitajika kujibiwa na wanafunzi au maswali ambayo yalihitajika kujadiliwa na wanafunzi au wasailiwa. Data iliwasilishwa kwa kutumia michoro mbalimbali inayowakilisha data lengwa.

### 3.8 Maadili ya Utafiti

Ili kutimiza malengo ya utafiti huu, mtafiti aliyashughulikia masuala yafuatayo. Kwanza mtafiti alipata barua ya utafiti Chuoni. Mtafiti alipata kibali cha kufanya utafiti kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi. Mtafiti alipata idhini ya Mkuu wa Elimu wilayani, walimu wakuu wa shule na wazazi wa watoto wasailiwa. Mtafiti alistahili kuwa na uwazi na uadilifu wakati wa utafiti wake. Haki za watoto zilizingatiwa, uhuru wa kutoa maoni yao na kuwa na usiri. Data iliyokusanywa, ilichanganuliwa na kuwasilishwa.

### 3.9 Hitimisho

Sura hii ilishughulikia mpangilio wa utafiti, vifaa vya utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa data na maadili ya utafiti. Sura iliyofuata ilishughulikia uchanganuzi wa taswira zilivyotumiwa kusawiri matumizi ya dawa za kulevya kwa kuongozwa na mhimili wa taswira zinazomjia msomaji akilini anapoisoma matini, kwa mujibu wa nadharia ya Mwitikio wa Msomaji.

# SURA YA NNE

# AINA ZA TASWIRA ZINAZO JIDHIHIRISHA KATIKA MATINI TEULE ZA FASIHI YA WATOTO YA KISWAHILI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti alishughulikia mhutasari wa matini teule; *Vioja vya Musa*, *Atamlilia nani?* na *Ah! Ajizi*. Taswira ni dhana inayotumiwa kuelezea neno, kirai au maelezo yanayohunda picha fulani akilini mwa msikilizaji au msomaji. Taswira huweza kuundwa kwa kutumia maelezo yanayohunda picha akilini mwa mtu. Tashbihi na sitiari hutumiwa kuunda picha akilini mwa msomaji. Picha hizi za akilini huwa na mvuto na mnato kwa msomaji na kumpelekea kushawishika kuwa na hamu na makini anapoisoma matini na kwa hivyo kuchangia kuielewa matini barabara.

## 4.2 Muhtasari wa *Vioja vya Musa*

Matini ya *Vioja vya Musa* iliandikwa na Hezron Mogambi mwaka wa 2007, na kupigwa chapa na Moran publishers mwaka wa 2007. Imegawanyika katika sehemu nne kuu. Musa akiwa shuleni Kaachonjo baada ya kugharamiwa masomo na mwajiri wa babake. Shuleni alianza kutumia na kuuza dawa za kulevya. Pili ni katika uwanja wa Kaachonjo walipozusha vurugu na vijana wengine wakiwa wametumia dawa za kulevya na kuwapelekea kukamatwa na polisi. Sehemu ya tatu ni Musa akiwa kifungoni katika shule ya kurekebisha tabia. Musa alizidisha matumizi ya dawa za kulevya zilizomharibu kabisa. Nne, ni maisha ya Musa baada ya kutumikia kifungo. Aliporudi nyumbani, alikataa katakata kurudi shuleni na kuwa hamali. Alizidisha ulevi wa pombe na bangi, hadi walipoiba nyanya wakakamatwa na polisi. Jamii inafunzwa kutunza, kuwaelekeza na kuwarudisha watoto ili kuepukana na athari za dawa za kulevya.

## 4.3 Muhtasari wa *Atamlilia nani?*

Matini ya *Atamlilia nani?* Iliandikwa na Said. A. Mohammed mwaka wa 2009 na kuchapishwa na Oxford University Press mwaka wa 2009. Hadithi imegawanyika katika sehemu tatu muhimu. Kwanza, ni kuzaliwa kwa mtoto Sembuli na wazazi wake Bi. na Bwana Bosire. Maisha yake kabla ya kuhitimu kujiunga na shule ya upili. Sembuli alikuwa mwingi wa hamaki. Vitendo vyake viovu vinamwonyesha kuwa mtoto asiye na adabu. Sehemu ya pili ni maisha ya Sembuli alipokuwa shuleni, shuleni na nyumbani alikuwa mtoto mkaidi sana. Akawa mlevi wa pombe, bangi iliyomharibia maisha yake, Sehemu ya mwisho, ni maisha ya Sembuli baada ya kuacha shule na

kuendelea kuwa mwizi wa kuku na mabata wa watu. Sembuli akawa mlevi na mtumiaji wa dawa za kulevya. Akawa mchokozi mkuu na mbakaji wa mabibi na mabinti wa watu. Akajiunga na genge la wahuni. Sembuli aliwachokoza vilema na kuyaharibu mali ya maskini bila sababu nao wakamlaani. Alipigwa risasi na babake alipotaka kumwibia babake pesa zake. Hadithi hii ni funzo kwa jamii kuwa mihadarati ina athari kubwa sana kwa wanaoitumia, na jamii kwa jumla.

### 4.4 Muhtsari wa *Ah! Ajizi*

Matini ya *Ah! Ajizi* iliandikwa na Tom Nyambeka mwaka wa 2015 na kupigwa chapa na kampuni ya No Boundaries mwaka wa 2015.Ajizi na Juhudi ndio wahusika wakuu. Imegawanyika katika sehemu tatu kuu. Sehemu ya kwanza ni Ajizi alipojiunga na shule ya Msingi, alivyokuwa mwenye bidii sana masomoni na alikuwa anafanya vizuri sana masomoni. Sehemu ya pili ni pale Ajizi alipoanza kutumia mihadarati, akawa mtukutu shuleni na kwa wazazi wake. Ajizi alidorora masomoni na kuanza kuburura mkia masomoni. Sehemu ya tatu ni pale Ajizi alipojiunga na kundi la watoto wahuni. Ajizi akaacha shule na kutoroka nyumbani na kuenda kuishi msituni. Ajizi alizidisha matumizi ya mihadarati, hadi akapagawa na hatimaye kufariki dunia. Hadithi hii ina funzo kubwa kwa watoto wa aina ya Ajizi ambao ujiingiza katika uraibu wa dawa za kulevya na kujiangamiza wenyewe huku wakijiharibia maisha yao wenyewe. Hadithi hii ni funzo kwa wanajamii. Kujua majukumu ya kuwaelekeza watoto wao na kuwaonya kuhusu athari za uraibu wa mihadarati.

### 4.5 Aina za taswira zilizojidhihirisha katika matini teule

#### 4.5.1 Taswira za Kimaelezo

Ili kutimiza lengo la kwanza la utafiti huu ambalo ni kufafanua taswira zilizojithihirisha katika matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule za fasihi ya watoto ya Kiswahili. Mtafiti alikusudia kufafanua taswira mbalimbali zilizotumiwa na waandishi wa matini: *Vioja vya Musa*, *Atamlilia nani?* na *Ah! Ajizi*: Mtafiti aliongozwa na mhimili wa nadharia ya Mwitikio wa Msomaji unaozingatia; Hisia za kimawazo na picha zinazomjia msomaji akilini baada ya kuisoma matini. Kulingana na Wamitila (2003) taswira za kimaelezo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi. Mwandishi anatumia lugha ambayo ina uwezo wa kujenga picha fulani katika akili ya msomaji

wake. Picha hizo zikijengeka akilini mwa msomaji humsadia kuielewa matini vizuri. Huweza kujua dhamira kuu ya matini na maudhui yanayojenga dhamira hiyo.

Suala la umaskini wa Musa lilielezewa na mwandishi wa *Vioja vya Musa*, Mugambi, mpaka maelezo yake yakaichora picha kamili ya umaskini, akilini mwa msomaji. Musa alisemekana kutoka katika aila maskini inayochangia umaskini wake. Tonui (2010), anasema kuwa masuala ibuka yana waathiri watoto kwa njia moja au nyingine. Musa aliyokuwa mwadilifu na mwenye bidii aliathirika vibaya kutokana na umaskini mpaka akabadilika na kuwa mtoto mbaya. Mwandishi alisema kuwa Musa alitimuliwa shuleni kwa kukosa karo. Akafadhiliwa na mwajiri wa babake akajiunga na shule ya malezi ya Kaachonjo. Kwa sababu ya umaskini hakuwa na pesa za masrufu. Hakuweza kununua kitafunio. Alichekwa sana na watoto wenzake akaudhika sana. Kila wakati alikuwa mwenye huzuni. Picha ya umaskini inajengeka akilini mwa msomaji na kumwona jinsi Musa alivyokuwa katika hali ngumu ya kimaisha. Picha ya uchochole wa Musa inajitokeza wazi. Mwandishi alielezea kuwa:

> “Musa hakujimudu kununua mkate. Hakuwa na pesa. Kwa hivyo, wakati mwingi alikunywa chai bila kitafunio. Ole wao baadhi yao kama Musa ambao walikosa pesa za kununua vitafunio. Walionekana kama mayatima pale shuleni huku wengine wakiwacheka!’’ *Vioja vya Musa* 2007:3-4

Kulingana na Kairu (2009) kuwa yale yaliyoandikwa katika matini ndiyo hayo yaliyowakumba watoto katika jamii halisi. Hali ya umaskini wa Musa haikuwa rahisi, ilikuwa ngumu sana na kuyatatiza maisha yake ya baadaye. Mwandishi alisema.

> “Wanafunzi wa shule walipoenda michezoni, Musa hakuwa na pesa zozote na aliishia kuombaomba. Wenzake waliponunua na kubeba mapochopocho. Musa alirudi shuleni mikono mitupu. “Hali hii ilimsukasuka sana na kumzonga akili sana. Hali hii ikamkosesha raha shuleni. Musa akawa mtoto wa kushika tama na kuhuzunika moyoni” *Vioja vya Musa* 2007:3-5

Maelezo haya ya mwandishi yanamfanya msomaji kuona picha ya umaskini wa Musa na athari zake ambazo ni huzuni, mawazo mazito akilini. Msomaji vile vile huelewa ni kwa nini Musa aliishia kufanya vitendo viovu vya kutumia na kuuza bangi.

Kama anavyosema Kairu (keshatajwa), Musa ni mfano wa watoto wengi wanaoteseka katika jamii halisi. Wengi wanapitia wakati mgumu kwa ajili ya umaskini. Musa aliyekuwa mtoto mtiifu, mwadilifu, mwerevu, mwenye bidii na kiongozi mzuri aliishia kuacha shule na kuwa mtu ovyo. Umaskini ulimwathiri na kumpelekea kuanzisha biashara ya kuuza mihadarati. Akafukuzwa shuleni, Nyota yake iliyong'aa ikazimika. Ni kweli kuwa watoto wengi katika jamii halisi wanapitia hali ya umaskini kama Musa wa jamii ya matini alivyopitia. Wengi katika hali ya jamii halisi wanakuwa na nidhamu mbaya kutokana na matumizi ya mihadrati kwa sababu ya hali yao ngumu ya maisha inayosababishwa na umaskini. Wengine huacha shule na wengine wakiangamizwa na mihadarati hiyo. Nafasi zao za kujenga kesho yao huharibika na kufika kikomo. Wengi ndio huwa wakora katika jamii.

Hali ya Musa na yale yote yaliyompata kama vile kukamatwa na polisi, kufungiwa katika seli na kufungwa katika shule ya kurekebisha tabia ni mifano inayowakumba watoto wengi katika jamii halisi. Hili ni funzo kwa wanajamii kuwa wayashugulikie mahitaji ya kimsingi ya mtoto. Walezi wa watoto, walimu, viongozi wa kanisa na Kiserikali wanapaswa kuichunguza mienendo na tabia za watoto ili kuwaelekeza na kuwarudisha mapema kabla hawajatumbukia katika lindi la maangamizi. Ni muhimu watoto washauriwe katika hali zao za kimaisha wajielewe na waweze kupambana nazo ili wasitumbukie katika ulanguzi wa mihadarati.

Ni muhimu walezi wa watoto na washika dau wengine waelewe kuwa watoto wakiathiriwa hawajali hata kutenda vitendo vya kuhatarisha maisha yao. Mwandishi wa *Vioja vya Musa* alieleza jinsi Musa na wenzake walileta vurugu ugani Kaachonjo. Alielezea vita vilivyotokea na kusababisha majereha kwa watu wasio na hatia, watoto hao waliyafanya hayo kwa msukumo wa bangi. Mwandishi aliichora picha ya vita pale ugani, mpaka msomaji anaipata na kuona jinsi mambo yalivyokuwa hata kama hakuwepo. Msomaji huwa na hisia fulani la tendo hili kama mhimili wa Mwitikio wa Msomaji wa hisia zinazomjia msomaji wa matini unavyopendekeza.

> "Zana za kila aina zilitumiwa na mashabiki pinzani kupigana, si mawe, chupa, miereka machungwa, mayai viza. Zana hizi zote zilivurumishwa ugani mpaka kukawa kila mtu ni mguu ni ponye. Askari walipokuja walitumia kila aina ya zana kutuliza sokomoko

> pale ugani. Wengi wakajeruhiwa vibaya sana." *Vioja vya Musa* (2007: 33-35)

Wamitila (2003) anasema kuwa taswira za kimaelezo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi. Yale maelezo yanayotolewa na mwandishi kuhusu mtu, kitu au jambo Fulani humfanya msomaji kuwa na picha Fulani ya kile kinachozungumziwa. Maelezo ya mwandishi wa matini ya *Vioja vya Musa*, alichora picha ya vile vita vilikuwa vikali wakitumia kila aina ya silaha ikitumika. Watu wakakimbilia usalama wao. Picha hiyo ilijitokeza vizuri. Mwandishi alimtumia mhusika hakimu kuelezea kuwa wale watoto walikuwa chini ya msukumo wa mihadarati. Msomaji anaelewa kisa kilivyokuwa pale ugani Kaachonjo. Vita vilivyoendelezwa pale ugani kuna mfanya msomaji kuwa na hisia za vita na madhara yake. Chanzo cha vita kilikuwa ni athari ya mihadarati.

> "Vijana ni lazima waepukane na mihadarati kwani inaharibu maisha yao. Ripoti ya daktari iliyofikishwa hapa inaonyesha kuwa vijana waliosababisha fujo na ghasia katika uwanja wa kandnda wa Kaachonjo huwa wanatumia mihadarati '*Vioja vya Musa* (2007:41)

Mwandishi wa *Atamlilia nani?* Aliyatoa maelezo ya kuhusu ukatili wa Sembuli wa vitendo alivyo vitendo, kudhihirisha ukatili wake. Sembuli alionyesha mawazo na hisia zake kwa njia ya vitendo vilivyodhihirika. Kweli Sembuli alifanya yote aliyoyafanya kwa msukumo fulani. Sembuli alikuwa na hisia potovu. Mwandishi alielezea kuwa Sembuli alizoea mara kwa mara kuugonganisha mlango kwa kishindo ili kuonyesha hasira yake. Alimfanyia mamake kila aina ya vitimbi. Alimdharau sana akampiga na kummwagia mchanga na kumtusi hadharani, Sembuli alisikia sauti ikimwambia avifanye vitendo viovu kila wakati Sembuli hakuwa na heshima kwa mama yake mzazi. Alimfokea na kumrushia vitu na kumfanyia madharau ya kiwango cha juu. Sembuli alisimama mbele ya mlango wa nyumba kwa muda huku akipima athari ya matendo yake. Alijua alilolitenda ni mbaya lakini hakuweza kujizuia. Maelezo ya mwandishi kumhusu Sembuli yanaafiki maoni ya (Cuddon, 2013), kuwa mtu aliyeathirika kiakili anaweza kuvitenda vitendo vya utovu wa nidhamu.

Maelezo ya waasisi wa nadharia ya Mwitikio wa msomaji, yanazingatia kuwa msomaji wa matini huwa na picha fulani kutokana na matendo hisia na mawazo yanayoelezewa na msomaji. Matendo ya Sembuli ya kumrushia mama mzazi vitu, kummwagia

mchanga, kumtusi na kumgongea mlango kunaleta picha ya utukutu ndani ya Sembuli. Anachoreka akilini mwa msomaji kama mtoto asiye na adabu na asiye heshimu mzazi wake. Vile vile anaonekana kua mwingi wa hasira na mtu anapokasirika na kuwaza kama mwanadamu. Tabia zake zilikuwa za unyama na wala si za ubinadamu.

Maoni ya Fish (1972) ni kuwa msomaji wa matini aelewe kuwa masuala ya kijamii na kiutamaduni ni muhimu kuzingatia wakati wa usomaji na uchambuzi wa matini za kifasihi. Suala la nidhamu ni muhimu katika jamii. Mtoto asiye na nidhamu ni mtoto ambaye hawezi kuheshimiwa na ambaye huchukuliwa kuwa mwenye tabia pinzani. Mtoto kumtusi mamake, kumlazimisha mamake kumpikia mayai matatu na kumpikia saa nane za usiku akija amelewa ni masuala ambayo hayaruhusiwa na jamii. Kwa mfano alipokanywa kuvunja mlango alimfokea mama na kusema,

> "Nitavunja, nitavunja, nitavunja……." alikazana sembuli. Alikuwa kama mbwa mkali aliyebweka" *Atamlilia nani?* 2009: 1-3

Sembuli aliuendeleza ukatili wake kwa kumfanyia mamake ufedhuli wa hali ya juu. Alimfyatukia kwa kusema,

> "Sili sili siliiiiii! huku akiparaganya vyombo vilivyopangwa pale juu ya meza kwa ajili ya kifungua kinyua, mikate siagi, jamu, corn flakes, maziwa kwenye jagi, matunda na lile yai moja la kukaanga. Vyote vilitapakaa kote chini. Sahani, vikombe, na visahani vyake vikavunjika vunjika". *Atamlilia nani?* 2009:1-3

Vitendo hivi vyovu vya Sembuli vilitokana na msukumo uliotokana na matumizi ya dawa za kulevya. Kama anavyosema Fish (1972) kuhusu masuala ya kijamii ya zingatiwe, ni muhimu kwa sababu vitendo vya Sembuli viliweza kuusababisha uhasama baina ya Sembuli na wazazi wake na jamii kwa ujumla. Uhasama katika jamii hutishia uhusiano mwema miongoni mwa wanajamii watachukiana na kukosa kuelewana. Amani itatishiwa katika jamii husika. Kuchukiana kunatishia amani na uhusiano mwema katika jamii, kutokuwa na utagusano mwema miongoni mwa wa wanajamii. Msomaji anapata picha ya jamii isiyo na umoja na ambayo inaweza kuwa na vita kwa sababu ya uhasama.

Mwandishi alisema kuwa aliwapiga paka na mbwa wa watu bure bilashi, aliwaiba kuku na mabata wa majirani na kuwachoma na kuwala. Alipoulizwa aliwatishia wenye kuku na mabata. Sembuli aliwapiga na kuwachekelea vilema bila huruma wala sababu. Sembuli aliyaharibu mali ya maskini bila sababu. Akawa mbakaji wa wake na mabinti ya watu. Vitendo vya ukatili kama wa Sembuli vilileta ukosefu wa amani katika jamii na kuleta hofu. Wanajamii hawawezi kuishi kwa amani wakiwa na hofu ya kunajisiwa, kuibiwa, kutishiwa maisha yao na hata kuharibiwa maisha yao bila sababu. Uhasama ukinawili katika jamii utakuwa na migawanyiko na kutishia umoja wa jamii. Jambo lolote ambalo ni tisho kwa jamii lazima lipigwe vita na kila mwanajamii. Maelezo ya mwandishi yalimchorea msomaji picha ya vile Sembuli alikuwa mkatili.

Msomaji baada ya kusoma matini huwa na maoni fulani kuhusu matini husika kama wanavyosema waasisi wa nadharia ya Mwitikio wa Msomaji. Picha inayojitokeza kutokana na maelezo ya mwandishi wa Mohamed ni kuwa Sembuli alikuwa katili, mwizi, mwizi wa kimabavu, mfitini, mbakaji na mtu asiye na huruma hata kidogo. Msomaji huwa na hisia ya Sembuli kuwa mtoto hatari katika jamii. Picha ya Sembuli inajitokeza ni kuwa tisho katika jamii. Wanajamii hawawezi kuishi kwa amani wanapohofia kushambuliwa, kuibiwa na kuharibiwa vitu vyao. Mabinti na wake wa watu hawakuwa na amani kwa kuhofia kubakwa.

Mpesha (1996), alisema yale yanayozungumziwa katika matini teule ni hali halisi ya yale yanayopatikana katika jamii halisi. Ajizi ni mfano mzuri wa kudhirhirisha wazo lake Mpesha. Picha ya upotovu wa maisha ya Ajizi ulichorwa kuwa kwanza alianza kama mtoto mtiifu na mwenye bidii masomoni na hata kuongoza darasani. Nyota ya Ajizi iliyong'aa angani, alianza kuzimika pindi tu alipojiunga na kundi potovu la akina Manywele, Makorokoro Matembo na Matindija waliomwangamiza kwa kumfanya avute bangi, safari ya maangamizi ya Ajizi ikaanza. Ajizi akiwa ana buruta mkia darasani na kufurahia sana. Hakuna mtoto mwenye akili timamu aliyeweza kufurahia kuburura mkia masomoni. Maisha ya watoto wengi yameathiriwa katika jamii na kwa sababu ya mihadarati. Kuna watoto ambao wameathiriwa na kulemewa na masomo na maisha baada ya kuzuzuka. Wengine huwa hawajielewi na hata wazazi wao hawawajui vizuri ni nini hasa inawafanya kuzuzuka. Wengine husema ni uchawi.

Watoto wengi katika jamii halisi wameathiriwa na dawa za kulevya mpaka wakawa wajeuri, wababakaji, wezi, wenye matusi, wafitini na wengine kuzubaa na kuzuzuka kwa matumizi ya mihadarati. Wengine uhishia kufa kama Ajizi. Watoto kama hawa huwa ni changamoto kwa wazazi, walimu na jamii kwa jumla, walinda usalama na viongozi. Wanapokuwa wezi, wababakaji miongoni mwa mengine huwa ni tisho kwa usalama wa kijamii. Kama vile Ajizi alivyokuwa tisho kwa jamii, wakaungana kumtafuta, wamkamate hivyo ndivyo jamii halisi na husika inapaswa kuungana na kuwasaka watumizi wa dawa za kulevya pamoja na walanguzi na kuwachukulia hatua zifaazo ili waache ulanguzi huo wa dawa za kulevya. Maoni ya Mpesha (1996) ni ya kweli kuwa yaliyoandikwa kwenye matini ni kioo cha yale yanayotendeka katika jamii halisi. Makundi ya watoto kama vile Ajizi, Matembo, Makorokoro, Manywele na Matindija ni mifano ya makundi ya watumiaji wa mihadarati katika jamii halisi. Watoto wanaonekana mitaani wakiwa mazuzu wengi wamekuwa hivyo kwa sababu ya matumizi ya dawa za kulevya. Viongozi wakiwa wa kidini na wakisiasa wanapaswa kuchukua hatua madhubuti za kujaribu kuwanusuru watoto na makundi ya watoto wanaozidi kuongezeka katika jamii halisi. Wengi wao hujingiza katika uraibu bila kujua. Kama wanajamii na polisi watakuwa wangalifu wataweza kuwanasa watumiaji wa mihadarati na kupunguza utumiaji watumiaji wa mihadarati.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa maelezo ya mwandishi humchorea msomaji picha kamili inayomfanya msomaji kuielewa matini barabara. Kwa kuzingatia maelezo ya mwandishi, matumizi ya tashbihi na istiari humfanya msomaji kuwa na picha akilini mwake. Hisia fulani zinamjia kuhusu vitendo vya wahusika, chanzo cha vitendo hivyo na athari za vitendo vya wahusika. Msomaji anaweza kufahamu lengo la mwandishi. Kwa mfano, katika matini teule, picha za watoto wahusika zinajitokeza. Umaskini wa Musa unampelekea kuwa na huzuni, mwenye hana raha na mwingi wa msongo wa mawazo na mwenye haya. Hali ya Musa ilimpelekea kuanza kutumia na kuuza mihadarati iliyomwangamiza. Sembuli kwa kutumia mihadarati akawa katili, mbakaji mwizi, mchokozi na mharibifu wa vitu vya vilema na maskini akalaaniwa. Maisha yake yakaharibika. Ajizi alizorota masomoni akatoroka nyumbani akapagawa na kufa. Msomaji huwa na hisia na picha zinazomsaidia kutafakari zaidi kuhusu wahusika, matini na kumulika jamii husika. Msomaji huweza kiutumiamatini kama kioo cha kuichunguza jamii vilivyo na vipasavyo. Hatua atakazo zichukua baadaye huwa ni

muhimu sana. Mhimili wa hisia, picha na mawazo ya msomaji huwa ni muhimu kutiliwa maanani wakati wa usomaji na uchambuzi wa matini.

### 4.6 Taswira za Kimsingi na Kimtindo

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), taswira za kimsingi ni dhana inayotumiwa na waandishi wa matini kuelezea taswira au sitiari inayotawala au kuchukua nafasi kuu katika kazi ya kifasihi. Kwa hivyo hii ni taswira inayochukua nafasi kuu katika matini husika. Kwa mfano matumizi ya methali, masimulizi, tashbihi kulingana na mwandishi.

Mtindo ni mazoea ya lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani na kwa lengo fulani. Leech na Short (19 81:10), Wanaumtindo, Crystal na Davy (1969:9-10) walieleza kuwa mtindo unaweza kuwa ni mazoea ya lugha ya mtu binafasi kama vile matumizi ya methali, jazanda au tashbihi. Lugha mtindo ni upekee wa mwandishi wa kujieleza katika maandishi au mazungumzo. Waandishi wa *Atamlilia nani? Ah! Ajizi* na *Vioja vya Musa* wametumia taswira za kimtindo.

Mtindo wa Kiathari kama anavyoeleza Fish (1972), ni yale yanaopitia akilini mwa msomaji anapoisoma matini na kumwathiri kwa njia moja au nyingine. Msomaji huathirika kwa njia moja au nyingine kuitokana na yale anayosoma katika matini husika. Baada ya kulinganisha yale amesoma na yale yamo katika jamii na humwezesha kuielewa vizuri. Anaelezea kuwa mabadiliko ya kijamii huleta mabadiliko katika mikakati ya kuyashughulikia masuala yanayotokea na kuiathiri jamii. Masuala mtambuko yanayoikumba jamii ni kama vile dawa za kulevya, dhuluma dhidi ya watoto.

Kulingana na Abrahams (1999), jazanda ni istilahi inayorejelea picha za kiakili zinazomjia msomaji akilini anapoisoma matini au shairi. Hata hivyo anasema picha hizi si zile zinazotokana na kuonekana kwa macho. Abrahams (keshatajwa) anasema taswira tajwa zinaweza tokana na maneno yanayoweza kuunda picha fulani. Abrahams keshatajwa ameainisha aina za taswira kama vile taswira za usikivu, mguso, joto/baridi/mnuso/harufu, mwonjo na safari. Aina hizi za taswira ndizo zinapaswa kuchunguzwa iwapo mtafiti ana ichambua matini kwa misingi ya taswira.

Mbatiah (2001) anaeleza jazanda kama kunga ya utunzi ambapo lugha hutumiwa kuisawiri picha fulani kutokana na maelezo yanayotumia maneno teule au tamathali za usemi na mtunzi humwezesha msomaji kuona, kuhisi au hunusa kitu kinachoelezwa, mwandishi huchora picha fulani akilini mwa msomaji kwa kulinganisha sifa za watu, wanyama, au vitu viwili tofauti na maumbile kwa msingi wa sifa fulani iliyopo katika vyote viwili bila kutaja sifa yenyewe. Jazanda huhusisha lugha ya isitiari ambayo hulinganisha sifa za vitu viwili au zaidi pasipo kutumia maneno ya kumithilisha kwa kutumia maneno kama; kama au mithili ya yale yamesimuliwa katika matini ya fasihi ya watoto ni picha kamili ya mambo halisi yanayotendeka katika jamii husika.

Kwa upande wake (Cuddon 2013), taswira inaweza kuwa matumizi ya lugha kuwakilisha vitu, matendo, hisia, mafikira, mawazo, hali ya kiakili na tajriba za kiakili. Anasema taswira inaweza kuwa ishara ya kuonekana kwa macho. Cuddon (keshatajwa) anaiainisha taswira kuwa kama, mnuso, mguso, usikivu, mwonjo, kiakili na safari. Anasema kuwa jazanda, inakuwa na maana za kifasihi kama ilivyotumiwa na waandishi wa matini za kifasihi; jazanda inaweza kuleta maana za kimielekeo au za ki-ishara.

Waandishi wa matini za *Vioja vya Musa*, *Atamlilia nani?* na *Ah! Ajizi* walitumia jazanda kuelezea. matumizi ya dawa za kulevya. Kama anavyosema Mbatiah (2001) kuwa jazanda ni matumizi ya lugha ya kumithilisha sifa ya kitu, au mtu kwa kutumia maneno kama: kama nia mithili ya, waandishi wa matini teule wametumia jazanda. Mogambi, kuelezea umaskini wa Musa uliompelekea kuwa mtumizi na muuzaji wa mihadarati anatumia neno la umithilisho kama kuonyesha jinsi watoto maskini walionekana kukaa kama mayatima, waombaji waliotusiwa na wenzao. Picha ya yatima na uyatima inajichora akilini mwa msomaji.

> “Wanafunzi wenzake Musa walipogundua uchochole wake Musa walimchukia na kumcheka sana hasa alipokunywa chai bila kitafunio kwa kuwa hakuwa na pesa za masrufu. Watoto waliokuwa maskini kama Musa walionekana kama mayatima. Waliishia kuwa ombaomba. Walitusiwa na wenzao. Jambo hili likamkosesha raha mpaka akaanza mpango wake wa siri wa kuuza sigara na mihadarati” *Vioja vya Musa* (2007:3-5).

Kama Musa hakuwa na umaskini angeendeleza ndoto yake ya kusoma kwa bidii na kuwa kiongozi mwadilifu kama alivyokuwa hapo awali. Musa alikuwa ameshauriwa

na wazazi wake na wakubwa wake mpaka wakamwona kwao kama kijana mzuri na mwenye heshima. Kuna watoto wengi wazuri lakini kwa sababu ya matatizo ya umaskini uishia kujiharibia maisha yake ya siku za usoni. Nyota yake iliyokuwa imeng'aa na kumpa matumaini sasa ilikuwa imezimika. Hii iliashiria kuwa maisha yake yalianza kuharibika. Kuna watoto wengi wanaoyapitia yale Musa alipitia. Ni muhimu wazazi, wahisani na walimu wawachunguze watoto ili waweze kuyaelewa yale wanapitia na kuwatafutia suluu matatizo yao ili wasijiingize katika uraibu wa matumizi ya mihadarati. Umaskini na matatizo mengi na huwapelekea watoto wengi kushawishika kuingilia matumizi ya dawa za kulevya.

Musa alielewa kuwa biashara aliyoifanya ya kuuza sigara na bangi ilikuwa haramu. Alikumbuka hata siku ambayo alikuwa karibu kufumaniwa akivuta sigara na kuwauzia wanafunzi wenzake. Musa aliyekuwa mwaminifu alianza kuwa msema uongo. Mabadiliko ya kiakili baada ya kuanza kuzitumia dawa za kulevya yalimbadilisha na kuwa na matatizo ya kukabiliana na hali yake baada ya athari ya dawa za kulevya. Maoni ya Fish (1972) kuwa mabadiliko ya kijamii huleta mabadiliko katika mikakati ya kuyashughulikia. Mojawapo ya mabadiliko haya ni matumizi ya dawa za kulevya. Matumizi ya dawa za kulevya huwa na athari zake na kwa hivyo zinahitaji mikakati ya kuzishughulikia ili kuwanusuru watoto na vijana wanaoendelea kuangamizwa. Matini ya *Vioja vya Musa* inao watoto wanaotumia dawa za kulevya. Uadilifu wa Musa umebadilika na kuwa mwongo, kwa mfano, mwandishi anasema.

> Musa alielewa biashara kama ile haingefanywa mchana. Pia alifahamu kuwa kitendo kile kilikuwa kinyume cha sheria. Kwake lilikuwa lisilobudi hutendwa. Aliitaji pesa za kutumia kuinua hadhi yake miongoni mwa wanafunzi. Musa aliitaji kujikwamua kutokana na fedheha ya umaskini, kuchekwa na kutusiwa na wenzake," *Vioja vya Musa* (207:5-6).

Musa walipofumaniwa wakivuta bangi walichana mbuga kwa kujua kuwa kitendo walichokuwa wakitenda si kizuri na kilikuwa cha kuvunja sheria. Mahitaji ya mtoto kama Musa na wengine katika jamii yakishunghulikiwa hawawezi kujiingiza katika uraibu wa matumizi ya mihadarati. Serikali inapaswa kuwa na mpangilio wa kuwashauri watoto kutoka jamii fukara ili waweze kuelekezwa vizuri jinsi ya kupambana na hali ngumu za kimaisha. Katika kipindi cha ushauri katika jamii,

kanisani au shuleni watafunguka wajielewe. Pamoja na ushauri, mahitaji yao yapaswa kushughulikiwa ipasavyo ili wajiendeleze vizuri masomoni na maishani.

Taswira inaweza kuwa matumizi ya lugha kuwakilisha mawazo. Cuddon (2013). Hii ina maana kuwa mawazo ya mwandishi yanaweza kuwakilisha wazo fulani. Musa mhusika mkuu katika *Vioja vya Musa* amechorwa akiwa katika hali ngumu ya kimawazo alipotoka ofisini mwa mwalimu wa zamu baada yakushitakiwa. Alishtakiwa kutumia na kuuzia wanafunzi sigara na dawa za kulevya. Hai yake ya huzuri, hofu na majuto ilionekana wazi. Hakujua hatima ya shitaka hilo kwa mwalimu wa zamu na hata kwa mwalimu mkuu. Mwandishi anelezea hali ya Musa ya kuchanganyikiwa na hofu aliokuwa nayo. Musa anajutia kitendo cha kuu za mihadarati kilicho sababishwa na hali ya umaskini.

> “Musa alipotoka ofisini kwa hatua ya hesabu akiinamisha kichwa mawazo yakimlemea kwa uzito wake. Akaingia kwenye giza la mawazo. Aliona giza totoro likiwa limeyangubika maisha yake ya usoni. Aliona kuwa mwangaza ambao ulikuwa umeanza kuingia maishani mwake ukiwa umezimwa ghafla. Alijisikitikia na kujikuta akijizungumzia gizani na uzito wa mawazo uliomlemea”.*Vioja vya Musa* 2007:23

Maelezo haya kumhusu Musa yanamfanya kuwa mtoto aliyetumbukia katika lindi la mawazo kwa shida ambazo hakuwa na mbele wala nyuma kujiokoa, sasa ndio alikumbuka kwao kulikokuwa na umaskini mwingi. Picha inayochorwa ni ya mtu mwenye mawazo mazito na mwenye majuto kwa yale aliyoyatenda. Umaskini uliomsababishia Musa ugumu wa maisha, kuchekwa na kudharauliwa na wenzake ndio uliomplekea kuwa muuzaji na mtumizi wa mihadarati. Kujihusisha na mihadarati ndiko kulikomletea masaibu ya kuwa na mawazo mazito moyoni na asijue la kufanya. Alikuwa amenaswa na utandu ambao ulikuwa ni vigumu kujinasua. Suala la ufukara wa familia ya akina Musa ujitokeza katika uzungumzi wake nafsia. Anazungumzia na hali ya moyo wake kuhusu maisha yake na hali ya umaskini iliyomtinga.

> “Lakini ningefanya nini ilhali nilihitaji ngwenje za kununulia mkate na mahitaji mengine. Ningefanyaje ilhali wazazi wangu hawakuwa na uwezo wa kunitimizia mahitaji yangu yote? Ningefanyaje ilhali wanafunzi walikuwa wananicheka? Musa atitaka kuwa kama wanafunzi wengine waliokuwa wakinunua mkate kila asubuhi.

> Uchechefu wa hela ulimkweza akabuni mbinu ya kuwauzia wengine sigara kama njia ya kujipatia pesa”. *Vioja vya Musa* 2007:25-26.

Maelezo ya Abrahams (1999) kuwa ‘Jazanda ni picha za kiakili zinazomjia msomaji akilini anapoisoma matini yathihirika bayana katika maneno ya Musa. Maswali anayojiuliza msomaji mwenyewe akilini ya msomaji uchora ukata wa familia ya Musa unaompelekea kukosa pesa za masrufu za kununulia mkate na mahitaji mengine. Masaibu aliyoyapitia ndiyo yaliyompeleka kuuza sigara na bangi. Watoto wengi wanapitia masaibu kama haya yanayopaswa kushughulikiwa. Mwandishi alilinganisha maisha yake ya ufukara na ya wanafunzi wenzake waliokuwa wametoka katika familia ambazo si maskini. Picha ya Musa inayochorwa akilini mwa msomaji na mwandishi ni kuwa ni mtoto mwenye mazoea ya kuvuta sigara na bangi. Mwandishi alichora hali ilivyokuwa pale kwenye kituo cha kurekebisha tabia. Mwandishi anaeleza jinsi alivyokuwa na hamu ya kuvuta bangi na sigara kama alivyokuwa amezoea. Yeye ni mgeni kwenye kituo cha kurekebisha tabia. Hajui haitoe bangi na sigara wapi? Mwandishi anamlinganisha na jogoo wa shamba kuonyesha hali yake ya kuchanganyikiwa na kutojua afanye nini aipate sigara na bangi.

> ‘Musa alikuwa amechoka tiki. Alikuwa ameingiwa ha hamu ya kuvuta sigare na bangi kama ilivyokuwa kawaida yake kabla ya kulala. Pale alikuwa kama jogoo wa shamba ambaye hangewika mjini. Hakujua jinsi angevipata vitu hivi katika mazingira haya mpya ili kujiliwaza kwa uraibu wa mihadarati. *Vioja vya Musa* 2007 :25-27.

Kama anavyosema Cuddon (2013), kuwa taswira inaweza kuwa matumizi ya lugha kuwakilisha hisia ni kweli kulingana na hali ya Musa katika kituo cha kurekebishia tabia. Musa ana hamu kuu ya kuvuta sigara na bangi. Hakujua kuwa kule alipopelekwa kungepatikana bangi. Musa alishangaa kuona bangi ikivutwa pale na tena kwa wingi sana. Watoto wanaoivuta wana mawazo na dhana potovu kuwa bangi hurahisisha maisha na kumwezesha mtoto kufaulu maishani. Dhana na mawazo kama hayo kuhusu bangi ni hatari maishani mwa mtoto. Dhana kama hiyo huchangia pakubwa kumpotosha mtoto, kwa hivyo wanapaswa kuelekezwa na kushauriwa vizuri kuhepukana na mitego miovu kama hii. Mtoto wengi wa wamehadaiwa na wenzao pamija na kwa kuonyesha umuhimu na manufaa ya kuvuta bangi. Wengi huingia pasi na kujua hatari ya uraibu wa bangi. Mawazo potovu yanampelekea Musa kusema.

> “Moshi wa bangi hunirahisisha maisha na kunivunjia milima mingi ambayo nimeshaipanda. Musa akasema, mwenzake akasema, kama ni hivyo, basi maisha yako yatakuwa rahisi humu. “*Vioja vya Musa* 2007: 47

Mawazo kama hayo ni hatari sana kwa watoto wasiojua hatari iliyoko ya kujiingiza katika uraibu wa matumizi ya mihadarati. Wengi huyaharibu maisha yao na hatimaye kuwa ovyo tu. Musa alipotoka kifungoni alikuwa ameharibiwa kabisa na bangi. Alipopewa wosia na mamake kurudi shuleni alikataa kata kata. Hali yake ya kiakili kama anavyosema Cuddon (2013) ilikuwa imeathirika. Alikuwa pale kama mfano wa mtu. Musa mwenyewe Aliuona ulimwengu ukiwa ombwe tupu na kila kitu kikimwendea upogo. Alijiunga na kundi la vijana wa kupiga mtindi kwa pesa alizozipata kutokana na kazi yake ya uhamali. Mwishowe akakamatwa kwa wizi. Alikuwa amekimbia mpaka jasho lilimtoka na kumtiririka kama maji. Kweli mbio za sakafuni huishia ukingoni. Hivi ndivyo watoto wengi hujiangamiza wanapotumia mihadarati. Mwandishi ameichora picha ya mwili wa Musa ulivyo roa jasho ilivyomtiririka baada ya kufumaniwa wakiiba nyanya. Walikimbizanwa nao na polisi mpaka walipokamatwa na polisi.

Mtaalam Wamitila (2003) anaeleza kuwa taswira inaweza kuwa matumizi ya lugha kuwakilisha matendo ya mtu au kitu. Katika matini ya *Atamlilia nani?* Matendo ya Sembuli yalitumika kuchora picha ya mtu mwenye hamaki kuu katili, mfitini, asiye na heshima na mwizi. Kila alipotaka kuonyesha hasira zake aliugonga mlango kwa nguvu zake na aghalabu kumfokea mamake. Kitendo cha kumfokea mamake, kumtendea mama Sembuli kama mtoto asiye na nidhamu, mkatili na mwenye hasira za mkizi.

> “Nitauvunja, nitauvunja, nitauvunja. Alikazana Sembuli akiwa kama mbwa anayebweka.” *Atamlilia nani?* 2009:1

Sembuli aliyatenda haya kwa msukumo wa kiakili uliotokana na matumizi ya mihadarati. Watoto wengi huvitenda vitendo vyenye kishindo mbele ya wazazi wao au hata mbele ya wanafunzi wenzao na walimu na wasijue kama vitendo wanavyovitenda ni athari za matumizi ya dawa za kulevya. Wakati mwingine huchukuliwa kuwa ameharibikiwa na akili au hata amerogwa. Ukweli ni kuwa wengine huwa wameathirika kiasi cha kutojua hata anafanya nini. Mwandishi alisema, anaeleza kuwa

kuna msukumo fulani uliomsukuma Sembuli kutenda maovu aliyoyatenda. Sembuli alikuwa na mawazo akili ni yaliyomsukuma Sembuli kuwadhulumu watu na wanyama.

> "Sembuli alipokwishatoka nje, alisimama mbele ya mlango kwa muda huku akipima athari ya matendo yake. Yeye binafsi alijua kwamba matendo yake yale yalikuwa ya kipuuzi. Lakini hata hakujua kwa nini hakuweza kujizuia. Alisikia sauti tu kichwani mwake iliyomwambia afanye vitendo vyenye kukera. Hakuweza kabisa kuizuia sauti hiyo. Kusema kweli wakati mwingine alijuta kufanya hivyo! *Atamlilia nani?* 2009:1

Ni muhimu wazazi, walimu na washikadau wote wanaohusika na utunzi wa watoto kuwa makini na matendo ya watoto na wakati wanapobadilika na kuwa na matendo mabaya. Wanapaswa kushauriwa vilivyo ili waache matendo mabaya. Wakiathiriwa na mihadarati wataharibika zaidi. Mienendo ya watoto pamoja na vitendo vyao vinapaswa kuchunguzwa mara kwa mara kuonyesha yanaambatana na maadili mema.

Matendo ya Sembuli yanachora picha ya mtoto asiye na nidhamu mchokozi mwizi na mkora aliyepotoka kabisa. Mawazo hayo yanapatikana akilini baada ya kusoma matini kwa mujibu wa nadharia ya Mwitikio wa Msomaji. Mhimili wa hisia au mawazo yanayounda picha fulani akilini. Tunamwelewa Sembuli kutokana na vitendo vinavyojidhirisha katika masimulizi ya mwandishi. Alipenda kuwachokoza, kuwakejeli, kuwacheka walemavu, vichaa na maskini Sembuli alilaaniwa kwa kuambiwa kuwa anayecheka kilema, hafi hadi kimfike. Matendo maovu ya watoto yanaweza kuwaletea laana kama Sembuli. Kwanza alilemazwa na vijana barobaro kwa kuwachokoza katika mkahawa wa Hollywood. Hatimaye risasi ya babake ikamlemaza kabisa. Sembuli alikuwa amewachosha watu kwa kuwaibia kuku na bata, kuwabaka wake na mabinti wa watu na kuwaharibia watu vitu vyao. Katika jamii halisi kuna watoto na vijana wengi wanaohusika kwa mambo ya wizi na uharibifu mwingine kama huu kutokana na matumizi ya mihadarati.

Ajizi katika matini ya *Ah! Ajizi*, mwandishi anaeleza kuwa alipoanza matumizi ya mihadarati akili yake iliharibika. Mawazo mahututi yalimtinga na kumsokota akilini. Mkururo wa fikra mithili ya siafu msafarani ulimsumbua asijue la kufanya. Aligeuka na kuwa mkatili sana. Taswira iliyochorwa ma mwandishi ni ya hali ya kiakili (Cuddon

(2013) anayelezea kuwa taswira inaweza kuwa matumizi ya lugha kuwakilisha hali ya kiakili. Akili ya Ajizi ilikuwa imeharibiwa na marafiki zake Manywele, Makorokoro, Matembo na Matindija waliouma uzi kuhakikisha kuwa wamemwangamiza na kumzuzua asiendelee na masomo yake. Ajizi alikuwa na mawazo mengi yanayo linganishwashwa na siafu msafarani. Haya yalimpeleka mbele na nyuma. Bangi iilizindisha masaibu yake. Picha ya uenda wazimu inajitokeza. Pale Ajizi alianza kukimbia na kucheka ovyo ovyo, kutembea na soksi moja na kupiga ukungu. Bila sababu. Mwandishi alieleza

> "Walianza kumfunza na kumwelekeza kwenye tabia zao mbaya katika bangwa waliloita, 'Njoo tuvute," katika mtaa wa kutajika na hodari waliuvua utu na kuuvalia uhayawani. Wote kwa pamoja walizama kwenye bahari ya uvutaji bangi, sigara na hata gudi. Ajizi alikuwa amepagawa na kuwa wazimu. Akawa anazitoa kungu na kamsa za mchana. Akawa mchafu mchafu. Akawa anavalia soksi moja kwenye mguu wa shamli na kiatu kimoja kwenye mguu wa yamini, akawa wa kujizungumzia na kuicheka nafsi yake. *Ah! Ajizi* (2015:14-20)

Ajizi waliishi msituni kwa mihadarati huku wakiwa na mazoea ya uwazimu na udhoofikaji wa afya. Ajizi aliyatenda matendo ya ajabu ajabu kama kuusalimia upepo! Kuangua kicheko ovyoovyo. Watoto na vijana wengi katika jamii halisi huwa wanapagawa hutokana na kuingizwa katika uraibu wa mihadarati wenye nia mbaya ili kuwaharibia maisha yao bila kujua. Watoto wanapaswa kupewa wosia wa kutosha kuwachunguza rafiki zao na kuepukana na rafiki wabaya wanaowashirikisha katika matumizi ya mihadarati. Washika dau wote wanaohusiana na utunzi wa watoto wawe waangalifu katika kuchunguza mabadiliko ya tabia na mienendo ya watoto. Ni muhimu mara kwa mara kuzichunguza tabia za watoto ili kuwaelekeza vilivyo.

### 4.7 Taswira za Mnuso

Taswira za mnuso urejelea harufu fulani au maelezo yannnayomfanya msomaji kuwa na hisi ya aina fulani ya harufu. Abrahams (1999) ameainisha aina za taswira na kusema kuwa kuna taswira za mnuso au harufu. Harufu hii inaweza kuwa ni ya chakula au kitu fulani. Harufu inayorejelewa inaweza kuwa ni nzuri yaani ya kunukia au harufu mbaya au ya kunuka. Harufu ya kunuka uhusishwa na vitu vilivyooza au kuharibika. Harufu ya kunukua inahusishwa na harufu ya kupendeza.

Wamitila (2003) vilevile ameianisha aina za taswira na kutaja kuwa kuna taswira ya mnuso. Mnuso ni harufu fulani kutokana na kitu fulani au chakula fulani. Maelezo kuhusu harufu fulani kunaweza leta taswira ya mnuso. Mwandishi anaweza elezea kuhusu kilichopikwa vizuri na kunukia vizuri haswa kinacho kaangwa na kutoa harufu ya kuvutia. Marashi vilevile huwa na harufu ya kupendeza. Harufu ya kitu kiovu haifurahishi.

Mtaalamu Abrahams (1999), ameainisha aina za taswira kama vile usikivu, mguso, joto/baridi, mnuso au harufu, taswira za mwonjo na safari. Wataalam hawa wote wanakubaliana kuwa kuna taswira ya mnuso au harufu. Taswira za mnuso kulingana na wataalam hawa ni taswira ambazo humletea msomaji picha zinazohusiana na harufu. Maelezo yaliyopatikana yanazua picha ambazo zinalenga hisia za msomaji za kunusa. Taswira za mnuso zimejitokeza katika matini teule za *Atamlilia nani? Vioja vya Musa* na *Ah! Ajizi*. Mwandishi wa *Atamlilia nani?*! Alieleza,

> “Vitendo vilivyotendwa na Sembuli na vilivyodhihirisha matumizi ya taswira za mnuso, baada ya Sembuli kuwa mraibu wa dawa za kulevya. “Sembuli alikuwa mkatili kiasi cha kuwa, Mbwa, Paka, Kunguru na hata binadamu walihisi kutishiwa tu walipoinusa harufu ya Sembuli. Walimkimbia, wengine wakipaa juu zaidi. “*Atamlilia nani?* 2009:5.

Sembuli alikuwa tisho kama walivyo vijana wengi katika jamii halisi ambao kutokana na uraibu wa mihadarati. Wanaogopewa na wanajamii kama alivyoogopewa Sembuli kiasi cha kuwa yeyote au chochote kilichonusa harafu yake alijiona hatarini na kujitahidi kujinasua au kujiepusha na janga la mauti. Waraibu wengine wa mihadarati huwa ni tisho kwa jamii. Walinda usalama wanapaswa kuwa waangalifu na kuchunguza matendo ya watoto hawa ili waweze kukamatwa wasije wakaendelea kuwatishia jamii katika harakati zao za kila siku.

Kama anavyosema Wamitila (2003) kuwa taswira ya mnuso umwelekeza msomaji kupata harufu ya kitu kinachozungumziwa, Sembuli alilazimika kuwafuata wenzake waliomtoroka alipoishiwa na fedha akiwaombaomba fedha au mihadarati. Uraibu wa dawa hizi kulimlazimu kuwafuata angalau ainuse ile harufu ya ‘Unga! Kama asingeinusa ile unga basi angejitafutia maangamizi. Watoto wengi hujiingiza kwa

uraibu huu wa mihadarati bila kujua hatari yake na huja kujuta baadaye, watoto washauriwe na kuonyeshwa mifano ya walioathirika na dawa za kulevya ili wajionee wenyewe. Hisia ya harufu fulani humfanya msomaji kuwa na picha ya kitu kinachohusishwa na harufu hiyo. Msomaji huwa na mawazo fulani kuhusu kile kinachohusishwa na harufu hiyo na kukiwazia zaidi jambo linalomfanya msomaji kuelewa zaidi.

Mhusika Musa katika Matini ya *Vioja vya Musa* aliendeleza maoni ya Abrahams (1999) kuwa taswira ya mnuso inaweza kuwa maelezo yanayoashiria harufu fulani. Musa shabiki wa timu ya kandanda ya Chui alisema,

> "Nani asiyefahamu kuwa mashabiki wa Simba ni wazusha vurugu na wenye midomo michafu? "*Vioja vya Musa* 2015:28

Maneno ya Musa yaliashiria midomo michafu kuwa ni midomo inayotoa harufu mbaya au inanuka. Hii pia ni lugha ya mabezo au dharau inayotumia maneno yanayovunja heshima au kuleta aibu. Musa kwa kuathiriwa na dawa za kulevya asingeweza kuuteua msamiati wa tasfida. Taswira hii ya mnuso humwezesha msomaji kuelewa zaidi ya le yanayozungumziwa anapolinganisha harufu inayozungumziwa na ile msomaji aliyoifahamu.

Maoni ya wataalam hawa Wamtitila (2003) Abraham (1999) na Cuddon (2013) yaliendelezwa na mwandishi kwa kuelezea jinsi vita vilichacha ugani Kaachonjo baina ya mashabiki wa Chui na wale wa Simba. Mwandishi alieleza jinsi vita vilipiganwa mpaka ikabidi vikosi vya polisi vile kutenganisha wapiganaji vita vili chacha mpaka damu yao ikazagaza harufu kila mahali. Hivi vilikuwa vikali. Picha ya majeruhi inajengeka akilini mwa msomaji. Hali ya vita inajitokeza akilini mwa msomahi Mwandishi alisimulia.

> 'Askari walijaribu kuzima vita vile ikawa ni bure bilashi. Ngozi ziliwachibuka wachezaji. Polisi waliongezewa kikosi kingine king'ang'a ne kutuliza vita. Vita vilivyoletwa na athari za dawa za kulevya na kuwafanya kutotafakari. Baada ya nusu saa uga wa Kaachonjo ulibaki tupu tena. Damu ya watu ilinuka kila mahali mle ugani. *Vioja vya Musa* 2015:34.

Watu kupigwa mpaka damu ya watu ikanuka kila mahali, havikuwa vita vya mchezo. Vita hivyo vilileta na watoto walioshiriki mihadarati. Athari za mihadarati hazingekuwepo watoto wangechukua muda wa kuyatafakari yale yangewasababishia watu mbele ya polisi. Hawangeona madhara ambayo wangejisabibishia wenyewe. Walipelekea watu wasio na hatia kuchapwa na kujeruhiwa. Vita vingi tunavyoshuhudia nyugani nyingi wakati wa michuano ya kandanda huenda vinatokana na athari za matumizi ya dawa za kulevya. Maafisa wa polisi wanapaswa kuwa macho kupambana na watoto au vijana wanaotaka kuzusha vurugu ugani.

Taswira ya mnuso kama anavyoelezea Cuddon (2013) ni maelezo yanaayotumia lugha kuelezea harufu au mnuso wa kitu. Ajizi hapo awali kabla ya matumizi ya dawa za kulevya alikuwa msafi kimwili na kimavazi. "Lakini aligeuka akawa bebeeru. Alinuka na kutoa fei! alinuka fondogoo. Ajizi akasahau umuhimu wa usafi. Hakupata nafasi ya kuoga hasa alipopagawa na akili. Watoto wengi haswa vijana waonekana katika jamii wakiwa wachafu na kunuka uchafu ni ishara tosha kwamba huenda wameathiriwa na dawa za kulevya na hawaoni maana ya kuoga. Ni aibu mtoto aliyokuwa anang'ara kama balamwezi sasa ndiye anayenuka kama beberu. Ni aibu kusema alinuka Fondogoo. Wengine wakiathiriwa na dawa za kulevya hawa kogi au kuwa watanashati. Uvundo wao unamithilishwa na wa beberu.

## 4.8 Taswira za Mwonjo

Kulingana na Wamitila (2003), taswira ya mwonjo ni taswira ambayo hulenga kwenye hisia ya kuonja, au kwenye maelezo yanayohusiana na chakula. Wamitilia (keshatajwa) anaeleza kuwa ladha ya chakula au kinachoonjwa pia huwa katika akili ya yule anayeonja. Ladha ya kitu kinachoonjwa kama mwonjaji aliwahi kukionja tena huwa akilini mwake. Mawazo haya yalioana na Cuddon (2013) anayesema kuwa taswira inaweza kuwa matumizi ya lugha kuwakilisha hali ya kiakili. Mwonjaji huwa na hali ya kiakili ya ladha ya kile anakusudia kuonja. Kama hana basi huwa na ladha hiyo akilini baada ya kuonja. Ladha yake inaweza kuwa tamu au chungu.

Maelezo ya mwandishi wa *Atamlilia nani?* alieleza taswira ya mwonjo anapotoa maelezo ya chakula Sembuli alichotaka na alichopikiwa. Sembuli kutaka kupikiwa mayai matatu ya kukaanga kama alivyozoea. Mamake alimkataza kwa sababu za

kiafya. Sembuli kwa hasira aliviparanganya vyombo vilivyopangwa juu ya meza kwa ajili ya kifunua kinywa. Mikate, siagi, jamu, cornflakes, maziwa kwenye jagi, matunda na lile yai la kukaanga vyote vikatapakaa chini, maelezo ya mwandishi kuhusu chakula kilichoandaliwa mezani kina chora taswira ya mwonjo. Vyakula hivyo vikitajwa huamsha hisia za mwonjo akilini na ladha yake humjia msomaji au mwonjagi akilini. Huwa na hali ya kiakili kama alivyosema Cuddon (2013) hali ya kiakili huunda taswira ya mwonjo akilini.

Sembuli alipolemazwa na kundi la vijana kati ya Klabu cha Hollywood alitemwa nje na kundi la Ungangster. Hakuweza kuwa na fedha za masrufu za kununulia bangi kutimiza uraibu wa kuvuta bangi. Aliwafuata marafiki zake angalau ainuse au aweze kuionja unga *Atamlilia nani?* 2009:28. Ni muhimu wanaotaka kuwa katika uraibu wa mihadarati waelewe kuwa watakapo kosa pesa za kununua dawa za kulevya na watakuwa wanakikemulia kifo macho. Wanaweza kuangamizwa au kujiangamiza au kutenda vitendo vya kuvunja sheira mradi wapate fedha za kununua ‘unga’ kama walivyouita. Neno ‘Unga’ kama linavyotumiwa na mwandishi linaleta picha fulani akilini mwa msomaji kama wanavyosema waasisi wa nadharia ya Mwitikio wa Msomaji. Msomaji anajua unga ya kawaida anapoona neno unga. Picha ya ile ‘Unga’ huja akilini mwake. Anatafakari kuhusu unga ya pili na kulinganisha unga mbili zinazorejelewa.

Brunner (2003) anaelezea kuwa hadithi ya Kifasihi huelezea matukio katika jamii na kuonyesha mambo yanayokusudiwa katika jamii. Hadithi hutoa onyo kwa wanajamii. Mhusika Musa katika *Vioja vya Musa* alipofungwa katika kituo cha kurekebisha tabia maisha yalikuwa magumu pale. Starehe alizozizoea pale nyumbani kwao. Chakula na uji vilikuwa vibovu sana na hakikulika. Chakula hakikuonjeka hadi akapoteza hamu, Wenzake waliozoea pale gerezani walikuwa wamepazoea na hali yao ya kiakili ikayakubali maisha magumu ili maisha yaendelee. Chakula kinachozungumziwa na mwandishi ni kibaya. Hakikupikwa vizuri. Hakikuwa na ladha ya kupendeza. Picha ya uji mbaya na chakula kibaya inajengeka akilini mwa msomaji.

Hisia na hali ya kiakili ilielezea kutoa onyo kuwa mle gerezani hamna raha kama Cuddon (2013) anavyoelezea kuhusu hali ya kiakili na hisia za mtu kuhusu jambo

fulani. Akili ya Musa ilivurugika kabisa. Musa hakuvutiwa na kile chakula. Hisia zinazomjia msomaji ni kuwa alikichukia chakula kile pamoja na uji. Mazingira ya kufungwa ndiyo yalimpelekea kukila tu ili kuokoa maisha yake. Alishangaa na kubung'aa kwa hali ya jera pale aliposema,

> "Nilistajabu ya Musa, lakini haya ni ya Firauni. Jamaa wanakisifu chakula ambacho hakiliki" *Vioja vya Musa* 2007:44

Uji haukuwa na ladha na haukunyweka. Musa alionekana kujuta yamkini ndivyo mambo ya hapa yalivyo! Huu ni mfano wa uji kwani umejaa matuna haunyweki. Haidhuru, lisilo budi hutendwa. Naona wengine wamejizoea na wanaupenda! Musa hakunywa uji ule kwa kuupenda. Aliunywa shingo upande. Picha ya kutoupenda inatokana na maneno yake Musa, kuwa lisilobudi hutendwa. Tutaunya uji mwenyewe hivyo tu. Kwa ukosefu wa lingine la kutenda ndipo alikubali kuunywa tu.

**4.9 Taswira ya Kiishara**

Kulingana na Wamitila (2003), hizi ni taswira ambazo hujengwa katika akili ya msomaji kutokana na uteuzi wa lugha ya mwandishi. Taswira za kiishara zina jumbe za ziada, yaani picha zinazoundwa zinaashiria kitu fulani. Kimsingi tunaweza kusema hizi ni taswira ambazo hufanya kazi kama ishara. Sembuli katika *Atamlilia nani?* kuugongesha mlango kwa nguvu zake zote, kumfokea mamake na kumfanyia vitimbi mamake ni ishara ya mtoto asiye na nidhamu na mwenye hamaki ya hali ya juu. Haya aliyatenda kwa sababu ya hali yake ya kiakili kama anavyosema. Hali yake ya kiakili ilikuwa imeharibiwa na mihadarati na kudekezwa kupita kiasi na babake. Bi. Boswire anamwogopa bwanake asije kumchapa.Bi. Bosire alilalamika lakini kichinichini.

> "Bwana Bosire ameshaharibu mtoto huyu alilalamika chinichini Bi Bosire, kwani hakuweza kumwambia mumewe waziwazi kuchelea fujo zake. *Atamlilia nani?* 2009:9

Huko kulalama kwa Bi. Bosire chinichini ni ishara tosha kwamba ni mwoga. Alimwogopa bwanake sana. Hali ya Bi. Bosire ya woga ilitokana na vitimbi, alivyofanyiwa na mumewe. Bi. Bosire anaona Bwana Bosire amemdekeza Sembuli kupita kiasi na fedha anazompa zikamfanya kuwa na uraibu wa mihadarati. Bi. Bosire alikuwa ametamaushwa na kutiwa woga na vitimbi vya Bwana Bosire na mwanawe

Sembuli. Aliona kuwa Sembuli hangerekebishwa kwani alikuwa sikio la kufa babake alimharibu kwa kumdekeza. Bi, Bosire aliona kilichobaki ni Sembuli kufunzwa na ulimwengu. Alisema,

> "Ninaingoja siku ambayo nitauona mwili wa Sembuli umenyooka chini." *Atamlilia nani?* 2009:22

Maneno ya Bi. Bosire yalitokana na kuwa Bwana Bosire hakuwa tayari kumrekebisha mwanawe na mkewe aliashiria kuwa waliingoja kuona masaibu ambayo yatamkumba mwanawe. Hatimaye Sembuli aliishia kulemazwa na kichapo cha vijana mpaka mamake akalia sana. Sembuli alipopona alipanga kumwibia babake laki nane. Usiku huo alipotoka benki babake alikuwa macho. Sembuli alipojaribu kumwibia babake pesa alipigwa risasi ikamlemaza.

Hali ya Musa shuleni ni ishara tosha kuwa nyumbani kulikuwa na ufukara wa hali ya juu. Mwandishi ametumia maneno kuelezea hali ya umaskini wa Musa. Hali ya mtu inaweza elezewa kwa lugha ya maneno. Shuleni Musa aliishi maisha ya upweke, hakuwa na pesa za kununulia vitafunio kama wanafunzi wengine wakati wa chai, shuleni vile vile aliishi maisha ya kuombaomba. Umaskini huo ukaathiri hali ya kiakili ya Musa. Hali hii ya kiakili ya Musa, ilimfanya kuwa na upweke sana akawa hata anaota ndoto za mchana. Hatimaye akawa muuzaji na mraibu wa mihadarati.

Musa alipokamatwa kwa kuzusha fujo ugani Kaachonjo, na kupelekwa shuleni kwa gari la polisi, alishukishwa akiwa na matongo machoni huku ulenda ukiwa unamtoka kinywani. Hii ilikuwa ishara tosha kuwa hakuwa amenawa uso asubuhi ile. Ilikuwa ishara tosha hakuwa amelala nyumbani. Kama angekuwa amelala nyumbani angekuwa ameoga. Katika kituo cha kurekebishia tabia hali ilikuwa kinyume na alivyotarajiwa. Bangi ilivutwa kama kawaida. Ishara zilitumika badala ya maneno na matendo. Mwandishi wa *Vioja vya Musa* anasema,

> "Mazungumzo pale chumbani ya kabaki ya kunong'onezena tu muda ulivyozidi kusonga mbele. Hawakuthubutu kunyanyua sauti zao juu kwani walihofu kujulikana kwa shughuli zao. *Atamlilia nani?* 2007:47

Hii ilikuwa ishara kuwa shughuli ile ya uvutaji bangi iliendeshwa kisiri, kilikuwa kinaya kuona watoto waliopelekwa gerezani kurekebisha tabia na kuacha uraibu wa bangi wakiendelea kuvuta bangi hata zaidi. Utepetevu wa polisi wanaolinda magereza na vituao vya kurekebishia tabia ndio unaopelekea bangi kuwafikia wavulana. Kama wangekuwa wangalifu bangi haingeingizwa vituoni vya kurekebishia tabia. Hata katika hali halisi ya magereza huenda hali ilikuwa ni hiyo tu. Utepetevu wa polisi wa gereza upelekea watu kuvuta bangi mle gerezani.

Wamitilia (2003) anaeleza kuhusu hali ya kiakali inayoweza kufasiliwa kupitia taswira. Matendo anayoweza kutenda mtu mara nyingi hutokana na hali yake ya kiakili. Ajizi, baada ya kujiunga na kundi la watoto wahuni waliomwingiza katika uraibu wa dawa za kulevya mpaka ajizi aliyekuwa anaongoza darasani akawa sasa anaburuta mkia darasni. Ajizi akaanza kuwatusi ndugu na dada zake. Shuleni akakosa kuhudhuria na alipohudhuria akawa kero kwa walimu na wanafunzi. Akawa ananuka fondogoo. Hizi zote zilikuwa ishara kuwa Ajizi alikuwa si yule Ajizi wa kwanza. Ajizi alieguka na kuwa beberu. Hakuzichana nywele zake hata siku moja. Hii ilikuwa ishara ya kuonyesha kuwa akili yake ilikuwa imeharibiwa na dawa za kulevya. Hali yake ya kiakili ilikuwa imeathirika kama anavyosema Cuddon 2013 kuhusu hali ya akili ya mtu inaweza kutoa taswira fulani. Maelezo ya hali ya Ajizi, yana mchorea msomaji picha kamili ya mhusika Ajizi katika *Ah! Ajizi*; jinsi alivyoathiriwa na mihadarati kiasi cha kujisahau kabisa. Alikuwa tayari kutundikwa na akili. Mawazo haya yanaoana na mhimili wa nadharia ya Mwitikio wa Msomaji kuwa kuna picha inayojengeka akilini mwa msomaji anapoisoma matini husika.

Ajizi alionyesha dalili za kuonyesha kuwa alikuwa ameharibikiwa na akili. Alivalia soksi moja kwenye mguu wa shimali kavaa kiatu kimoja kwenye mguu wa yamini; kaptura bila shati ilimkaa mwilini na hakuona hilo kama jambo kwa kuwa akili yake ilikuwa imepagawa. Ajizi alijizungumzia na kucheka nafsi yake. Alicheka ovyo ovyo na kuangua kilio bila ya sababu wala mkasa. Ajizi aliyatenda hayo yote kama ishara kuwa alikuwa ametindikwa na akili. Hakuna mtu mwenye akili timamu anayeweza yatenda hayo yote.

## 4.10 Hitimisho

Katika sura hii aina za taswira zilizotumiwa na waandishi wa matini teule kuelezea athari za matumizi ya dawa za kulevya zimeonyeshwa. Katika kuzionyesha mhimili wa nadharia ya Mwitikio wa Msomaji unaosema kuwa, kuna picha au hisia fulani zinazomjia msomaji akilini anapoisoma matini. Picha hizo humfanya msomaji kuwa na mawazo au hisia fulani kuhusu yale aliyoyasoma. Vile vile picha hizi zinaweza kumfanya msomaji kuielewa matini zaidi. Taswira zilizoshughulikiwa ni; Taswira ya maelezo, taswira ya mnuso, taswira ya mwonjo, taswira za kimsingi na kimtindo na taswira ya maelezo na kiishara. Taswira hizi zina umuhimu na mchango mkubwa katika kueleza athari za matumizi ya dawa za kulevya. Katika sura ifuatayo, mtafiti atashughulikia athari za matumizi ya dawa za kulevya.

# SURA YA TANO

# ATHARI ZA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA KWA WATOTO KATIKA MATINI TEULE ZA FASIHI YA WATOTO YA KISWAHILI

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti alishugulikia aina mbalimbali za athari za dawa za kulevya kama zilivyosawiriwa katika matini teule. Mtafiti alichunguza utovu wa nidhamu, kuathirika kimasomo, kuathirika kiuchumi, kiafya na kiakili na mwisho uraibu wa mihadarati, kifo na huzuni. Mtafiti alizingatia mhimili wa athari zinazomwathiri msomaji wa matini katika nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Msomaji huchukua hatua fulani baada ya kusoma matini. Lengo la pili la kueleza athari za matumizi ya dawa za kulevya lilishughulikiwa.

## 5.1 Athari ya kutenda maovu

Fasihi inajukumu la kuelimisha, kuonya, kuhamasisha, kudumisha uhusiano, kukuza uadilifu na kukosoa wanajamii Mutembei na Kapele. (2013). Vitendo vya Sembuli vinaendeleza utovu wa adabu. Vitendo vyake vya ubakaji, wizi, wizi wa kimabavu uharibifu wa mali ya watu na kuwachokoza vilema na vichaa kulikuwa kunaharibu uhusiano mwema katika jamii. Vitendo vyake na semi zake vinapaswa kuwa onyo kali kwa kila mwanajamii kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya. Wazazi kama Bwana Bosire wanaowadekeza watoto wao kiasi cha kutowaonya na kuwachunguza watoto kuhusu chanzo cha tabia zao pinzani wanapaswa kuanza kuchukua hatua za tahadhari. Wanapaswa kuachana na kuwadekeza wanao kiasi cha kutojali tabia zao. Bwana Bosire alikuwa amemcha mwana kulia na sasa alikuwa tayari kulia mwenyewe bila kumlaumu mtu mwingine.

Mtoto anapaswa kurekebishwa mapema na kuongozwa kuzingatia maadili ili atakapokuwa mtu mzima awe mtu mwenye maadili na mtu wa maana katika jamii yake. (Gitobu 2014). Mtoto asipoyazingatia marekebisho na mwongozo wa wazazi, walezi walimu hujikuta katika majuto makuu atakapojiangamiza mwenyewe. Kwa kujiingiza katika uraibu wa pombe na mihadarati uraibu huo unawapelekea kutenda vitendo viovu na vya hatari. Katika matini ya *Vioja vya Musa*, Musa na wenzake walizusha vita ugani Kaachonjo. Walikamatwa na polisi. Musa alifikishwa mahakamani na kusomewa

mashtaka yake. Mashahidi wakatoa ushahidi na mahakama ikampata Musa na hatia kwa makosa ya kuchochea fujo ugani Kaachonjo. Hakimu alisema,

> Baada ya kusikiliza kesi ya ushahidi uliotolewa, koti hii imempata Musa Fumbo na hatia kwa makosa aliyoshtakiwa kwayo. Uamuzi wa mahakama ni kuwa atumikie kifungo cha miezi sita katka kituo cha kurekebisha tabia. Watoto hawa wamefungwa bila faini. Vijana lazima waepukane na mihadarati kwani imeharibu maisha yao. Ripoti ya daktari iliyofikishwa hapa inaonyesha kuwa vijana waliosababisha fujo na ghasia katika uwanja wa kandanda wa Kaachonjo huwa wanatumia mihadarati". *Vioja vya Musa* 2007:40-42

Maisha ya watoto wahusika watatu, Sembuli, Musa na Ajizi yaliharibiwa kwa kutumia dawa za kulevya. Wasingalitumia dawa za kulevya wasingali yaharibu maisha yao. Juhudi ambaye hakujihusisha na dawa za kulevya alitia bidii masomoni na kufaulu. Alisoma hadi Chuo kikuu akapata kazi iliyomwezesha kugombea kiti cha ubunge na kuchaguliwa kama mbunge wa eneo bunge la Msonge. Juhudi aliyainua maisha ya wanajamii kwa kuwaletea maendeleo kama kilimo cha kunyunyizia mashamba maji, kuwajengea barabara na vijane kupata ajira.

Kutokana na vitendo vya Sembuli, Musa na Ajizi kama ilivyodhihirishwa na waandishi wa *Vioja vya Musa* (2007), *Atamlilia nani?* (2009) na *Ah! Ajizi* (2015) watoto wamefahamu dalili fulani zinazohusishwa na athari za dawa za kulevya. Dalili hizo ni pamoja na kuwa na mapuuza ya ushauri anaposhauriwa, kuacha shule bila kukamislisha masomo, kufanya vitendo vya kikatili, kutokuwa na heshima, kuwa wezi, kuwa na vitendo vyenye utovu wa maadili miongoni mwa zingine. Wahusika hawa mwishowe waliishia kuwa na maisha ya shida nyingi kwa kujiangamiza kwa njia ya kujihusisha katika uraibu wa dawa za kulevya. Musa aliishia kuwa na maisha ya shida nyingi sana. Akawa mtu wa kulewa chakari na asiyeweza kujifanyia chochote maishani. Musa alikuwa na nafasi nzuri ya kujiendeleza maishani kimasomo kwa kuwa alikuwa akiongoza masomoni na alikuwa na mhisani. Musa alikuwa na kipawa cha uongozi. Sembuli alikuwa na nafasi ya kujiendeleza maishani kwa kuwa wazazi wake walikuwa na nafasi nzuri ya kumwelimisha kwa kuwa walikuwa na pesa. Hakuitumia nafasi hiyo vizuri. Hatimaye aliteswa na mabarubaru katila klabu cha Hollywood na mwishowe kupigwa risasi na babake iliyomlemaza kabisa. Sembuli aliyewadharau na kuwatesa walemavu akawa mlemavu. Kweli mcheka kilema hafi bila kuwa kilema.

Ajizi alikuwa anafanya vizuri sana shuleni kabla ya kujiingiza katika uraibu wa dawa za kulevya. Baada ya kuanza kutumia mihadarati, alikuwa na mapuuza ya ushauri akawa na mahudhurio mabaya shuleni na kuanza kuburura mkia masomoni. Ajizi alitoroka nyumbani na kujiunga na watoto wenye nia mbaya waliompotosha na kumwangamiza. Kwa kutumia mihadarati, Ajizi alipagawa akilini na hatimaye kuaga dunia. Wazazi wake wakajawa na huzuni mwingi. Jamii ya Ajizi ilikuwa na matumaini makubwa kumhusu Ajizi maishani katika siku za usoni. Ajizi aliwahuzunisha na kuwatamausha vibaya, kupitia kukataa masomo, kutoroka nyumbani, kuwa mraibu wa matumizi ya dawa za kulevya na mwishowe kupagawa na kufa. Dawa za kulevya ni tishio kubwa kwa maisha ya watoto, vijana na watu wazima. Dawa za kulevya zina athari kubwa na zinapaswa kuambawa kabisa na kupigwa vita na wadogo kwa wakubwa.

Walinda usalama wanapaswa kuwa macho kila wakati wakishirikiana na wanachi kuwasaka wanaouza na kusafirisha dawa za kulevya. Ulaji rushwa ni sababu moja inayopelekea walanguzi wa mihadarati wapitishe dawa za kulevya kote nchini bila hofu ya kukamatwa. Huwa wanaziuza dawa za kulevya kwa watu na wanajulikana wazi na wananchi. Ni vizuri washitakiwe baada ya kuripotiwa na wananchi kwa polisi. Lalama eti wanashirikiana na walinda usalama haipaswi kuwepo. Wengine wao huwa na vikundi vinavyotishia maisha ya wale waliowafichua, lakini mkono wa serikari ni mrefu. Serikali inapaswa kulinda wananchi wake wanaowafichua walanguzi wa dawa za kulevya na walinda usalama wanaohusika kuwafunika walanguzi, wauzaji na watumiaji wa dawa za kulevya.

Ni muhimu kuwe na utaratibu wa kuwafunza watoto athari za matumizi ya mihadarati. Kuwe na programu za runinga na redio wikendi, zinazohusisha watoto wakisimulia hadithi kuhusu athari za dawa za kulevya. Watoto wanaweza kukariri mashairi kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya. Watoto wanawezaletewa mchezo wa kuigiza kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya. Filamu na kanda za video kuhusu dawa za kulevya zinapaswa kusambazwa shuleni, kanisani, sokoni na kwenye mikutano ya hadhara zote zikifunza kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya.

Kila kundi la waigizaji linapaswa kuuchukulia mzigo wa mihadarati kama mzigo wa kitaifa na janga la kitaifa na kushiriki vita dhidi ya dawa za kulevya kwa kutunga mtungo au michezo ya kuigiza kuhusu athari za dawa za kulevya. Katika Sikukuu za kitaifa wapewe nafasi kuwasilisha tungo zao kuhusu vita dhidi ya mihadarati. Serikarli inapaswa kutenga fedha za kutosha za kupambana na dawa za kulevya ili kuwe na kongamano, semina na warsha kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya. Shuleni watoto washirikishwe katika tamasha za muziki zinazohusu athari za matumizi ya dawa za kulevya. Wanaweza kariri mashairi, imba nyimbo, michezo ya kuigiza kwa mashindano kutoka mashinani hadi ngazi ya kitaifa. Kunapaswa kuwa na utaratibu wa kuwatibu waraibu wa mihadarati. Kukiwa na dawa ambayo watadungwa nayo ili wakiziona dawa za kulevya wahisi kutapika itawafaa sana. Ni muhimu kuwa na utarabu wa ushauri kutoka nyumbani, shuleni, kanisani, mikutano ya hadhara kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya. Wanaofichua walanguzi, wauzaji na watumiaji wa dawa za kulevya wawe wanatuzwa. Vita dhidi ya dawa za kulevya viwe ni vya kila mtu.

### 5.2 Aina mbalimbali za athari zilizosawiriwa katika matini Teule

Athari kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu TUKI (2000) ni mabadiliko yanayoletwa na mtu au kitu kingine. Athari inaweza kuwa hasi au chanya. Aghalabu, athari huwa ya kiakili. Athari inapokuwa hasi, huwa na mielekeo wa kupinga, kushindwa, kukata tamaa, kukosa matumaini au kuwa jumla kwa na mielekeo pinzani. Athari ikiwa chanya ni kuwa kuna mielekeo unaoegemea mazuri na kuwa na matumaini. Mara nyingi anayeathiriwa na athari anaweza kuonyesha athari yake kwa vitendo vyake au kupitia misimamo au maneno anayoyasema. Natharia ya Mwitikio wa Msomaji ina mhimili unaozingatia kuwa msomaji wa matini fulani baada ya kuisoma matini huchukua hatua fulani kama njia ya kuonyesha athari aliyoipata baada ya kuisoma matini.

Kanake (2013), anaelezea kuwa athari haitokei hivyo bure. Akichunguza makosa ya kifonolojia miongoni mwa mwanafunzi wa Kiigembe katika ujifunzaji wa Kiswahili, athari hutokea kwa sababu ya kuingiliana kwa lugha hizi mbili ambazo ni Kiswahili na Kiigembe. Maoni ya Kanake (keshatajwa) yanampa msomaji hakikisho la kujua kuwa ili athari iwepo kuna mwingiliano fulani. Msomaji anapotagusana na matini huwa na mwigiliano fulani unaosababisha athari fulani.

Nandi (2009), akifafanua athari, alitafitia ubainishaji wa athari za makosa katika Insha za wanafunzi tathmini ya athari za makosa hayo katika uelewekaji wa maana katika Kiswahili sanifu. Uchunguzi wake uling'amua kuwa athiri ya lugha ya mama kama vile Kikisa, makosa yake yanaweza athari maana, badili maana na kupoteza maana husika kabisa. Athari hizi ni hasi na zinaathiri mawasiliano kwa njia kubwa sana.

### 5.3 Utovu wa Nidhamu

Matendo ya wanajamii humulikwa kwa njia mbili. Yale mema wanayoyatenda ambayo husifiwa na yale maovu ambayo yanapaswa kupuuzwa na kukashifiwa kama utovu wa nidhamu. Kila jamii huwa na njia zake za kufunza maadili. Watoto na Vijana Aghalabu hufunzwa maadili ili watakapokua wawe watu wenye maadili na watu wanaokubalika katika jamii.

Wanadamu na viumbe vyote vilivyo na uhai huwa na tabia ambayo wanajifunza na bali si ya kuzaliwa nayo. Kimani na Chimerah (1999) wanafafanua kuwa tabia ni mara mbili. Yaani tabia nzuri na tabia mbaya. Mwanadamu anapozingatia kutenda matendo yaliyo mema huchukuliwa kuwa na matendo mema na kwa hivyo kuwa na tabia njema. Mwanadamu anapokuwa na tabia inayokiuka kanuni za kijamii huchukuliwa kuwa mtu mwenye tabia mbaya. Vitendo vyake huchukuliwa kuwa vibaya. Musa hakurekebishwa mapema kuhusu madhara ya dawa za kulevya. Umaskini ulimsukuma kuanzisha biashara ya uuzaji wa sigara na bangi shuleni. Vilevile alianzisha matumizi ya mihadarati shuleni. Uadilifu wake ukawa katika mizani. Alimdanganya mwalimu walipokuwa wakivuta sigara na kusema hakujua ni kina nani walikuwa pale nje.

Matumizi ya dawa za kulevya kunamplekea Musa kutumwa nyumbani ukweli ulipobainika. Huu ukawa ndio mwanzo wa kuporomoka kwa maisha yake. Nyota yake ya masomo na uongozi iliyokuwa imeng'ara ikaanza kuzama. Akitumikia adhabu ya kutumwa nyumbani, yeye na watoto wengine walizusha zogo ugani Kaachonjo kukawa na vita vikali. Watu wengi walijeruhiwa sana. Walikamatwa na kutiwa rumandi, licha ya kushauriwa na wavyele wake, bangi ilimfumba macho na Akili asiweze kuyakumbuka maneno ya wosia wa mama.

> “Musa ukiwa shuleni, lazima ulenge masomo pekee, usihadaiwe na wanafunzi wengine kuhusu mihadarati. Ukifanya hivyo utapwaya kimaisha *Vioja vya Musa* 2007:26.

Musa aliyapuuza maneno ya mamake kuwa asidanganyike na watoto wabaya aje kuingilia dawa za kulevya zije kumwangamiza na kumharibia maisha yake ya siku za usoni. Musa aliangamia kimasomo na maishani kwa kupuuza ushauri wa mamake mzazi. Kutozingatia ushauri wa mama, Musa akawa mraibu wa dawa za kulevya. Musa alijiunga na genge la waraibu wa dawa za kulevya. Aliweza kuhadaiwa na genge kuwa

> “Ukitaka masaibu yote yanayokukumba kutoweka mara moja jaribu bangi. Itausafisha ulimwengu wako na kuuondoa uchafu wote. Hautababaishwa tena. Mambo hayatakwenda segemnege” *Vioja vya Musa* 2007:50-52.

Ingawa Musa aling’ang’ana kuacha ikawa ni vigumu mwenyewe alisikika akijuta ni kwa nini alijiingiza kwa uraibu ule. Ulimharibia pesa zake alizozipata kutokana na uhamali. Alisikika akisema,

> “Haki ya Mungu, sitarudi kunywa pombe tena. Inanivunjia maisha!
> *Vioja vya Musa* 2007: 53-54.

Musa alitaka kujitoa katika uraibu huu lakini ikawa ni vigumu. Wanaojihusisha na matumizi ya dawa za kulevya waonywe kuwa kuna hatari ya kujiingiza kwa uraibu wa dawa za kulevya. Kulingana na mtandao wa Washington State Healthy Youth Servey (2012) wanasema kuwa watoto wanaotumia bangi kupunguza wasiwasi na kuboresha mielekeo wao shuleni hukumbwa na ugumu wa kukumbuka mambo, upotovu wa fikira na mielekeo, mawazo yaliyotiwa chumvi au yasiyokuwa na mantiki, njozi za ajabu, wazimu, wasiwasi, mfadhaiko, upungufu wa kiakili, kukosa motisha na bidii, kupoteza hamu katika shughuli walizokuwa wakifurahia na matatizo ya kiafya. Wengine wanakuwa na utovu wa nidhamu, kuwa wanatoa uvundo au harufu, huwa hawana msimamo, kuonekana mjinga na mwenye wasiwasi, kucheka cheka ovyo ovyo, kuwa na matumizi yasiyoeleweka ya pesa.

Sembuli kwa msukumo wa bangi anadhihirisha kuwa semi zake na matendo yake yana utovu wa nidhamu. Alipopandwa na mori njia yake yakuonyesha hasira yake ilikuwa ni kuugonganisha mlango. Sembuli alimwambia mamake kuwa nyumba haikuwa yake

wala ni ya baba. Alimfokea mamake na kumwambia, ampikie mayai matatu na alitaka siku nyingine kupikiwa chakula na mamake. Alimlazimisha kumfanyia vitu kwa lazima. Kwa sababu ya utovu wa nidhamu.

> "Nakuambia nataka unikaangie mayai matatu sasa hivi. Sili sili siliii, Mimi sijui hayo. Nasema nataka chakula tu. Nipikie chakula …. Nipikie chakula…." *Atamlilia nani?* (2009:1-18)

Shuleni Sembuli aligombana na walimu pamoja na wanafunzi wenzake bure bilashi. Sembuli alikuwa na kesi chungu nzima mpaka walimu wakatamani asije shuleni. Sembuli alikuwa na vitendo vya kikatili, viliwafanya ndege, paka, mbwa wa watu kumwogopa. Sembuli aliwachokoza, akawachapa na kuwaharibia vilema na maskini mali yao. Nao walimlaani. Vitendo vya kuchokoza watu, kuwatusi, kuwapiga na kuwaharibia vitu vyao ni utovu wa nidhamu.

> "Mtoto wewe unanifanya hivi? Haya Mungu yupo". *Atamlilia nani?* 2009:5

Fasihi inajukumu la kuelimisha kuonya, kuhamasisha, kudumisha uhusiano kukuza uadilfu kukosoa wanajamii. Vitendo vya Sembuli kuendeleza utovu wa adabu unapaswa kuwa onyo kwa wasomaji. Sembuli alifurahia kuharibu mali ya watu, akawa mtundu, mwenye ugomvi, dharau, mtovu wa adabu asiye na heshima. Sembuli akawa mwizi wa kuku na mabata ya watu. Alikuwa na miaka kumi na sita akiwa na kesi nyingi za uharibifu alikamatwa mara kwa mara na polisi. Alitolewa na babake kwa kutumia pesa na ushawishi aliokuwa nao katika jamii. *Atamlilia nani?* 2009:12-15.

> Sembuli aligeuka na kuwa mwizi, mwizi wa hadaa au tapeli, mbakaji na mwizi wa nguvu. Aliwapiga watu ovyo ovyo akidai kuwa alikuwa akiwatia adabu, laana ya walemavu ilimpata alipo mchokoza Finali katika kilabu cha Hollywood alipopigwa na kulemazwa akapona lakini baadaye akaja kulemazwa na risasi ya babake mzazi alipojaribu kumwibia pesa zake. *Atamlilia nani?* 2009: 25-34.

Mtoto anapaswa kurekebishwa mapema na kuongozwa kuzingatia maadili ili atakapokuwa mtu mzima awe mtu wa maadili na mtu wa maana. Asipozingatia mashauri atakuwa mwenye majuto mengi atakapojiangamiza mwenyewe.

> Wazazi wa Ajizi walimshauri tu jinsi ya kutia bidii shuleni jambo alilolifanya na akatiafora masomoni. Pindi tu alipojiunga na genge la watoto wavuta bangi: Manywele, Makorokoro, Matembo na Matindija, tabia yake ilibadilika kabisa. Akawa mtoto mtundu shuleni, akawa anafika nyumbani usiku wazazi wake hawakutaka kuchunguza mienendo yake ili kujua chanzo chake cha kuburuta mkia masomoni na kubadilika kitabia. Shuleni akawa kisirani kwa walimu na wanafunzi ambao walimfurahia kutokuwa shuleni. *Ah! Ajizi* 2015.

Utovu wa nidhamu ni suala la dharura kwa watoto, wazazi na serikali. Lazima lishungulikiwe ipasavyo ili kuwanusuru watoto wetu. Ni lazima mienendo ya watoto, vitendo vyao na lugha wanayoitumia iwe ikichunguzwa mara kwa mara kubaini kama kuna uwezekano wa matumizi ya dawa za kulevya. Iwapo kutakuwa na uwezekano wa matumizi ya dawa za kulevya hatua madhubuti zichukuliwe kuwarekebisha.

### 5.4 Kuathirika Kiakili na Kiuchumi

Kulingana na WHO (2015), takribani watu milioni 27 Duniani wanaishi na athari za kiafya za matumizi ya dawa za kulevya na wengine laki nne wanakufa kila mwaka kutokana na matumizi ya dawa za kulevya. Kujidunga dawa za kulevya kwa kutumia sindano, kuvuta, kula, kumeza, kunusia, kunywa, kutafuna na kumeza kunachangia kwa asimilia 30 ya maambukizi mapya ya virusi vya HIV na inachangia pia katika maambukizi ya Hepatatis B na C kote duniani. Magonjwa haya yanazidishia athari za kiafya miongoni mwa watumiaji wa dawa za kulevya.

#### 5.4.1 Athari ya Kiakili

Casey J B na wenzake (2008) wanaeleza kuwa akili ya watoto huwa ingali inaendelea kukua na haijakomaa. Matumizi ya dawa za kulevya mapema kunaathiri akili ya mtoto sana. Mohammed katika *Atamlilia nani?* (2009) anasema kuwa;

> "Sembuli mtoto mdogo alikuwa na hasira ambayo haikueleweka ilikuwa ya nini?" *Atamlilia nani?* 2009:5

Hamaki hii ilisababishwa na athari ya dawa za kulevya ambazo zilikuwa tayari zimeathiri akili yake na kumsukuma kutenda vitendo ambavyo hakuweza kuvizuia. Sembuli alisikia sauti kichwnai mwake iliyomwambia afanye vitendo vyenye kukera. Sauti hii ilikuwa sauti ya akilini na ni ishara tosha kuwa alikuwa ameathiriwa kiakili.

Alimfokea mamake akamfanyia vitimbi mbele ya watu na kuviparaganya vyombo vilivyokua mezani vya staftahi na vikombe vikavunjika Na kuwa vigae vigae. *Atamlilia nani?* 2009:1-34.

Mhusika Musa katika *Vioja vya Musa* 2007 aliporudi nyumbani baada ya kifungo kukamilika, alikuwa kaharibikiwa na akili kabisa. Mwandishi anasema,

> "Mamake alijaribu kumshauri kurudi shuleni na kuendelea na masomo lakini alinyamaza kimya na hakusema kitu. Mamake alipozidi kumsihi si kidogo lakini Musa alikuwa pale tu kama mfano wa mtu kanyamaa kimya hazidishi hapunguzi. Alikuwa kama mgonjwa wa kiakili. Musa alikuwa ameathirika kiakili na kubadilika ajabu. Babake alijaribu kumshauri lakini hakusema chochote. Alinyamaza tu na kukaa kama mtu ambaye amezubaa na kuchanganyikiwa. Ndoto yake ilikuwa kazimika. Nyota yake iliyong'aa hapo awali ikawa imezimika." *Vioja vya Musa* 2007:50-51

Ajizi katika matini ya *Ah! Ajizi* 2015 alikuwa mtoto mzuri. Ajizi baada ya kuanza kutumia mihadarati alikuwa mtoto mwenye bidii masomioni, alikuwa akiongoza kwa masomo darasani. Alikuwa safi. Alipoanza kutumia dawa za kulevya aligeuka na kunuka kama beberu. Alinuka na kutuoa fee. Alinuka fondogoo. Nywele zikawa za kipilipili. Hakujijua wala kujitambua. Akili ya mhusika ilikuwa kadhoofika kabisa. Mwandishi anasema;

> "Alipagawa na akili akawa mwendawazimu. Alikuwa mwenye kungu na kamsa za mchana ambazo hazikuwa za kawaida mle msonge, huku akipiga duru na kucheka ovyo ovyo. Alianza kuvalia soksi moja, kiatu kimoja, kuvaa kaptura bila shati. Ajizi akawa anajizungumzia na kucheka nafsi yake." *Ah! Ajizi* 2015:18-20.

Haya yote aliyatenda kama ishara ya kuonyesha kuwa alikuwa amepagawa na akili. Asingeweza kujisaidia maishani. Watoto kama hawa baadaye huwa ni mzinga wa jamii. Kuwatafutia tiba na kuwatunza maishani.

Matumizi ya dawa za kulevya huathiri mtumiaji kiafya. Moyo wa mtumiaji wa bangi udunda haraka kuliko kawaida. Kinywa chake chakauka, macho kuwa mekundu,

kusahau kwa haraka na kupata hamu mkubwa ya chakula. Huvutaji wa bangi huathiri mapafu, ini na ubongo kufikia hata kuwa mwendawazimu kama Ajizi.

### 5.4.2 Athari ya Kiuchumi

Sembuli alipowaharibia watu mali yao, akawa mwizi, tapeli, mbakaji na mwizi wa kimabavu alikuwa na kesi nyingi. Babake Bwana Bosire alikuwa tajiri na mwenye ushawishi wa cheo, alitumia pesa nyingi kuwahonga polisi na waliotuhumiwa mpaka akafilisika. Alimwambia Sembuli siku moja.

> "Sasa mapato yetu yemekuwa madogo, hatuwezi tena kukupa pesa kama zamani", *Atamlilia nani?* 2009:15-19

Sembuli alimfanya akaathirika kiuchumi akabakia na fedha kidogo. Hii ni dhahiri shahiri kuwa mtoto anayetumia dawa za kulevya anaweza kumwathiri mzazi wake kiuchumi.

## 5.5 Kuathirika Kimasomo

Kulingana na Uchunguzi uliofanywa Marekani mjini Washington mwaka wa 2012 ilifahamika kuwa watoto wengi wa umri mdogo hutumia pombe na bangi. Watoto wa miaka 12-17 hutumia dawa za kulevya na huwa wameathirika kiasi cha kutafuta matibabu hospitalini. Wengi wao hupata alama za chini shuleni. Akili zao uathirika zaidi na kushindwa shuleni. Wengine hulazimika kuacha shule. Watoto wengine hukosa motisha na bidii na kupoteza hamu katika shuguli walizokuwa wakifurahia kama vile masomo.

Kuna mifano kadha wa kadha ya watoto walioathirika kimasomo kwa sababu ya matumizi ya dawa za kulevya. Musa katika *Vioja vya Musa* 2007 alikuwa mtoto mwadilifu, mwenye bidii masomoni na kiongozi mzuri sana shuleni. Dawa za kulevya zilimplekea kufungwa jela na baada ya kumaliza kifungo alikataa katakata kurudi shuleni. Kituoni cha kurekebisha tabia alizidisha utumiaji wa bangi mpaka akili yake ikaathirika kabisa. Kilikuwa ni kinaya kuona katika kituo cha kurekebisha tabia ya ulevi wa bangi, ndipo kulikuwa na bangi chungu nzima. Hili lilitokana na utepetevu wa kiongozi wa kituo cha kurekebisha tabia pamoja na wale askari waliofanya kazi pale.

Hakuendelea na masomo. Musa aliamua kufanya kazi ya uhamali. Mwishowe alikamatwa kwa tuhuma ya wizi wa nyanya. *Vioja vya Musa* 2007.

Sembuli alikuwa mtoto mwenye bidii masomoni. Alipoanza uraibu wa dawa za kulevya aliathiriwa kiakili. Akawa mwingi wa hasira. Hamaki ilimfanya kumfanyia mamake vitimbi. Shuleni akawa kero kwa walimu na wanafunzi. Kwa utovu wake wa nidhamu Sembuli aligongana na kila mtu. Shuleni akawa msumbufu kwa wanafunzi walimu na kutatiza masomo shuleni. Walimu walipojaribu kumwadhibu lakini babake aliyemdekeza alimkinga. Walimu waliamua kumnyamazia kimya na kumtazama kwa macho. Sembuli akaacha shule na kuwa mchokozi, mfitini wa vilema na vichaa, mharibu wa mali ya watu, mwizi, tapeli na mwizi wa kimabavu. Sembuli akawa tisho na kero kwa jamii.

Mhusika Ajizi katika matini ya *Ah! Ajizi* 2015, alikuwa mwenye bidii masomoni. Matumizi ya bangi yalimfanya akazembea masomoni, na kuwa wa mwisho darasani. Alikuwa akiongoza masomoni lakini akawa anavuta mkia. Ajizi aligeuka na kuwa mtovu wa nidhamu. Alikuwa kisirani kwa walimu na wanafunzi ambao walimfurahia kutokuwa shuleni. Alijiunga na genge la watoto watukutu watumiaji wa bangi waliompangia maangamizi ili asiendelee na masomo. Aliacha shule, akatorokea msituni mpaka alipopagawa na kuwa mwehu. Alikufa na kuleta huzuni kwa jamii.

Kifo cha mtoto mdogo kama Ajizi, kutoendelea na masomo kama Musa na Sembuli ni hasara kubwa kwao, kwa wazazi wao na kwa jamii nzima. Kuna watoto wametamatisha masomo yao na kuwa tisho kwa jamii. Ni muhimu wazazi, walimu na jamii kuwa macho kuchunguza mienendo ya watoto wao. Ni muhimu kuketi nao, kujadili kuhusu athari za dawa za kulevya na jinsi ya kuepukana na matumizi ya dawa za kulevya. Wazazi lazima wawe na miongozo ya kuwaeleza umuhimu wa tabia nzuri. Watoto waelewe umuhimu wa afya, kutekeleza majukumu nyumbani, kufuata sheria za familia na za shule, kuheshimu wazazi na watu wengine, mahudhurio ya shule. Wazazi wafuatilie tabia za wanao na mara kwa mara kuwa na mawasiliano na ya kuwashauri.

### 5.6 Athari ya Kutenda Maovu na Kufungwa Jela

Kwa Mujibu wa Washington State Health Youth Servey (2012) ni kuwa watoto wanaotumia bangi wanaweza kuasi yale wanayoagizwa kuzingatia. Watoto hao uasi na kuwa kinyume cha kuzingatia maadili yanayokubaliwa na wanajamii kuwa na tabia pinzani. Mienendo mibaya husababisha kutenda maovu ya kila aina pasi na kufikiria athari za kutenda maovu kama vile kufungwa jela. Wakati mwingine watoto hao uhisi chuki moyoni, chuki hiyo inawezampelekea kutenda vitendo viovu kama vile vita. Vita vinakuwa na athari zake. Watoto wanapotumia dawa za kulevya huweza kuwa na moyo wa kulipiza kisasi. Tabia hii ya kulipiza kisasi hukithiri sana miongoni mwa watumiaji wa dawa za kulevya. Tabia hii inaweza kusababisha utendaji wa matendo maovu yanayoweza kuwa na athari zingine kama vile kufungwa jela.

Matini teule zinazotafitiwa, *Vioja vya Musa* (2007), *Atamlilia nani?* (2009) na *Ah! Ajizi* (2015) zina mifano kadha wa kadha inayodhihirisha ukweli kuwa watoto wanaotumia dawa za kulevya hutenda vitendo viovu vya kuhatarisha maisha yao kutokana na athari za dawa za kulevya. Sembuli katika *Atamlilia nani?* (2009) alianza kuwaiba kuku na bata wa watu na kuwachoma na kuwala, kitendo hicho ni kiovu na kilisababisha uhasama baina ya Sembuli, familia ya Bwana Bosire na wale walioibiwa kuku na Bata wao. Sembuli aliwapiga mbwa, paka, ndege, walemavu, watu wenye vichaa, maskini na kuwaharibia vitu vyao kiholelaholela. Sembuli alimfanyia vitimbi kama kumrushia mchanga mbele ya watu. Alimfokea mamake na kumlazimisha ampikie chakula saa nane za usiku.

Sembuli aliyatenda maovu ambayo yangempelekea kufungwa jela kama babake asingalikuwa na uwezo wa kifedha na ushawishi wa kijamii. Bwana Bosire alitumia pesa nyingi kuwahonga polisi waliomsaka Sembuli kila siku. Asingalikuwa na baba mwenye pesa na ushawishi asingalikuwa huru. Polisi wangekuwa wamemnasa na kumfikisha kotini na kufungwa.

Katika *Vioja vya Musa* 2007 Musa na Jotokubwa waliwaongoza rafiki zao kuzusha fujo ugani Kaachonjo. Vita vilizuka na watu wengine wakajeruhiwa bure bilashi. Watoto hawa walisababisha fujo kwa kuwa akili zao zilikuwa zimeathiriwa na dawa za kulevya zilizowasukuma kutenda maovu. *Vioja vya Musa* 2007: Musa na Joto kubwa

walikamatwa na kuwekwa rumande. Walifikishwa mahakamani na kufungwa jela. Jamii ikampoteza Musa aliyekuwa jela. Jamii ikampoteza Musa aliyekuwa mtoto mwaminifu, mwadilifu, kiongozi shupavu na mwenye bidii masomoni.

Ni muhimu kuwa na mikutano ya kuwahamasisha watoto na washikadau wote kuhusu dawa za kulevya. Shirika la NACADA linapaswa kushirikiana na wazazi, watoto, walimu, viongozi wa serikali na wa kidini kupanga semina, warsha na kongamano za mara kwa mara kote nchini. Kuwaelimisha watoto kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya ili waweze kujua athari zake via kuepukana nazo. Kuwe na mpangilio wa kuwahusisha watoto wa shule za msingi na sekondari kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya, kupitia nyimbo, mashairi, michezo ya kuigiza, hotuba na filamu na semina zinazoonyesha watoto walioathiriwa na dawa za kulevya. Shuleni, somo la dawa za kulevya lizingatiwe kwa makini kuanzia chekechea hadi shule ya upili. Kanisani wahubiri na wanaofunza watoto kanisani wazingatie mpangilio wa kuwahusisha watoto kuigiza athari za matumizi ya dawa za kulevya. Selikali inafaa kutangaza dawa za kulevya kama janga la kitaifa na kutenga fedha za kuzipiga vita dawa za kulevya. Dawa za kulevya zisipopigwa vita watoto wengi na Vijana wataangamia.

Wazazi, walezi wa watoto na walimu wanapaswa kuwa na mwongozo dhabiti wa kuzingatia katika kuchunguza iwapo mtoto anashiriki matumizi ya dawa za kulevya. Mwongozo huu unapawa kuwa na njia mwafaka za kuwasiliana na watoto kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya. NACADA inapaswa kuwa na kipindi cha kuwaelimisha watoto kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya, kwenye runinga na redio siku ya Jumamosi au Jumapili wakati watoto wamo nyumbani. Pia kunapaswa kuwa na kanda za video zinazoonyesha watoto walioathiriwa na matumizi ya dawa za kulevya. Kanda hizi zionyeshwe shuleni, kanisani na kwenye semina na warsha au kongamano za kufunza watoto kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya.

Mwandishi wa *Ah! Ajizi* (2015) anaeleza kuwa mwanzoni, Ajizi na Juhudi walikuwa na bidii za duduvule masomoni. Baada ya kuanza matumizi ya dawa za kulevya akabadilika kabisa.

> "Ajizi akaanza kufika nyumbani akiwa amechelewa. Ushauri wa wavyele wake ukaambulia kwenye maskio yaliyokwisha

> kuukaribisha uziwi usiojua tabibu wala tiba. Ajizi akawapuuza wazazi wake na kuwa mkaidi mkubwa. Ushauri ulikuwa kama kumpigia mbuzi gitaa. Ajizi aliwatusi wazazi wake, wanafunzi wenzake dada na kaka zake. Ajizi akawa mchokozi wa kutajika. Akawa anapigana na wasiomkosea. Ujeuri wake ukakithiri kama moshi!! *Ah! Ajizi* 2015:4-6.

Ajizi aliacha shule akiwa darasa la sita. Alijiunga na marafiki watundu, Matindija, Matembo, Manywele na Makorokoro wa kakaa msituni kwenye Bangwa waliloliita "Njoo tuvute" katika mtaa wa Konambaya. Waliwatishia wachanja kuni pale mwituni. Waliwatishia na kuwabaka mabinti na wake wa watu. Wakawaibia watu fedha zao. Kama si utepetvu wa walinda usalama watoto hao wangekamatwa na kutiwa dani. Wanakaria Wamsonge na serikali walijua pale walikaa na hawakushughulika hadi Ajizi alipopagawa na kuwa mwehu na hatimaye kuaga dunia. Wanakijiji wa mtaa wa Konambaya wangeshirikiana mapema kuyanusuru maisha ya Ajizi na watoto wengine na kupigana na matumizi ya dawa za kulevya wangeyanusuru maisha ya Ajizi.

### 5.7 Uraibu wa Mihadarati

Meier M.H na wenzake (2012) wanaeleza kuwa watoto wanaokuwa na uraibu wa matumizi ya bangi huwa na upungufu wa kiakili wanapostawi kutoka utotoni had miaka ya kuanza kuwa watu wazima. Hard Y.L na wenzake wanasema kuwa watoto na vijana wanaoanza kutumia dawa za kulevya mapema na kuendeleza matumizi ya dawa za kulevya huwa na uraibu wa matumizi ya dawa za kulevya-uraibu huo huwaweka hatarini ya kujikuta katika majanga kame vile maradhi, tabia mbaya inayoweza kuwahatarishia maisha yao. Uraibu wa dawa za kulevya, ni mazoea ya kutumia dawa za kulevya na kumweka mtumiaji katika hali ya kuwa hawezi kukosa kuitumia kwa madhara yatakayompata.

Sembuli katika matini ya *Atamlilia nani?* 2009, alikuwa mraibu wa dawa za kulevya. Sembuli alipata fedha za kununulia mihadarati kutoka kwa babake na pili kutoka kwa kundi la wahuni la U-gangster. Hapo ndipo alipata fedha za anasa na kununulia mihadarati. Sembuli alipolemazwa na kichapo cha mabarubaru saba katika mtaa wa Hollywood alitimuliwa kwenye genge lile. Ilikuwa sadifa kuu kuwa babake naye alikuwa kafilisika. Hakuweza kupata pesa kununua mihadarati. Marafiki zake nao walimtoroka. Aliteseka sana kama watesekavyo waraibu wa mihadarati.

Aliwafuatafuata rafiki zake angalau ainuse mihadarti hiyo. Sembuli alimsihi Saruti amsihi Bosi amkubali katika genge la U-gangster ili apate pesa kununua mihadarati.

> “Saruti na kusihi umshawishi Bosi akubali kunirejesha katika kundi la U-gangester angalau ni pate pesa za kununulia “unga’ unajua bila shaka kutoendelea kuzitumia dawa hizo kutanisababishia maafa” *Atamlilia nani?* 2009:25-31

Saruti alimshauri kumwibia babake fedha laki nane. Kujaribu kumwibia babake alipigwa risaai iliyomharibia mishipa ya hisia. Sembuli akawa mlemavu aushini mwake. Familia yake ilihuzuniksa na wakalia.

Musa alipokamatwa na kutiwa katika seli, wazazi wake walimtafuta sana. Walimkuta alikuwa kalala katika seli. Wazazi wake walihuzunishwa sana na kitendo cha Musa kukamatwa. Mama yake alikuwa amemshauri kuepukana na watoto wenye tabia mbaya asije akaambukizwa mienendo mibaya. Mamake alikuwa amemshauri kuwa tabia mbaya ingempelekea kujuta na kumharibia kesho yake. Mamake alisema,

> “Kefule! Mungu wangu, huyu mwana amejichoma mwiba kwenye kidonda. Nani sasa atamwauni? Babake Musa hakusema lolote. Alionekana kupigwa na bumbuazi. Hatimaye alisema machozi yakimtoka,
> “Musa umenichafua roho. Sasa hili nalo tutafanyaje?
> *Vioja vya Musa* 2007:35

Kama Musa, vijana wengi siku za leo ndivyo wanavyowahuzunisha wazazi wao kwa matendo maovu. Musa, mhusika mkuu katika *Vioja vya Musa* (2007) aliendeleza uraibu wake wa dawa za kulevya. Akakataa shule katakata. Musa aliungana na vijana wenzake kupiga mtindi na kushiriki raha na starehe nyinginezo. Wazazi wake walihuzunika sana. Musa alivuta bangi hadi fedha zake zote zikamwishia akawa hana senti mfukoni. Alijisahau kabisa na kuimba nyimbo za kila aina akielekea alikoishi. Alivamiwa na vijana wenzake na kunyang’nywa pesa alipolewa chakari, Musa alihuzunika kwa kuibiwa pesa zake na kulala kwa mtaro. Aliendelea katika hali hiyo mpaka alipokamatwa kwa tuhuma ya wizi wa nyanya.

Ajizi alianza matumizi ya dawa za kulevya alipojiunga na genge la wahuni. Timu hiyo ilihusisha Manywele, Makorokoro, Matembo na Matindija. Waliishi msituni na kutenda maovu. Alipopagawa alianza kupiga kamsa. Wazazi na wanajamii walihuzunishwa na vitendo vyake. Wanakitongoji waliungana wakamsaka na kumpata. Afya yake ilikuwa kadhoofika. Alipelekwa hosptalini lakini alikohoa, “Koh! Koh! Akakata roho” tukio hilo lilileta huzuni sana kwa wazazi na wanao.

### 5.8 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti ameshughulikiwa usawiri wa athari za matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule za Fasihi ya watoto ya Kiswahili kama: Utovu wa nidhamu, Kuathirika kiakili, Kuathirika kiuchumi, Kuathirika kiafya, kutoendelea na masomo, kufungwa jela, kusababisha kifo na huzuni. Katika sura iliyofuata mielekeo wa watoto ulishughulikiwa.

# SURA YA SITA

# MIELEKEO WA WATOTO KUHUSU DAWA ZA KULEVYA KATIKA MATINI TEULE ZA FASIHI YA WATOTO YA KISWAHILI

## 6.1 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia Uchanganuzi wa hojaji ya Mizani ya Likert na dodoso ya mjadala wa wasailiwa kwa makundi ili kutathimini mielekeo wa watoto kuhusu dawa za kulevya. Utathimini wa mielekeo wa watoto kuhusu dawa za kulevya ni muhimu kwa ushauri wao. Sura ya nne ilishughulikia ufafanuzi wa taswira zilizotumiwa kusawiri matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule za Fasihi ya watoto. Sura ya tano ilishughulikia athari za matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule. Sura ya sita ilijikita katika kuchunguza mielekeo wa watoto.

## 6.2 Uchanganuzi wa Hojaji ya Mizani ya Likert

Holland (1975) anaeleza kuwa mielekeo huwa ni jambo la hisia. Kwa vile mielekeo wa msomaji ni wa kisaikolojia, unapaswa kutathiminiwa kwa vifaa ambavyo vitamsababisha msailiwa kujieleza vizuri. Mahochi (2005) anaeleza kuwa hojaji ya Mizani ya Likert ni muhimu katika kuchunguza mielekeo ya wasailiwa kuhusu jambo fulani. Ili hojaji ya Mizani ya Likert iweze kusababisha data ya kutosha inapaswa kuwa na maswali mengi. Kuchunguza mielekeo ya wasailiwa, mtafiti awe na vifaa zaidi ya kimoja. Carranza (1982) na Oskamp (1991) wanakubaliana kuwa vifaa zaidi ya kimoja humpa msailiwa nafasi ya kuelezea mielekeo wake. Wanapendekeza kuwa hojaji ya maswali huru na funge yanaweza kutumiwa. Hojaji funge humfunga msailiwa na hujibu maswali ya mtafiti aliyoyaandika. Maswali huru hutoa nafasi kwa msailiwa kujieleza kwa njia ya urahisi. Wasailiwa walipewa hojaji ya Mizani ya Likert baada ya kusoma matini teule *Vioja vya Musa (2007), Atamlilia nani? (2009) na Ah! Ajizi (2015).* Waliitajika kusoma matini teule ili wawe na ufahamu wa athari za dawa za kulevya. Ufahamu wa athari za dawa za kulevya uliwawezesha kueleza mielekeo wao.

Wasailiwa walipewa hojaji ya Mizani ya Likert yenye maswali kumi yenya vibadala vitano. Kila msailiwa alitarajiwa kukichagua kibadala kimoja. Majibu ya wasailiwa yalichanganuliwa kwa kuzingatia kibadala ambacho msailiwa alichagua. Vibadala vilikuwa vitano: Nakubali kabisa, Nakubali, Sina hakika, Sikubali na Sikubali kabisa. Wale wote waliochagua kibadala cha nakubali kabisa au nakubali walichukuliwa kuwa na mielekeo chanya. Wale wote waliochagua vibadala vya sikubali na sikubali kabisa

walichukuliwa kuwa na mielekeo hasi. Waliochagua sina hakika waliwekwa katika kundi lao. Asilimia ya kila kundi ilihesabiwa ili kutimiza lengo lililowekwa na mtafiti kuwa kigezo cha kutathimini mielekeo ni hamsini na tano (*55%*). Kundi lililofikisha asilimia 55% au zaidi ndilo lilichukuliwa kuwa na mielekeo chanya, huku lile lingekuwa na asilimia chini ya hamsini na tano (55%) lingechukuliwa kuwa na mtazamo hasi. Jumla ya maswali yalikuwa kumi. Ili kupata asilimia ya wasailiwa wa kila kauli, idadi ya wavulana na wasichana ya kila kibadala ilijumlishwa ili kuona ni wangapi kwa jumla ya wote 18 walichagua kila kibadala. Idadi yao kwa jumla ya wote 18 mara mia moja ili kupata asilimia. Ili kupata asilimia ya wasichana au wavulana idadi ya waliochagua kila kibadala ilikuwa 9 kwa sababu kulikuwa na wasichana 9 na wavulana 9. Ilipozidishwa kwa 100 moja kupata asilimia.

Jedwali 3: Kauli ya kwanza: Dawa za kulevya huwa na athari nyingi kwa watoto wanaozitumia

| Jinsia | Mwitikio chanya | | Mwitikio Hasi | | Wasiokuwa na hakika | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | |
| Wavulana | 6 | 66.7 | 1 | 11.1 | 2 | 22.2 | 9 |
| Wasichana | 7 | 77.8 | 0 | 0 | 2 | 22.2 | 9 |
| Jumla | 13 | 72.2 | 1 | 5.6 | 4 | 22.2 | 18 |

Katika kauli hii, jumla ya wanafunzi waliokubaliana na kauli hii walikuwa 13 wakilinganishwa na jumla ya wanafunzi wote 18. Wavulana walikuwa ni 6 kwa jumla ya wote tisa. Wasichana walikuwa 7 kwa jumla ya wote tisa. Wavulana wawili na wasichana wawili hawakuwa na hakika. Mvulana mmoja alikuwa na mielekeo hasi, kwa kuwa hawakubalianiana kauli husika. Kwa mfano wavulana 6 kwa 9 mara 100%.

Asilimia ya wavulana ilikuwa na asilimia 66.7%, wasichana wakiwa 7 kwa 9 mara 100% wakiwa na asilimia 77.8%. Makundi haya mawili, wasichana na wavulana yalikuwa na zaidi ya kigezo cha asilimia 55%. Jumla ya wasichana na wavulana ilikuwa 13 kwa 18 mara 100% wakawa na asilimia 72.2% na kuweza kutimiza na kupitisha kiwango cha 55% kilichotengwa kama kigezo cha kutathiminia mielekeo. Mielekeo wa wasailiwa ni kuwa dawa za kulevya huwa na athari kwa watoto wanaozitumia. Wasichana walikuwa na asilimia ya juu kuliko wavulana. Kuna umuhimu wa kuwashauri na kauli waliyopewa. Asilimia 22.2% hawana hakika, kwa hivyo hawa

wakishauriwa wataweza kuwa na uhakika wa mielekeo watakao huchukua. Kuna uwezekano kuwa wavulana walikuwa na asilimia ya chini ya wasichana kwa kuwa wametagusana na wenzao wanaoshiriki matumizi ya dawa za kulevya na labda ndipo mmoja akawa na mielekeo hasi. Wavulana wanahitaji ushauri zaidi. Huenda wasichana wanachukia kushiriki dawa za kulevya kwa kuwa kijinsia utamaduni unawadunisha wakitumia mihadarati.

Jedwali 4: Kauli ya pili: Dawa za kulevya huchangia watoto wanaozitumia kuacha shule

| Jinsia | Mwitikio chanya | | Mwitikio Hasi | | Wasiokuwa na hakika | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | |
| Wavulana | 6 | 66.7 | | | 2 | 22.2 | 9 |
| Wasichana | 8 | 88.9 | | | 1 | 11.1 | 9 |
| JUMLA | 14 | 77.8 | | | 3 | 16.7 | 18 |

Utaratibu wa kupata asilimia ya jumla ya wasailiwa ilihesabiwa kwa kuchukua jumla ya wasailiwa wa jinsia zote kwa jumla ya 18 mara 100%. Ya jinsia ilikuwa jumla ya kila jinsia kwa tisa mara 100%. Jumla ya wasailiwa waliokubali kuwa dawa za kulevya huwafanya watoto wanaozitumia kuacha shule walikuwa 14 kwa jumla ya 18 mara 100% ambao ni asilimia 77.8%. Walipitisha kigezo cha mtafiti cha 55% wavulana walikuwa 6 kwa jumla 9 mara 100% ambao asilimia ilikuwa ni 66.7% ikiwa juu ya 55%. Wasichana walikuwa 8 kwa jumla ya 9. Wakiwa na asilimia 88.9 wakiwa juu zaidi mbali na kigezo cha 55%. Wavulana wawili ambao ni asilimia 22.2% na msichana mmoja ambaye ni asilimiia 11.1% hakuwa na hakika. Licha ya kuwa kiwango hiki kiko chini wanapaswa kuangaziwa na kushauriwa vizuri. Mpangilio wa kuwashauri hawa ambao hawana hakika uzidishwe zaidi ya hawa wengine kama wavulana.

Jedwali 5: Kauli ya Tatu: Watoto uhadaiwa kuingilia dawa za kulevya bila kujua athari zake.

| Jinsia | Mwitikio Chanya | | Mwitikio Hasi | | Wasiokuwa na hakika | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | |
| Wavulana | 5 | 55.6 | 2 | 22.2 | 2 | 11.2 | 9 |
| Wasichana | 6 | 66.7 | 3 | 33.3 | 0 | 0 | 9 |
| JUMLA | 11 | 61.1 | 5 | 27.8 | 2 | 5.6 | 18 |

Utaratibu wa kupata asilimia ya jumla ya wasailiwa ilihesabiwa kwa kuchukua jumla ya wasailiwa wa jinsia zote kwa jumla ya 18 mara 100%. Katika kauli ya tatu inaonyesha kuwa jumla ya wasailiwa 11 kwa 18 ndio walikubaliana na kauli kuwa watoto hujiingiza kwa dawa za kulevya kwa kuhadaiwa na bila kujua athari zake. Ilikuwa asilimia 61.1%. Kutokana na wasailiwa 11 kwa 18 mara 100% asilimia ya 61.1% imekaribiana na asilimia 55%. Kuna uwezekano wa kuwa watoto hawajui ni vipi wengi wanaingia katika uraibu wa dawa za kulevya. Katika hali halisi watoto wanapaswa kuelimishwa na kushauriwa kuhusu mbinu walanguzi wa dawa za kulevya wanazozitumia kuwalai watoto kushiriki ulanguzi wa dawa za kulevya na hatimaye wakawa watumiaji wa dawa za kulevya. Asilimia ya wavulana ni 55.6% kutokana na 5 kwa 9 mara 100% ikiwa karibu na kigezo cha 55%. Asilimia ya wasichana ni 66.7% kutokana 6 kwa 9 mara 100% ikiashiria kuwa wasichana huwa na mielekeo chanya. Mtagusana wa wavulana na wasichana katika jamii huenda uliwafanya kushiriki matumizi ya dawa za kulevya ndiyo jumla ya watano walikuwa na mielekeo hasi. Mpangilio wa ushairi ufanywe kwa wote.

Jedwali 6: Kauli ya Nne: Dawa za kulevya huchangia utovu wa nidhamu shuleni

| Jinsia | Mwitikio chanya | | Mwitikio hasi | | Wasiokuwa na hakika | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | |
| Wavulana | 9 | 100 | | | | | 9 |
| Wasichana | 9 | 100 | | | | | 9 |
| JUMLA | 18 | 100 | | | | | 18 |

Jumla ya wasailiwa walikuwa 18 kupata asilimia 18 kwa 18 mara 100% ikawa asilimia 100%. Wasailiwa wote kumi na nane walikubali kuwa dawa za kulevya huchangia utovu wa nidhamu shuleni. Mielekeo huu huenda ulichangiwa na tabia za wahusika wakuu watatu: Musa wa *Vioja vya Musa (2007)*, Sembuli wa *Atamlilia nani? (2009) na* Ajizi *wa Ah! Ajizi (2015).* Wahusika hao walikuwa na utovu wa nidhamu shuleni. Watoto wanapaswa kuhamasishwa kuhusu athari za dawa za kulevya zaidi ili wawe waangalifu.

Jedwali 7: Kauli ya tano: Dawa za kulevya zinaweza mfanya mtumiaji kufungwa jela

| Jinsia | Mwitikio chanya | | Mwitikio hasi | | Wasiokuwa na hakika | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | |
| Wavulana | 6 | 66.7 | 2 | 22.1 | 1 | 11.1 | 9 |
| Wasichana | 7 | 77.8 | 1 | 11.1 | 1 | 11.1 | 9 |
| Jumla | 13 | 72.2 | 3 | 16.7 | 2 | 11.1 | 18 |

Utaratibu wa kupata asilimia ya jumla ya ilihesabiwa kwa kuchukua jumla ya wasailiwa wa jinsia zote kwa jumla ya 18 mara 100%. Jumla ya wasailiwa 13 kwa 18 mara 100% walikubaliana na kauli husika. Jumla ya asilimia ni 72.2%. Asilimia hii iko juu ya kigezo cha 55% cha mtafiti. Wavulana wana asilimia 66.7%. Wasichana wana 77.8% kutokana na 7 kwa 9 mara 100%. Wavulana na wasichana wamepita kigezo cha mtafiti cha kutathimini mielekeo wa watoto kuhusu dawa za kulevya. Kuna asilimia 22.1% kutokana na 2 kwa 18 mara 100% iliyo na mielekeo hasi na silimia 11.1% hawana hakika. Kuwaonya watoto na kuwahamasisha kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya ni muhimu. Wavulana wanastahili kushughulikiwa katika kushauri kuhusu dawa za kulevya.

Jedwali 8: Kauli ya sita: Watoto wanaotumia dawa za kulevya huwa ni kero kwa walimu, wanafunzi, wazazi na jamii

| Jinsia | Mwitikio chanya | | Mwitikio hasi | | Wasiokuwa na hakika | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | |
| Wavulana | 8 | 88.9 | | | 1 | 11.1 | 9 |
| Wasichana | 8 | 88.9 | | | 1 | 11.1 | 9 |
| JUMLA | 16 | 88.9 | | | 2 | 11.1 | 18 |

Utaratibu wa kupata asilimia ya jumla ya wasailiwa ilihesabiwa kwa kuchukua jumla ya wasailiwa wa jinsia zote kwa jumla ya 18 mara 100%. Katika kauli hii jumla ya wasailiwa 16 kwa 18 walikubaliana na kauli kuwa watoto wanaotumia dawa za kulevya huwa ni kero kwa walimu, wanafunzi na wanajamii. Wasailiwa hao ni asilimia 88.9%. Asilimia ya wavulana na wasichana ilikuwa sawa, asilimia 88.9% kutokana na wasailiwa 8 kwa tisa mara 100%. Katika hali halisi shuleni kuna wanafunzi ambao ni kero kwa walimu, wanafunzi wenzao, wazazi na hata jamii. Huenda hali ndiyo ilicangia idadi kubwa kuunga mkono kauli kwa idadi kubwa. Wanahitaji ushauri na kuelimishwa dhidi ya athari za matumizi ya dawa za kulevya.

Jedwali 9: Kauli ya saba: Dawa za kulevya zina athari kubwa na zinapaswa kupigwa vita na kila mtu

| Jinsia | Mwitikio chanya | | Mwitikio hasi | | Wasiokuwa na hakika | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | |
| Wavulana | 8 | 88.9 | | | 1 | 11.1 | 9 |
| Wasichana | 8 | 88.9 | | | 1 | 11.1 | 9 |
| JUMLA | 16 | 88.9 | | | 2 | 11.1 | 18 |

Utaratibu wa kupata asilimia ya jumla ya wasailiwa ilihesabiwa kwa kuchukua jumla ya wasailiwa wa jinsia zote kwa jumla ya 18 mara 100%. Kauli ii ilivutia wasailiwa 16 kwa jumla 18 waliokubaliana na kauli hii. Wawili wakiwa hawana hakika. Asilimia ya waliokubaliana na kauli ilikuwa 88.9% kutokana na 16 kwa 18 mara 100%. Wavulana na wasichana walikuwa na asilimia 88.9% iliyotokana na 8 kwa 9 mara 100%. Wale hawakuwa na hakika ni 11.1% ikiwa ni 2 kwa 18 mara 100%. Wasailiwa wasiokuwa na hakika wakishauriwa watachukua hatua na kuwa na msimamo ambao unaweza kuwafanya wawe na mielekeo chanya. Huenda wasailiwa hawa waliathiriwa na hali walizokumbana nazo wahusika wakaangamia.

Jedwali 10: Kauli ya 8: Kuwa dawa za kulevya huwa na uraibu

| Jinsia | Mwitikio chanya | | Mwitikio hasi | | Wasiokuwa na hakika | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | |
| Wavulana | 5 | 55.6 | 2 | 22.2 | 2 | 22.2 | 9 |
| Wasichana | 6 | 66.7 | 1 | 11.1 | 2 | 22.2 | 9 |
| JUMLA | 11 | 61.1 | 3 | 16.7 | 4 | 22.2 | 18 |

Utaratibu wa kupata asilimia ya jumla ya wasailiwa ilihesabiwa kwa kuchukua jumla ya wasailiwa wa jinsia zote kwa jumla ya 18 mara 100%. Katika kauli hii wasailiwa 11 kwa umla 18 walikubaliana na kauli. Watatu wakiwa na mielekeo hasi na wanne hawakuwa na hakika. Asilimia ya wale waliunga mkono ilikuwa ni 61.1% na walikuwa na mielekeo hasi wakiwa ni asilimia 16.7% kinyume na wasiokuwa na hakika wakiwa na asilimia 22.2%. Washikadau wote wanapaswa kupambana na dawa za kulevya kwa kuwaelimisha na kuwashauri watoto mara kwa mara wasijiingize kwa uraibu wa dawa za kulevya. Matokeo haya huenda yalichagiwa na wasailiwa kutojua vizuri kama kuna

uraibu na unasababishwa na nini. Daktari wanapaswa kushirikishwa kuelezea kuhusu uraibu.

Jedwali 11: Kauli ya 9: Dawa za kulevya uharibu akili

| Jinsia | Mwitikio chanya | | Mwitikio hasi | | Wasiokuwa na hakika | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | |
| Wavulana | 6 | 66.7 | 3 | 22.2 | | | 9 |
| Wasichana | 7 | 77.8 | 2 | 11 | | | 9 |
| JUMLA | 13 | 72.2 | 5 | 27.8 | | | 18 |

Utaratibu wa kupata asilimia ya jumla ya wasailiwa ilihesabiwa kwa kuchukua jumla ya wasailiwa wa jinsia zote kwa jumla ya 18 mara 100%. Katika kauli hii wasailiwa 13 kwa jumla ya 18 walikubaliana na kauli hii, asilimia yao ikiwa 72.2% kutokana na kuwa 13 kwa 18 mara 100%. Wasailiwa watano ambao asilimia yao ilikuwa 27.8% kutokana na 5 kwa 18 mara 100% walikuwa na mielekeo hasi. Wavulana 6 kwa jumla ya 9 mara 100% wakiwa na asilimia 66.7% walikuwa na mielekeo chanya, nao wasichana 7 wakiwa ni asilimia 77.8% kutokana na 7 kwa 9 mara 100% walikuwa na mielekeo chanya. Elimu kuhusu athari za dawa za kulevya ni muhimu na itawasaidia kuwa na mielekeo chanya kuhusu dawa za kulevya. Kuna umuhimu kushirikishwa katika ushairi wa watoto.

Jedwali 12: Kauli ya 10: Dawa za kulevya huwafanya watoto kuipoteza ndoto yao ya siku za usoni

| Jinsia | Mwitikio chanya | | Mwitikio hasi | | Wasiokuwa na hakika | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | Mara tokezi | % | |
| Wavulana | 7 | 77.8 | 1 | 11.1 | 1 | 11.1 | 9 |
| Wasichana | 8 | 88.9 | | | 1 | 11.1 | 9 |
| JUMLA | 15 | 83.3 | 1 | 5.6 | 2 | 11.1 | 18 |

Utaratibu wa kupata asilimia ya jumla ya wasailiwa ilihesabiwa kwa kuchukua jumla ya wasailiwa wa jinsia zote kwa jumla ya 18 mara 100%. Kauli hii ilivutia wasailiwa 15 kwa jumla ya 18 waliokubaliana na kauli hii. Hawa asilimia yao ilikuwa ni 83.3% kwa kuwa 15 kwa 18% mara 100% ikilinganishwa na mmoja aliyekuwa na mielekeo hasi. Wasiokuwa na hakika walikuwa wawili. Asilimia ya waliokubali ni 83.3%

waliopinga ilikuwa ni 5.6% ikiwa 1 kwa 18 mara 100% nayo asilimia ya wasiokuwa na hakika ilikuwa ni 11.1% ikiwa ni 2 kwa 18 mara 100%. Watoto wanapaswa kuonywa, kuhamasishwa, kuelimishwa kuhusu athari za dawa za kulevya ili wawze kutimiza ndoto zao za siku za usoni. Ushauri kwa wavulana utakuwa muhimu kwa kuona wana mtoto mwenye mtazamo hasi.

Kulingana na hojaji ya mizani ya Likert, baada ya uchanganuzi wa majibu ya wasailiwa ni kuwa kwa jumla na katika maswali yote wasailiwa walikubaliana na kila kauli na kuwa na asilimia zaidi ya kigezo cha mtafiti cha asilimia 55%. Wavulana na wasichana wote katika kila swali walipata asilimia iliyokuwa juu ya kigezo cha mtafiti cha 55%. Ni muhimu kuhitimisha kwa kusema kuwa mielekeo wa watoto ni chanya. Watoto wanapaswa kutunzwa vizuri na kuelekezwa ili wasijiingize katika matumizi ya dawa za kulevya. Kuna wale wanaathiriwa na wana rika, mazingira wanamoishi hali ya kiuchumi miongoni mwa mengine. Wataalamu kama walimu na daktari wahusike kuwawekea watoto misingi ya maadili.

Wasailiwa walipangwa katika makundi matatu. Kila shule ilifanya kikundi kimoja walipewa maswali matano ya dodoso. Maswali ya dodoso yalikusudiwa kutathimini mielekeo wa wasailiwa kwa kuwapa nafasi ya kujieleza na kutoa mielekeo wao. Baada ya mijadala kila kundi lilipiga kura kwa misingi ya kukubali, kutokubali na kutokuwa na hakika. Mtafiti alihesabu asilimia ya kila kundi kuona kama lilitimiza asilimia 55% ambayo ni kigezo cha mtafiti cha kutathimini mielekeo.

Jedwali 13: Kura kuhusu Kuunga Mkono, Kupinga au Kutokuwa na Hakika

Jedwali hili linaonyesha jumla ya wanafunzi waliopiga kura katika kila swali. Katika kuhesabu asilimia yao, mtafiti alichukua jumla ya wasailiwa katika kila swali kuwa mara tokezi ingekuwa ni 30 kutokana na maswali yote matanona kila kundi lilikuwa na wasailiwa sita. Jumla ya mara tokezi kwa kila swali ndiyo ilitumika kutafuta asilimia ya jumla ya wasailiwa kutoka kila shule iliyochukuliwa kama kundi moja. Mtafiti alilenga kubaini mielekeo wa wasailiwa kwa kuangazia maswali ya dodoso na wala sio mielekeo wa jumla ya shule pamoja. Hii ndio sababu asilimia ya jumla ya shule haija shirikishwa.

| Swali | 1 | | | 2 | | | 3 | | | 4 | | | 5 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Shule | Chanya | Hasi | Hana hakika | Chanya | Hasi | Hana hakika | Chanya | Hasi | Hana hakika | Chanya | Hasi | Hana hakika | Chanya | Hasi | Hana hakika |
| Miomponi | 5 | | 1 | 4 | 1 | 1 | 6 | | | 6 | | | 3 | 1 | 2 |
| Karou | 6 | | | 3 | | 3 | 5 | 1 | | 6 | | | 2 | 1 | 3 |
| Premier | 5 | | 1 | 3 | 2 | 1 | 4 | 1 | 1 | 6 | | | 3 | 1 | 2 |
| JUMLA | 16 | 0 | 2 | 10 | 3 | 5 | 15 | 2 | 1 | 18 | 0 | 0 | 8 | 3 | 7 |


Shule ya Miomponi ilikuwa na waliounga mkono mara tokezi 24 ambao ni asilimia 80%. Kutokana hesabu ya 24 mara tokezi kwa jumla tokezi 30 tarajiwa mara 100%. Waliokuwa na mielekeo hasi walikuwa 2 kwa 30 mara 100% wakiwa na asilimia 6.7%. Katika kundi la wale wasiokuwa na hakika walikuwa 4 kwa 30 mara 100% wakitimiza asilimia 13.3.%. Kwa jumla kundi la Miomponi lilitimiza kigezo cha kuamua mielekeo wa wasailiwa kuwa ni chanya. Walikuwa na asilimia 80% ili kuendelea kudumisha mielekeo huu chanya, ni muhimu washauriwe vizuri.

Shule ya Karou ilikuwa na jumla ya wasailiwa 22 mara tokezi kwa jumla 30 mara tokezi iliyokusudiwa mara 100% waliounga mkono wakiwa asilimia 73.3%. Wasailiwa waliopinga walikuwa 2 kwa mara tokezi kusudiwa 30 mara 100% na asilimia yao ikiwa 6.7%. Kundi la wale hawakuwa na hakika lilikuwa na wasailiwa 6 kwa mara 30 mara 100% asilimia yao ikiwa 20% kwa jumla shule ya Karou ilipata asilimia 73.3% ambayo ni zaidi ya kigezo cha mtafiti cha kutathimini mielekeo wa wasailiwa ulikuwa chanya. Wazazi na walimu wawashauri na kuwaonya dhidi ya mihadarati ili waendelee kudumisha au kuboresha mielekeo wao.


Shule ya Premier ambayo ni ya kibinafsi ilikuwa na wasailiwa 21 Mara tokezi kwa 30 mara tokezi kusudiwa mara 100%. Waliounga mkono hii ikiwa ni asilimia 70%. Wasailiwa waliopinga walikuwa 4 ambao ni asilimia 13.3%. Wale waliokuwa hawana hakika walikuwa asilimia 16.7% ambayo iliwakilishwa na wasailiwa 5 kwa 30 mara 100%. Shule ya Premier waliweza kutimiza kigezo cha mtafiti cha 55% kwa kuwa na asilimia 70%. Mielekeo wao ni chanya. Mielekeo wa wasailiwa kuhusu mihadarati kutoka shule zote ni chanya. Kuwashauri, kuwaelimisha na kuwahamasisha watoto mara kwa mara kutawafanya wawe waangalifu kuhusu dawa za kulevya na kudumiasha mielekeo huo chanya au hata wauboreshe mpaka huimarike.

Michoro ya kuonyesha jumla ya mielekeo ya wasailiwa wa shule tatu kwa mujibu wa majibu yao kwa kila swali maswali matano kwa asilimia kuonyesha wametimiza kigezo cha mtafiti cha 55% cha kutadhimini mielekeo wao

Kielezo 1: Jumla ya maoni ya shule kwa ba grafu




Kielezo 2: Jumla ya maoni ya shule kuonyeshwa kwa pai chati




Kwa jumla utafiti huu ulitimiza lengo la utafiti kwa kuleta majibu yaliyodhihirisha mielekeo wa watoto kuhusu dawa za kulevya, kuwa ni chanya

**6.3 Hitimisho**

Katika sura hii, uchanganuzi wa hojaji ya mizani ya Likert na Dodoso ya mjadala wa makundi ulishughulikiwa ili kutathimini mielekeo wa wasailiwa kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya. Uchanganuzi huu umethihirisha kuwa wasailiwa wana mielekeo chanya. Suala la mielekeo kama linavyopendekezwa katika mhimili wa nadharia ya Mwitikio wa Msomaji ulijidhihirisha. Katika sura iliyofuata ilishughulikia muhtasari, matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo.

## SURA YA SABA

## MUHTASARI WA UTAFITI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

### 7.1 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia suala la hitimisho la utafiti huu. Masuala yaliyoangaziwa ni mukhtasari, matokeo ya utafiti na mapendekezo ya utafiti wa usoni kuhusu usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya katika fasihi ya watoto ya Kiswahili, matumizi ya dawa za taswira zilizotumiwa na waandishi kuelezea athari za dawa za kulevya, kuelezea athari za mihadarati na kubainisha mielekeo wa Watoto kuhusu dawa za kulevya.

### 7.2 Muhtasari

Utafiti huu ulichunguza usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya kwa watoto. Malengo ya utafiti yalikuwa ni; kufafanua aina za taswira zilizotumiwa na waandishi kuelezea usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya katika matini teule za Fasihi ya watoto, kueleza athari za matumizi ya dawa za kulevya kama zilivyosawiriwa katika matini teule za Fasihi ya watoto kutathimini mielekeo wa watoto ili waweze kushauriwa kuhusu dawa za kulevya. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani na nyanjani. Maktabani mtafiti aliteua matini ambazo zilishughulikia matumizi ya dawa za kulevya kwa watoto ili kuvisoma na kuvichambua. Matini teule ni riwaya za watoto za Kiswahili, *Vioja vya Musa* (2007), *Atamlilia nani? (2009)* Na *Ah! Ajizi* (2015). Umuhimu wa utafiti huu ulikuwa kuchangia maarifa ya kitaaluma katika Fasihi ya watoto. Maktabani mtafiti alizisoma matini teule na kuzichambua. Nyanjani, mtafiti aliwachagua watoto wasailiwa wakapewa matini teule wasomi ili wajifahamishe na maswali muhimu katika matini teule na kisha wajibu maswali ya hojaji kwa ufasaha kutokana na kuelewa kwao kwa matini teule.

Maswali ya dodoso ya kimakundi, hojaji za mizani ya Likert ilitumika kama vifaa vya kukusanya data kwa vile mtazamo ni wa kisaikolojia unahitaji vifaa zaidi ya kimoja ili wasailiwe wajieleze vizuri. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji. Nadharia hii ya Mwitikio wa Msomaji ilifaa kwa kuwa utafiti huu ulimhitaji msailiwa kusoma matini na hatimaye kupokea ujumbe na kuelewa vizuri. Msailiwa alijibu hojaji ya Mizani ya Likert. Mhimili mmoja wa nadharia ya Mwitikio wa Msomaji ulisisitiza kuwa msomaji wa matini huweza kuchukua hatua fulani baada ya

kuisoma matini. Wasailiwa waliweza kujibu maswali kama mojawapo ya hatua walichukua baada ya kusoma matini.

Tasnifu hii imegawika katika sura saba kwa jumla. Sura ya kwanza ni Misingi ya Utafiti, ilishughulikia Usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti sababu za kuchagua mada, upeo wa utafiti na maelezo ya istilahi zilizotumika katika utafiti huu.

Sura ya pili ilihusisha mwauo wa maandishi, maandishi kuhusu Fasihi ya watoto, dhana na dhima ya Fasihi ya watoto. Masuala haya yalishughulikiwa kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali. Tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya watoto ziliangaziwa ili kuonyesha mchango wake katika utafiti huu na tofauti zake. Sura hii pia iliangazia kiunzi cha nadharia iliyoongoza utafiti huu na muhtasari wa vitabu teule. Sura ya tatu ilishughulikia mbinu za utafiti, mpangilio wa utafiti, vifaa vya utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa data na maadili ya utafiti. Sura ya nne ni maelezo na ufafanuzi wa aina za taswira zilizotumiwa na waandishi wa matini teule. Mhimili wa picha za akilini zinazomjia msomaji anapoisoma matini, ilitumika kuongoza kuchanganua data katika sura. Picha zinazomjia msomaji akilini ndizo taswira. Mtafiti alishughulikia lengo la kwanza ambalo ni kufafanua matumizi ya taswira kueleza kusawiri dawa za kulevya.

Sura ya tano imeshughulikia athari za matumizi ya dawa za kulevya katika fasihi ya watoto. Mtafiti alizingatia mhimili wa Mwitikio wa Msomaji kuwa kuna athari fulani inayomwathiri msomaji akilini mwake baada ya kuisoma matini.

Sura ya sita iliangazia mielekeo wa watoto kuhusu dawa za kulevya. Sura ya sita iliongozwa na mhimili wa nadharia ya Mwitikio ya Msomaji kuwa msomaji wa matini huwa na mielekeo fulani baada ya kuisoma matini. Mtafiti alilenga kutathimini mielekeo wa wasailiwa. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha taswira hutumika kusawiri matumizi ya dawa za kulevya katika Fasihi ya watoto. Kuna athari za matumizi ya dawa za kulevya katika matini za watoto katika Fasihi ya watoto. Mwisho ni kuwa mielekeo wa watoto ni chanya. Data baada ya kuchanganuliwa imewasilishwa kwa njia ya

maelezo na majedwali. Sura ya saba ilihitimisha kwa kutoa muhtasari, matokeo ya utafiti na mapendekezo ya utafiti wa usoni.

**7.3 Matokeo ya Utafiti**

Mifani ya athari za dawa za kulevya kama zilivyodhihirika matini teule *Vioja vya Musa* (2007), *Atamlilia nani?* (2009) na *Ah! Ajizi* (2015). Wafula na Kimani (2007) wanasema matendo ya wanajamii katika kila jamii humlikwa kwa milengo miwili. Yale mema yanayokubalika yanayopaswa kuigwa na yale mabaya yanayopaswa kupingwa. Mhusika Musa katika *Vioja vya Musa* (2007) alikuwa mfitini aliyezusha fujo uwanjani Kaachonjo na kuleta vita vikali. Alikamatwa kwa tuhuma ya wizi. Sembuli naye alikuwa na hasira iliyomplekea kumgongea mama mlango kwa hasira. Alimfokea mamake na kumfanyia vitimbi hadharani, kumlazimisha kumpikia. Alikuwa mwizi, tapeli mwizi wa kimabavu na mbakaji. *Atamlilia nani?* (2009). Ajizi alikuwa mwizi, mchokozi na mbakaji. *Ah! Ajizi* (2015). Haya yote yalisababishwa na dawa za kulevya.

Kwa mujibu wa WHO ni kuwa watoto wanaotumia mihadarati wanaishi na athari za kiafya. Casey, B. J. na wenzake (2008) wanaeleza kuwa akili ya watoto wachanga huathiriwa na dawa za kulevya. Musa baada ya kumaliza kifungo alikuwa ameharibika akili kabisa na ndipo alionekana kama mtu aliyezubaa. Alikataa shule katakata. *Vioja vya Musa* (2007). Sembuli akili yake ilipoharibika alianza kuwachokoza vilema, vichaa kuwafitini watu wote. Sembuli aliwaharibia watu vitu vyao ovyo ovyo. Akawa na hasira kuu. Aliwapiga mbwa, paka na ndege ovyo ovyo na bila sababu. *Atamlilia nani?* (2009). Ajizi alikuwa kaathirika kiafya. Ikawa hali yake ilikuwa imedhoofika sana. Bangi ilimfanya kapagawa akawa anapiga kamsa kote kijijini. Akawa mbakaji. Hatimaye akaaga dunia kama alivyo eleza mwandishi wa *Ah! Ajizi* (2015)

Uchunguzi wa Marekani mjini Washington (2012) wanasema kuwa watoto wanaotumia pombe na bangi uathirika zaidi kiakili, huacha shule kwa kupata alama za chini na kukosa motisha na bidii shuleni. Matini teule zimesawiri watoto walioathiriwa na dawa za kulevya na wakalemewa kimasomo hadi wakaacha masomo. Musa alikuwa mwenye bidii na aliongonza kwenye darasa lao. Alipoathiriwa na bangi hakuendelea tena masomoni. *Vioja vya Musa* (2007). Sembuli naye aliacha shule angali mtoto mdogo kwa kuadhiriwa na bangi. Atamilia nani? 2009. *Ah! Ajizi* (2015) alipoathiriwa

na bangi alikuwa mkatili, akawa si Ajizi aliyekuwa akiongoza hapo mbeleni sasa. Ajizi aliacha shule na kutorokea msituni.

Kwa mujibu wa mtandao wa Washington State Health Youth Servey (2012) watoto wanaoutumia bangi huwa ni waasi na huwa na matendo yanayoweza kuwatia hatarini. Musa alianzisha matumizi ya bangi na kuanza kuiuza. Uuzaji wa bangi ni hatari na ni haramu. Alikuwa kwa kundi lililoiba nyanya wakakamatwa. Musa walizusha vita ugani Kaachonjo mpaka wakafungwa jela. *Vioja vya Musa* (2007). Sembuli alikuwa na vitendo vingi vibaya vya wizi, utapeli, uharibifu wa mali ya watu na ubakaji. Polisi walikuwa wanamtafuta wamtie kwa jela. *Atamlilia nani?* (2009).

Meier M.H na wenzake (2020) wanaeleza kuwa watoto wanaokuwa na uraibu wa matumizi ya bangi huwa na upungufu wa kiakili wanapostawi. Hard na wenzake wanasema watoto wanaoweza kutumia mihadarati mapema huwa na uraibu ambao unamweka hatarini ya kujikuta katika majanga. Musa mhusika mkuu katika *Vioja vya Musa* (2007) Baada ya kuwa mraibu anaona hawezi kurudi shuleni tena. Anakuwa mlevi wa pomba na bangi kupindukia. Fedha alizozipata kutokana na kazi ya uhamali ziliishia kwa pombe hadi yeye mwenyewe akahuzunika. Wazazi walihuzunika alipokamatwa na kufungwa jela. Sembuli aliangaika sana kwa kuwa mraibu wa mihadarati. Alipotimliwa katika genge la U-gangster hakupata fedha za kununulia bangi. Sembuli alihuzunika sana kukosa bangi. Aliona kifo kwa macho. Familia yake ilihuzunika sana alipolemazwa na barubaru katika mkahawa Hollywood na risasi ya babake alipotaka kumwibia pesa zake. *Atamlilia nani?* (2009), Ajizi alikuwa mraibu wa pombe. Uraibu huu ulimpelekea kupagwa hadi kufa kwake. Kifo chake kilisababisha huzuni kwa aila yao na kanisa la Mungu kwa jumla. *Ah! Ajizi* (2015).

### 7.4 Hitimisho

Utafiti huu ulichunguza usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa watoto katika matini teule za Fasihi ya watoto ya Kiswahili. Utafiti huu uliweza kuthibitisha kuwa matini za Fasihi ya watoto zilishughulikia usawiri wa matumizi ya dawa za kulevya na kuelezea athari za matumizi ya dawa za kulevya katika Fasihi ya watoto. Utafiti huu pia umeweza kuthibitisha kuwa taswira zinaweza kutumiwa kuelezea athari za matumizi ya dawa za kulevya. Utafiti huu uliweza kushibitisha kuwa

watoto wana mielekeo chanya kuhusu dawa za kulevya. Utafiti huu ulidhihirisha umuhimu wa kuendeleza utafiti dhidi ya watoto na hasa katika nyanja hii ya dawa za kulevya.

### 7.5. Mapendekezo

#### 7.5.1 Mapendekezo ya Kushughulikia athari za matumizi ya dawa za kulevya

Ni muhimu kuwa na mikutano ya kuwahamasisha watoto na washika dau wote kuhusu dawa za kulevya. Shirika la NACADA linapaswa kushirikiana na wazazi, watoto, walimu, viongozi wa serikali na wa kidini kupanga semina, warsha na kongamano za mara kwa mara kote nchini. Kuwaelimisha watoto kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya ili waweze kujua athari zake na kuepukana nazo. Kuwe na mpangilio wa kuwahusisha watoto wa shule za msingi na sekondari kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya, kupitia nyimbo, mashairi, michezo ya kuigiza, hotuba na filamu na semina zinazoonyesha watoto walioathiriwa na dawa za kulevya. Shuleni, somo la dawa za kulevya lizingatiwe kwa makini kuanzia chekechea hadi shule ya upili. Kanisani wahubiri na wanaofunza watoto kanisani wazingatie mpangilio wa kuwahusisha watoto kuigiza athari za matumizi ya dawa za kulevya. Serikali inafaa kutangaza dawa za kulevya kama janga la kitaifa na kutenga fedha za kuzipiga vita dawa za kulevya. Dawa za kulevya zisipopigwa vita watoto na vijana wataangamia.

Wazazi, walezi wa watoto na walimu wanapaswa kuwa na mwongozo dhabiti wa kuzingatia katika kuchunguza iwapo mtoto anashiriki matumizi ya dawa za kulevya. Mwongozo huu unapaswa kuwa na njia mwafaka za kuwasiliana na watoto kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya. NACADA inapaswa kuwa na kipindi cha kuwaelimisha watoto kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya, kwenye runinga na redio siku ya Jumamosi au Jumapili wakati watoto wamo nyumbani. Pia kunapaswa kuwa na kanda za video zinazoonyesha watoto walioathiriwa na matumizi ya dawa za kulevya. Kanda hizi zionyeshwe shuleni, kanisani na kwenye semina na warsha au kongamano za kufunza watoto kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya.

#### 7.5.2 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye

Mtafiti ameshirikisha matini tatu za Kiswahili za fasihi ya watoto ambazo ni *Vioja vya Musa* (2007), *Atamlilia nani?* (2009) na *Ah! Ajizi* (2015) ambazo ni matini

zilizoandikwa na waandishi tofauti tofauti. Nadharia ya Mwitikio wa Msomaji ilitumika. Malengo matatu ya utafiti yalishugulikiwa. Utafiti wa baadaye unaweza kufanywa ukitumia matini tofauti kuchunguza usawiri wa dawa za kulevya kwa kutumia nadharia tofauti na iliyootumiwa na mtafiti wa utafiti huu. Utafiti wa baadaye unaweza kufanywa kwa kutumia hadithi fupi, tamthilia, ushairi na riwaya kulinganisha mwingiliano wa matini kuhusu usawiri wa dawa za kulevya katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Utafiti wa baadaye unaweza kufanywa kwa kuwahoji watoto nyanjani bila kusoma matini yoyote kupata kufahamu kwao kuhusu matumizi ya dawa za kulevya na athari zake. Utafiti wa baadaye unaweza kufanywa kuhusu mabadiliko miongoni mwa watoto kuhusu mielekeo wao dhidi ya dawa za kulevya.

## MAREJELEO


Abrahams, R. (1999). Emotional Intelligence in Organizations: A Conceptualization. Genetic, Social and General Psychology Monographs 125 (2), 209-224

Akinyemi, A. (2003). Yoruba Oral Litreture; A Source of Indigenous Education for Children.In Akin Oyatede (ed). *Journal of African studies.* Volume 2 Dec 2003

Akinyi, D. (2017). Upokezi wa Hadithi za Fantasia Miongoni mwa Watoto wa Shule za Msingi, Tasnifu za Umachiri za Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Akinyi, D. (2017). *Upokezi wa Hadithi za fantasia miongoni mwa watoto wa shule za msingi,* tasnifu za Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Alembi, E. (1991). An Analysis of Style and Social significance of the Abanyole children's Oral Poetry.M A. Thesis. Kenyatta University.

Bakize, H. (2013). Changamoto zinazokabili Fasihi ya Watoto Tanzania katika Kiswahili, Juz, 76, Daressalaam; Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Kuv. 61-70

Bakize, L. (2013). *Changamoto zinazikabili fasihi ya watoto Tanzania katika Kiswahili*, Juz, 76, Dar es Salaam; *Taasisi ya Taaluma za Kiswahili kur*.61-70

Bleich, D. (1978). *Subjective Criticism*. Baltimore: Johns Hopkins Up, Bloomington: Indian University Press.

Brunner, J. (2003). Making stories, .Law, literature, life, Cambridge, London: Harvard university press.

Casey, B., Jones R., & Itare T. (2008). The adolescent brain. Ann. N.Y Acad. Sci.; 1124:111-126.

Cianciolo, P. (1981). *Yesterday comes alive for readers of historical fiction*" katika language Arts, Juz.58, No 4, *Children's literature, national council of teachers of English* kutoka http://www.jstor.org/stabble/41961351, ilisomwa tar.06/7/2019. Kur 452-462.

CODE, (2015) "Reading code; Assessing a comprehensive readership intitiative in Tanzania," Kutoka www/academia. Edu/:/reading code assessing a comprehensive readership ililosomwa 13/5/2016.

Crystal, D., & Davy, D. (1969). Investigating English Style, I[st] Edition, Indian University Bloomington; London publisher

Cuddon, J. (2013) "A Dictionary of Literature Terms and Literary Theory" Fifth Edition, John Weley & Sons, Ltd. Publication.

Deaton, M. (1946) "Learning the time concept through historical/fiction". Katika the elementary English review Juz 23, Na? National Council of Teachers of English, http.www. Jstor. Org/Stable 1382950, ilisomwa tar.06 112/2004, Kur, 301-303.

Erickson, J. (1994), "The truth of historical fiction. Researching Osseo senior high". The English journal, Jaz…28, Naz National council of teachers of English tt://www jstor. Org/stable 115, Ilisomwa tar. 06/12/2014 Kur 36-39.

Eysenk, H. (1947) Mundo wa Binadamu. New York, NY: John Wiley NA Wanaume., Inc.

Fish, S. (1972). *Is There a Text in This Class?* The Authority of Interpretive Communities.Berkley California Up,

Freeman, E., &. Levstik, L. (1988). "Recreating the past: Historical Fiction in the social studies curriculum," Katika the elementary school journal Juz 88 na 4 kutoka http://www.jstor.org/stable 100/686 ilisomwa tar 06/12/2014 kur 329-337.

Halliday, M. (1978). *Language as social semiotic.* The social interpretation oF language and meaning. London; Edward Arnold.

Hannah, R., & May, R. (2019). '*Substance Use*". Published online at Our World in data.

Haviland, V. (1973). *Children and Literature views and reviews*, London: the bodley head Ltd.

Holland, N. (1975). "Unity, Identity Self the Dynamics of Literary Response." *PLMA*.90.5813-22

Hunt, P. (1994). An Introduction to Children Literature. New York: Oxford University Press

Hunt, P. (1994). *An Introduction to Children Literature*. New York: Oxford University Press.

Hurd Y., Michaelides, M., Miller M., & Jutras-Aswad, D. (2014). Trajectory of adolescent cannabis use on addiction vulnerability. Neuropharmacology. 2014; 76 Pt B:416 -24.

Jahoda, M., & Warren, N. (1966), *Attitudes.* Penguin Books: h.m.

Kairu, W. (2005). *Uhalisia na mtindo wa Ken Walibora katika fasihi ya watoto*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kanake, J. (2013) Makosa ya Kifonolojia Miongoni mwa Wanafunzi wa Kiigembe katika Ujifunzaji wa Kiswahili. Shahaday ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kapele, H. (2013). Uwanja wa Kiswahili: Fasihi Simulizi. Daressalaam

Karuga, M. (2005). Uhakiki na Upokezi wa Fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika Shule ya Msingi Nchini Kenya.Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Katiba ya Kenya (2010). *Government printers*. Nairobi

Kavuria, P. (2008). Dhuluma Dhidi ya watoto katika Riwaya za Kiswahili.tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta.

King'ei, K., & Kemoli, A. (2001) *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Limited

Leech, G., & Short, M. (1969). *English Grammar for Today*; New Introduction.

Lemon, N. (1973). *Attitudes and Their Measurement*. B.T. Batsford Ltd.: London.

Lyimo, E. (2014). Usaguzi wa kijinsia katika vitabu vya Kiswahili vya fasihi ya watoto na mielekeo wa wadau nchini Tanzania Tasnifu ya Uzamivu Chuo Kikuu Dar es Salaam.

M'Nganithi, T. (2008*). Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mahochi, E. (2005), Mielekeo ya wanafunzi kuhusu lugha ya Kiswahili na athari zake katika matokeo ya mtihani wa kiswahili wa kidato cha nne katika mikoa ya Pwani na Nyanza, Kenya. Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Egerton.

Matei, A. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi kwa Shule za Upili*. Nairobi University Press.

Matundura, B. (2007). Taswira Dumifu za Uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto. Tasnifu ya Umahiri. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Matundura, E., Kobia, J., & Mukuthuria, M. (2013). "*Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya watoto*", katika Mulika, Na, 32, Dar es Salaam; Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Kur, 28-47.

Mbatiah, M. (2002). *Kamusi ya Fasihi*: Nairobi: Standard Textbooks.

Mbuthia, E. (2005). *A Thematic and stylistic Analysis of Kiswahili*.Thesis Novel in Tanzania.Tasnifu ya Umahiri Chuo Kikuu cha Nairobi.

Meier M., Caspi, A., & Ambler, A., et al (2012). Persistant Cannabis users show Neurophychological Decline from Childhood to Midlife. Proc. Nat L. Acad. Sci. U.S.A 2012: 109 (40) E 2657-64

Mogambi, H. (2007). *Vioja vya Musa*, Nairobi*;* Moran (E.A) Publishers Limited

Mohamed, S. (2009). *Atamlilia nani?* Nairobi. Oxford University Press

Mohammed, S. (1995). *Kungu za Nathari ya Kiswahili*; Riwaya, Tamthilia na Hadithi fupi. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mpesha, N. (1996). *Children's Literature in Tanzania*. A literary appreciation of its growth and development. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi Nairobi*: East African Educational Publishers.

Mtandao wa Navigation (    ) Aina mbalimbali za dawa za kulevya na athari zake.

Mugenda, O., & mugenda, A. (2003). Research Methods: Quantitative and Qualitative Approach es Nairobi; Africa Center for Technology Studies (ACTS) Press

Mugenda, O., & Mugenda, A. (2003). *Research Methods; Quantitative and Qualitative approaches Nairobi*; Africa Centre for Technology Studies (ACTS) Press.

Muleka, J. (2001). *The Portrayal of Girl Characters in Selected Children's Books in Kenya*, MA Thesis Kenyatta University.

Muriungi, C. (2006). *Emerging trends in Kenya Children's fiction: A study of Sasa Sema's Lion Books*. Published, PhD. University of Witwatersr and. Johannesburg.

Mutahi, M., & Mbuthia, E. (2017). The Impact of the Depiction of Children in Selected Swahili Children Stories; Vol 4 no. 1

Mutembei, A. (2013). Hali na Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili katika Tanzania, Daressalaam.

Muthubi, F. (2005). *Mikakati na Mbinu za usilimishwaji katika fasihi ya watoto*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mwanzi, Helen (1982). *Unpublished thesis an Analysis of Children's Prose Fiction* University of Nairobi. Print.

Nandi, M. (2019) Ubainishaji wa Fonimu za Kikisa katika lugha ya Kiswahili sanifu.

Nandia, M. (2019). Ubainishaji wa Fonimu za Kikisa katitka Lugha ya Kiswahili Sanifu.

Nawrot, K (1996). "*Making connnections with historical fiction".* The clearing house Juz, 69.

NCB (2020) Urabiu wa madawa ya kulevya na pombe kwa watoto na barubaru watia hofu.

Ngugi, P (2009). *Language and literaly Education.* The state of children literature in Kiswahili in Primary Schools in Kenya.Tasnifu ya Uzamivu ya Chuo Kikuu cha Vienna.

Ngugi, P. (2011) Ufundishaji wa Fasihi ya watoto katika shule za msingi Nchini Kenya: Katika kioo cha lugha.

Ngugi, P. (2014) "Hatua za maendeleo katika tafiti zilizofnywa katika Idara ya Kiswahili: Mfano kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta". Makala yaliyowasilishwa katika kongamano la Chakama, lililofanyika katika chuo kikuu cha Rongo Kenya. Tarehe 13-1, Mei 2014.

Ngugi, P. (2014) Fasihi ya watoto katika kutekeleza mahitaji ya kisaikolojia ya mtoto," Katika Kiswahili, Juz. 77 Dar es Salaam: Tacesisi ya Taaluma za Kiswahili Kur 170- 180.

Ngugi, P. (2016). Usawiri wa Masuala ibuka katika Fasihi ya Watoto Mfano: Kutoka Kenya katika Mulika na 3. Daressalaam, Taasisi ya Taaluma

Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa shule za Sekondari*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Njogu, K. (2007). *Ufundishaji wa Maswala*–ibuka katika shule za nchini Kenya katika Kiswahili na Elimu nchini Kenya. Nairob. Twaweza communication 11-23.

Njogu, K., & Chimerah, R (1999) Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na mbinu, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkata, D. (2001). *Continiuty and Change in Story Telling: Childrens stories in Uganda past and present.* Papers presented at the 15th IRSCC Biennial conference: Warmbatha South.

Nyaga, F. (2017). *Itikadi za kisiasa katika vitabu teule vya fasihi ya watoto ya Kiswahili*.Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuuu cha Chuka.

Nyambeka, T. (2015). *Ah! Ajizi.* Storymoja Publishers Nairobi

Odaga, A. (1985). *Literature for children and young people in Kenya*. Nairobi, Kenya Literature Bureau of Systematic Reviews. J Adolesc Health. 2016 Oct; 59 (4 Suppl): 561-575, doi:10, 1016 IJ. Jado health 2018: 06:021.

Ohly, R. (1985). *Literature in Swahili in Andrejew S, pilaszewics, tyloch*, literature in African language theoretical issues and sample surveys Wiedzapowszechna, varsa via cambriindge university press.

Osazee, F. (1991*)*. Childrens' Literature Research in Africa problems and prospect. In saur K.G (ed) *Childrens Literature Munchen International Resources and exchange*.

Oskamp, S. (1991). *Attitudes and Opinions*. Prentice Hall: Englewood Cliffs, New Jersey.

Phelan, J. (2005) Living to tell it. A Rhetoric and Ethics of Character Narration. Ithaca & London: Cornell University Press.

Rosenblatt, L. (1978). *The Reader, The Text, The Poem: The Transactional Theory for theLiterary Work*. Carbondale, Il: Southern Illinois Up

Rycik, M., & Roseir, B. (2009) The return of historical fiction, the reading teacher, Juz, 2: Wiley, katika http://www.sto.org/stable, 140347997, ilisomwa tar.06/12/2014 Kur 163-166.

Senkoro, F. (1982). *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Stephen, J. (1992). *Language and Ideology in Childrens fiction*. New York: Longman.

Sumara, D. (1996). *Private Readings in Public: Schooling the Literary Imagination.* New York: Peter Lang.

Sutherland, R. (1985). Hidden Persuaders Politic Ideologies in Literature for Childrens published in childrens literature in education, vol.16.No 3: Agatton Press Inc. *The Journal of Adolescent Health Interventions for Adolescent Substance Abuse:* An Overview.

The Republic of Kenya (2001). *The Hansard.* Nairobi. Government of Kenya Printers.

Tonui, K. (2010). *Portrayal of HIV/AIDS in selected childrens story in Kenya* tasnifu ya Umahiri Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Transforming our World, (2015). *The 2030 Agenda for Sustainable Development Goals*.

Tucker, N. (1991). *The Child and the Book: Apsych Logical:* Cambridge University Press. United Nations New York.

Tuki (2000) English- Swahili Dictionary. Second Edition. Daves Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: focus Publications Ltd.

Wamitila, K. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi; Focus Publication Ltd.

Wizara ya Elimu na Teknolojia, (2002). Masuala Ibuka Katika Kuandika Fasihi ya Watoto Government Printers Nairobi Kenya.

World Drug Report (2017). 29.5 Million People globally suffer from drug use disorders, UNODC Research. Vienna Austria.

World Drug Report (2018). Executive summary Conclussions and Policy Implications:

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho 1: Hojaji ya Wanafunzi (Mfumo wa Likert)

Jina la Shule ____________________ Jina la Mwanafunzi ____________________

Darasa ____________________ Jinsia ____________________

**Unatakiwa uonyeshe mielekeo wako kuhusu athari za matumizi ya dawa za kulevya katika fasihi teule ya watoto. Utarejelea matini teule, *Vioja vya Musa* (2007. *Atamlilia nani?* (2009) na *Ah! Ajizi* (2015)**

**Maelekezo**

Eleza mielekeo wako wa dhati kuhusu dawa za kulevya.

Tumia alama [√] kuonyesha jibu lako

**Tafadhali onyesha msimamo wako hukusu kauli zifuatazo kwa kuweka alama ya** [√] **katika jibu ulilolichagua**

1. Dawa za kulevya huwa na athari nyingi kwa watoto wanaozitumia.
   Nakubali kabisa __________ Nakubali _________ Sina Hakika _____________ Sikubali ________________ Sikubali kabisa ____________.

2. Matumizi ya dawa za kulevya yanachangia watoto wanaozitumia kuacha shule na kushindwa kuendelea na masomo. Nakubali kabisa __________ Nakubali___________ Sina Hakika ______________Sikubali ____________Sikubali kabisa _____________

3. Watoto wengi hujiingiza katika uraibu wa matumizi ya dawa za kulevya kwa kuhadaiwa bila kujua athari zake. Nakubali kabisa _________ Nakubali ___________ Sina Hakika _________Sikubali _________Sikubali kabisa _________

4. Matumizi ya dawa za kulevya huchangia pakubwa utovu wa nidhamu miongoni mwa watoto wanaozitumia. Nakubali kabisa _________ Nakubali _________ Sina Hakika _________Sikubali _________ Sikubali kabisa _________

5. Matumizi ya dawa za kulevya huchangia kufungwa jela kwa watoto wanaozitumia. Nakubali kabisa________ Nakubali_________Sina Hakika _________Sikubali _________Sikubali kabisa _________

6. Watoto wanaotumia dawa za kulevya huwa ni kero kwa walimu, wanafunzi, wazazi na jamii kwa jumla. Nakubali kabisa ________ Nakubali________ Sina Hakika ________Sikubali ________Sikubali kabisa ________

7. Kwa kuwa dawa za kulevya zina athari nyingi kwa watoto wanaozitumia, zinapaswa kupigwa vita na kila mtu. Nakubali Kabisa ________Nakubali________Sina Hakika ________Sikubali ________ Sikubali Kabisa________

8. Dawa za kuilevya zinawafanya watoto kuwa waraibu wake. Nakubali Kabisa ________Nakubali ________ Sina Hakika________Sikubali ________Sikubali Kabisa________

9. Dawa za kulevya uharibu akili ya watoto wanaozitumia na kuwafanya wasiwaze vizuri. Nakubali Kabisa ________ Nakubali________Sina Hakika ________ Sikubali ________Sikubali Kabisa________

10. Matumizi ya dawa za kulevya huweza kumfanya mtoto kuipoteza ndoto yake ya siku za usoni. Nakubali Kabisa ________ Nakubali ________Sina Hakika ________ Sikubali ________Sikubali Kabisa________

**Kiambatisho 2: Dodoso ya Wanafunzi ya Mjadala**

1. Jadili maisha ya mhusika Musa katika *Vioja vya Musa* (2007) alipoanza matumizi ya bangi na utoe maoni yako kuhusu dawa za kulevya kama bangi kwa watoto
2. Sembuli katika matini ya *Atamlilia nani?* (2009) alibadilika sana alipoanza kutumia mihadarati. Jadili mabadiliko hayo na utoe maoni yako kuhusu dawa za kulevya
3. Mhusika *Ah! Ajizi* katika *Ah! Ajizi* (2015) alikuwa mtoto mwenye bidii masomoni. Jadili mabadiliko yaliyotokea baada ya kuanza kutumia mihadarati na utoe maoni yako kuhusu dawa za kulevya
4. Kulingana na tabia za wahusika Sembuli, Musa na Ajizi dawa za kulevya ziachiliwe ziendelee kutumika? Ndio ___________ au zipigwe vita _____________. Jadili maoni yako kuhusu mihadarati.
5. Jadili ni vipi dawa za kulevya ambazo zimegeuka kuwa hatari katika jamii zinaweza kukabilianwa nazo

## Kiambatisho 3: Kibali cha Utafiti

REPUBLIC OF KENYA

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION**

Ref No: **815519**

Date of Issue: **23/March/2020**

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. CYPRIAN KITHINJI MBEERE of Chuka University, has been licensed to conduct research in Tharaka-Nithi on the topic: USAWIRI WA DAWA ZA KULEVYA KATIKA MATINI TEULE ZA FASIHI YA WATOTO. for the period ending : 23/March/2021.**

License No: **NACOSTI/P/20/4160**

**815519**

Applicant Identification Number

Director General

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.